

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Sita – Tarehe 12 Septemba, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Nane, leo ni kikao cha Sita. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mhe. Rehema Juma Migilla

**SPIKA:** Katibu.

**DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Saba wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria nne zifuatazo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Bill, 2017*];

(ii) Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa mwaka 2017, [*The Natural Wealth and Resources Contacts Review and Renegotiation of Unquestionable Terms Bill, 2017*];

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2017, [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments), 2017*]; na

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017, [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2017*].

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kuliharifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari miswada hiyo imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi zinazoitwa:-

(i) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili (Na. 5) ya mwaka 2017, [*The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act, No. 05 of 2017*];

(ii) Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Maliasili za Nchi (Na. 6) ya mwaka 2017, [*The Natural Wealth and Resources Contacts Review and Renegotiation of Unquestionable Terms Act, (No. 6) of 2017*];

(iii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 7) ya mwaka 2017, [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, (No. 7) of 2017*]; na

(iv) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) ya mwaka 2017, [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, (No. 8) of 2017*].

Katibu.

**DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria na Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2017*].

**MHE. RASHID A. SHANGAZI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria na Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2017*].

**MHE. KASUKU S. BILAGO – K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2017*].

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 67

**Kituo cha Afya Mtina**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna vituo vitatu vya afya. Kituo cha Afya Mtina kina zaidi ya miaka 30 hakijafanyiwa ukarabati na pia hakuna wodi ya wazazi.

Je, ni lini Serikali itajenga wodi ya wazazi katika kituo hicho na kufanya ukarabati ili kiweze kutoa huduma bora kwa wakazi wa vijiji vya Nasya, Semeni, Nyerere, Angalia na wakazi wa kata ya Mchesi na Lukumbule?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na nguvu za wananchi imekamilisha ujenzi wa zahanati sita za Njengi, Mwenge, Tuwemacho, Nasumba, Semeni na Kazamoyo ambazo zimeanza kutoa huduma.

Aidha, nampongeza Mbunge wa Jimbo kwa kuweka kipaumbele na kutumia shilingi milioni 6.2 kwa ajili ya ukarabati wa chumba cha kujifungulia na chumba cha kuhifadhia maiti katika kituo cha afya Mtina.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaweka kipaumbele na kuhakikisha fedha zinatengwa kupitia Halmashauri katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha afya Mtina kinakamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate, swali la nyongeza, nimekuona.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu aliyotoa Naibu Waziri, lakini Jimbo langu la Tunduru Kusini vituo vyake vya afya vimechakaa na vina hali mbaya na vina matatizo lukuki pamoja na uhaba wa wafanyakazi,hakuna gari, wala chumba cha upasuaji.

Swali langu, ni lini Serikali itahakikisha vituo hivi vya afya vinapata watumishi wa kutosha ili viweze kuhudumia wananchi wa Tunduru?

Swali la pili, katika kampeni ya uchaguzi mwaka 2010, Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga kituo cha afya katika Mji wa Nalasi ambao una zaidi ya watu 25,000. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii ya kujenga kituo cha afya pale Nalasi ili kuweza kuwahudumia wananchi wale ambao wako katika vijiji sita katika Mji ule wa Nalasi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kuongeza watumishi, Serikali hivi sasa iko katika mchakato wa kuajiri watumishi mbalimbali. Katika hilo Jimbo la Tunduru tutalipa kipaumbele katika suala zima la mgawo wa watumishi kwa sababu Tunduru ina changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili nashukuru Mheshimiwa Mpakate alini-*accompany* vizuri sana wakati nimeenda katika Jimbo lake. Ni kweli watu wasiojua Tunduru, ukitoka barabarani mpaka Jimbo la Mheshimiwa Mpakate kuna changamoto kubwa sana. Ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge alipoleta *request*, tukaamua kipaumbele cha

kwanza twende tukamjengee kurekebisha Kituo cha Afya cha Mkasare.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba leo ninavyozungumza tayari tumeshaingiza shilingi milioni 500 kwa ajili ya kituo kile. Katika kituo kile tutajenga jengo la upasuaji, *mortuary*, wodi ya wazazi na tutafanya ukarabati mwingine halafu tutawawekea vifaa. Vilevile eneo hili la pili tutaliangalia kwa sababu lengo letu kubwa ni wananchi wa Tunduru waweze kupata huduma nzuri ya afya kwa sababu tunafahamu Wilaya ya Tunduru kwa jioografia yake, changamoto ya afya ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mpakate kwamba ahadi na maombi yake tulipokuwa katika mkutano, tumeyatekeleza na tunaendelea kuyafanyia kazi kwa kadri iwezekanavyo.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda.

Na. 68

### **Madai ya Walimu ya Kusimamia Mtihani**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa walimu madai yao ya kusimamia mtihani wa kidato cha nne mwaka 2015 na mtihani wa kidato cha pili mwaka 2016?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, walimu waliosimamia mthani wa Taifa wa kidato cha nne mwaka 2015 wanadai jumla ya shilingi bilioni 1.6 na walimu waliosimamia mitihani ya kidato cha pili mwaka 2016 wanadai jumla ya shilingi bilioni 3.2. Hivyo, jumla ya madai kwa mitihani yote miwili ni shilingi bilioni 4.89.

Mheshimiwa Spika, madeni hayo yamewasilishwa Hazina kwa ajili ya uhakiki ili walimu hao wapewe madai yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, maswali ya nyongeza kama yapo.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini napenda tu kujua, maana sasa wamesimamia kwa muda mrefu tangu mwaka 2015/2016 ni muda mrefu sasa.

Je, ni lini sasa uhakiki huu utaweza kukamilika ili walimu waweze kulipwa madai yao? (*Makofi*)

Swali la pili, katika madai hayo, walimu tu Wilaya yetu ya Geita wanadai zaidi ya shilingi milioni 120, napenda pia kujua ni lini walimu hawa wanaotoka Wilaya yangu ya Geita wataweza kulipwa madai yao? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika *leve*/mbalimbali, mchakato huu wa uhakiki wa deni umeshakamilika. Kwa hiyo, nadhani Hazina sasa hivi wanajipanga, wakati wowote deni hili litaweza kulipwa ili mradi kila mtu haki iweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo najua Mheshimiwa Bukwimba ni mpiganaji mkubwa sana wa watumishi wake katika jimbo lake, lakini siyo jimbo lake peke yake isipokuwa

katika maeneo mbalimbali. Katika eneo la Jimbo lako kwamba lini watalipwa mgao huu wa deni hili ambalo Hazina wanalishughulikia, likilipwa lote litalipwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tuvute subira kwa sababu Hazina ndiyo walikuwa wanafanya uhakiki wa madeni mbalimbali siyo wa walimu ni mchakato wa kulipa madeni mbalimbali. Jambo hili litakamilika na wananchi wa Busanda kule katika jimbo lako Geita wananchi wa eneo lile watapata hasa hasa watumishi wa Serikali ambao ni walimu watapata madai yao kama ilivyokusudiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, lakini kwa Waheshimiwa Wabunge wanya tunaowaapisha hawa, hii ndiyo namna ya kuuliza maswali. Ukitaka swali lako liwe zuri, anza na neno je, halafu endelea, kama alivyoanza Mheshimiwa moja kwa moja bila maneno ya kupamba pamba yale ambayo hayana sababu.

Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 69

### **Mgao Unaotokana na *Service Levy***

**MHE. ESTER A. MAHAWE** aliuliza:-

Fedha zinazokusanywa za asilimia 0.3 ya *service levy* zimeshindwa kusaidia Halmashauri nchini kwa uwiano unaolingana.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka fedha hizo kukusanywa na TAMISEMI ili kila Halmashauri iweze kupata mgao unaolingana?



**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *service levy* ni chanzo kinachokusanywa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 kifungu cha 6(1) na 7(1). Ushuru huo unatozwa kutoka kwa makampuni, matawi ya makampuni na mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ambaye anafanya shughuli zake katika Halmashauri husika. Hivyo, Halmashauri ndiyo yenye mamlaka ya kukusanya ushuru huo kwa mujibu wa sheria. Ofisi ya Rais, TAMISEMI kazi yake ni kuandaa sera, sheria, kanuni na miongozo na kusimamia utekelezaji wake kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuboresha utaratibu unaotumika kukusanya ushuru huo kwenye Halmashauri kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ili kuondoa utata uliokuwepo ambapo makampuni yalikuwa hayalipi ushuru huo kwa kuzingatia kuwa unalipwa Makao Makuu ya Kampuni.

Mheshimiwa Spika, Bunge litapata fursa ya kujadili marekebisho hayo ambayo yanakusudia kuziwezesha Halmashauri kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango cha kuridhisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mahawe, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa muda mrefu sasa Halmashauri nyingi nchini zimekuwa zikipoteza mapato ambayo yamepotea kupitia kampuni mbalimbali za simu kwa kutokulipa hizo *service levy* katika maeneo mengi nchini.

Je, ni lini sasa Serikali itazibana kampuni hizo ili ziweze kulipa hiyo *service levy*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutokana na Halmashauri nyingi nchini kuwa na vyanzo vichache vya mapato. Je, ni lini Serikali itaweza kufanya mpango wa kuziongezea *Capital Development Grants* Halmashauri hizo nchini? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MIKOA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Ester kwa sababu najua kwamba anaguswa na Halmashauri zake zote ambazo anazisimamia katika mkoa wake. Naomba niwahakikishie kwamba ndiyo maana tumeandaa sheria hii ya fedha, mabadiliko ya Sura Namba 290 kwa lengo la kufanya utaratibu mzuri wa kukusanya hizi kodi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ester amezungumzia suala zima la minara ambalo lilikuwa linaleta mkanganyiko mkubwa sana. Katika jambo ambalo litashughulikiwa kwa undani zaidi ni suala zima la ushuru wa minara ambalo tunaliwekea utaratibu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nina imani ikifika hapa Bungeni, tutajadili tuone ni utaratibu gani tutafanya. Ninaamini na sheria itakuja siyo muda mrefu, tutaweka utaratibu mzuri ili tuweze kuwabana vizuri hawa wenye makampuni mbalimbali hasa ya simu, waweze kulipa kodi vizuri. Lengo kubwa ni kuziwezesha Halmashauri zetu ziweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika mchakato huu wote wa sheria hizi, lengo kubwa la Serikali ni kuziongezea Halmashauri zetu uwezo wa kupata mapato ya kutosha kwa ajili ya kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika suala zima la kujiendesha, kuongeza ile *Capital Development Grand* ni jukumu la Serikali. Ndiyo maana hata ukiachia hilo, ukiangalia ile *Local Government Development Grants* hata mwaka huu tumeongeza zaidi ya shilingi bilioni 251 kwa lengo tu la ku-*facilitate* Halmashauri ziweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, eneo hilo tutaangalia nini tufanye Halmashauri zetu ziweze kufanya vizuri tukijua kwamba Halmashauri zikifanya vizuri ndiyo nchi itaenda vizuri katika suala zima la maendeleo.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, hakuna wa kumuulizia, CCM! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Paresso, nilikuona.

Na. 70

### **Kubadili Matumizi ya Shule ya Sekondari ya Wazazi Tarafa ya Kamsamba**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Katika Tarafa ya Kamsamba kuna Shule ya Sekondari ya Wazazi inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya CCM ni muda mrefu sasa shule hiyo haitumiki na haina mwanafunzi hata mmoja na hivyo kufanya majengo yake kuharibika.

Je, kwa nini Serikali ya Awamu ya Tano isirudishe shule hiyo kwa wananchi ili waweze kuitumikia au kubadili matumizi na kuwa Chuo cha Ufundi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest David Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Wazazi ya Kamsamba, iliyoko katika Tarafa ya Kamsamba, Wilaya ya Momba ambayo inamilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya CCM haitumiki na haina wanafunzi. Shule hii ni ya kutwa kwa wavulana na wasichana, kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne na ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 225 iwapo miundombinu yake yote itakamilika na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri itafanya mazungumzo na mmiliki wa shule ili kuona uwezekano wa kurejesha majengo hayo Serikalini ili shule ianze kupokea wanafunzi.

**SPIKA:** Hili swali la uchokozi hili. Mheshimiwa Paresso ndiyo uliuliza eeh? Si ndiyo utaratibu jamani! Haya mwenye swali amekuja. *(Kicheko)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kukubali kwamba watafanya mazungumzo na mmiliki ambaye ni Chama cha Mapinduzi, shule hii ni muda mrefu sana imefungwa, karibu miaka kumi hamna mwanafunzi anayesoma pale. Ni kwa nini msione sasa ni wakati muafaka wa kuirudisha kwa wananchi ili tuweze kuitumia?

Mheshimiwa Spika, ombi letu la pili, tunaomba shule hii tuitumie kwa ajili ya kidato cha tano kwa sababu Halmashauri ya Wilaya Momba haina shule ya kidato cha tano? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, nafikiria sioni swali. Maana unaposema warudishe, umeshasema mwenyewe kwamba inamilikiwa na CCM. Huyu bwana siyo mfanyakazi wa CCM wala nini. Kwa nini Mheshimiwa Silinde, wewe usiongee na CCM halafu mkaafikiana? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema shule hii inamilikiwa na Chama cha Mapinduzi kupitia Jumuiya yake ya Wazazi. Kwanza naishukuru Jumuiya ya Wazazi kwa sababu imefanya *intervention* kubwa kwa nchi hii kujenga shule mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba niweke katika kumbukumbu kwamba Jumuiya ya Wazazi kupitia Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, alitusaidia sana kupatikana kwa Shule ya Umumwani, ambayo Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo alikuja kutukabidhi pale na juzi nimeenda kule Kagera watoto wanasoma pale. Kwa hiyo, tunaishukuru sana jumuiya hiyo kwa kazi kubwa sana inayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Serikali, hatuwezi kuirudisha tu hivi hivi, isipokuwa kuna utaratibu wa *negotiation*, pale Jumuiya ya Wazazi itakapoona inafaa, kwa sababu jukumu lake kubwa ni kuwasomesha watoto wa Tanzania kwa mbinu muafaka, basi inawezekana tukaongea na Mwenyekiti pale ambaye nadhani ni Mjumbe wa Kamati Kuu, aangalie nini cha kufanya, aidha kuiboresha mwenyewe ili ichukue watoto ama kuangalia utaratibu kama alivyotusaidia kule Umumwani kwa lengo la kuwasaidia Watanzania. Hili siyo jambo baya sana.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kuifanya shule hii iwe ya Kidato cha Tano na cha Sita, nadhani hili ni wazo zuri na Jumuiya ya Wazazi pale watakapoona, aidha wenyewe kuifanya na kuiboresha miundombinu yake iwe ya kidato cha tano na cha sita kwa Tanzania, ama kuirudisha Serikalini. Mwenyekiti wa jumuiya hiyo yuko humu, atatuelekeza nini tufanye kwa muktadha wa kusaidia wanafunzi na watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekutaja sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM na upo Bungeni, swali la nyongeza, Mheshimiwa Bulembo, nimekuona. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLA M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijauliza swali, naomba unipe nafasi kidogo niseme maneno mawili kidogo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Silinde kama ameona mali za Chama cha Mapinduzi zinaweza kuja kuombwa Bungeni, nafikiri ni dalili nzuri kwamba naye anaelekea kuja CCM, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu linasema hivi, maombi haya yanayoletwa kwa ajili ya Shule ya Jumuiya ya Wazazi, Wizara naomba iniambie; je, kwa nini msishirikiane na Mbunge mkaimarisha shule nzuri ya Julius Nyerere ambayo inaonekana imeharibika, haifai, haina huduma nzuri, mpaka mwende kutafuta mali za CCM? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Alhaji Bulembo alikuwa anatoa ushauri na mimi napenda kumpongeza sana kwa juhudi kubwa anayofanya katika shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, nadhani ushauri huu kama Serikali tumeupokea, kwa sababu Mheshimiwa Alhaji Bulembo wewe ni mlezi wa watoto na ndiyo maana umeamua kujenga shule hizi na kuzisimamia. Kwa hiyo, tutakachokifanya ni kuboresha maeneo mbalimbali ili watoto wetu waweze kusoma kwa kadiri iwezekanavyo.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, nilikuwa najjuliza tu hapa, CCM angalau ina shule mpaka za sekondari. Sasa

hawa CHADEMA, CUF na wengine hivi wana shule hata ya chekechea hawa kweli? *(Kicheko)*

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Tulijenga wote wakati wa chama kimoja. Zilijengwa na wananchi wote enzi ya chama kimoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** CCM, CCM!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Hata zahanati hawana.

**SPIKA:** Swali la Mheshimiwa Silinde limeleta uchangamfu wa aina yake. Mheshimiwa Mattar.

Na. 71

### **Uhaba wa Nyumba kwa Wanajeshi – Zanzibar**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Tatizo la makazi kwa wanajeshi wetu ni kubwa kiasi kwamba maaskari wetu kupata usumbufu na kuathiri utendaji kazi wao.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za makazi kwa wanajeshi wa upande wa Unguja?

(b) Je, ni nyumba ngapi Serikali imepanga kujenga Zanzibar?

(c) Je, ni lini ujenzi wa nyumba kwa upande wa Zanzibar utaanza?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kuboresha makazi ya wanajeshi kwa kujenga nyumba za familia idadi ya 10,000. Kwa awamu ya kwanza ujenzi wa nyumba za familia za askari idadi 6,064 umefikia hatua ya mwisho kukamilika. Aidha, katika awamu hii hakuna ujenzi unaofanyika Unguja.

(b) Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza kwa upande wa Zanzibar, nyumba zimejengwa katika Kisiwa cha Pemba. Nyumba zilizojengwa ni ghorofa 40 zenye uwezo wa kuchukua familia idadi 320. Hatua inayofuata ni kukamilisha miundombinu ya umeme na maji ili nyumba hizo zianze kutumika.

(c) Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanza ujenzi wa nyumba za askari awamu ya pili unaotarajiwa kukamilisha ujenzi wa nyumba 10,000 unaendelea. Mgawanyo wa nyumba hizo utazingatia hitajio katika Kambi za Jeshi kwa ujumla ikihusisha Kambi za Unguja. Ujenzi huu utaanza mara mchakato utakapokamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mattar, swali la nyongeza.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa. Nina maswali mawili madogo ya kuuliza.

Mheshimiwa Spika, zipo nyumba za zamani kabisa ambazo wanajeshi wetu wanazitumia hadi sasa na hali yake siyo nzuri kabisa.

Je, Wizara ina mikakati gani ya kuzifanyia marekebisho angalau zikaendana na hali ya sasa?



Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri, amesema hana uhakika kama atajenga nyumba Unguja kwa awamu hii.

Je, ni lini anaweza kutueleza anaweza akatuanzia nyumba za Unguja wakati Unguja bado pana matatizo makubwa ya nyumba za kijeshi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za zamani kufanyiwa ukarabati, hilo liko katika bajeti zetu. Nataka niwaeleze tu kwamba kwa kawaida bajeti inakuwa na miradi mipya na fedha za ukarabati.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mwaka huu wa fedha tuliweka fedha za ukarabati katika Bajeti ya Ngome na ni mategemeo yetu kwamba fedha zikipatikana tutakuwa tukirekebisha nyumba hizo awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni lini za Unguja zitajengwa? Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba mchakato wa mazungumzo ya kupata fedha ajili ya kumaliza awamu ya pili unaendelea na utakapokamilika tu, basi bila shaka tutaanza awamu hiyo. Nataka nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba awamu hiyo itahusiaha kambi zilizokuwepo upande wa Unguja.

**SPIKA:** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Na mimi nitoe pole kwanza kwa Mheshimiwa Waziri kwa Naibu Waziri wake kujiuzulu na yuko peke yake na kazi nzito alizokuwanazo kwa muda huu, lakini huu ni umakini wake na aendelee kupiga kazi kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Serikali ijibu Swali langu Namba 72, lakini kabla ya kusahau niombe ku-*declare interest*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku, *interest* gani unayo-*declare*?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mfanyabishara. Huwezi kudharau dafu kwa embe ya msimu. Nikitoka hapa nitarudi tena kufanya biashara.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Ni msemo huo!

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa Jaku mnajua tena.

Na. 72

### **Eneo la Gati la *Malindi Wharf* – Dar es Salaam**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa meli za mizigo za Zanzibar zimetengewa eneo maalum la kufunga gati linaloitwa *Malindi Wharf (lighter key)* kwenye bandari ya mizigo ya Dar es Salaam na kuna taarifa kuwa sehemu hiyo sasa inatarajia kujengwa katika upanuzi wa bandari, jambo ambalo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, ingawa sehemu hiyo ni muhimu sana katika kutoa huduma ya meli za upande wa pili wa Muungano (Zanzibar).

(a) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kutengwa eneo lingine maalum kwa ajili ya kufunga gati meli za mizigo za Zanzibar ili Wazanzibar waendeleo kupata huduma kwenye bandari ya nchi yao?

(b) Endapo itaonekana ipo haja hiyo, je, ni sehemu gani kwenye bandari iliyopangwa kwa ajili ya meli za mizigo za Zanzibar endapo sehemu ya sasa itajengwa?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, lenye Sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Bandari ya Dar es Salaam inafanyiwa marekebisho makubwa ikiwa ni pamoja na kujenga gati jipya katika eneo la *Gerezani Creek*, kupanua na kuongeza kina cha lango la meli, kupanua na kuongeza kina cha eneo la kugeuzia meli, kuimarisha na kuongeza kina cha gati kutoka Namba 1 mpaka Namba 7 na kuongeza eneo la kuhudumia shehena kwa kutumia vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kazi hizi zinafanywa katika sehemu ya awamu ya kwanza ya mpango wa kuboresha bandari yote ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub kwamba katika awamu hii ya kwanza maboresho yanayoendelea hayatahusisha miundombinu ya eneo la *Kighter Quay*, hivyo huduma zinazotolewa katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na zile za meli za mizigo za Zanzibar, zitaendelea kutolewa kama kawaida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hashim Jaku, swali la nyongeza kama lipo.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, hayakosekani.

Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na muafaka. Nawaomba tu Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, wanapojibu maswali kwanza wafanye utafiti kabla ya kuja kujibu humu ndani. Tumekuwa na masikitiko sana *back bencher* huku na...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku nimekuvumilia sana. Una maneno mengi ambayo hayana sababu. Wewe uliza swali tu.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, hewala!

**SPIKA:** Yaani unamwambia Profesa hajafanya utafiti kweli! Haya endelea kuuliza swali.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, swali langu la msingi ni kuhusu meli za Zanzibar na meli hizi ni za *local* na zimekuwa zikiwa-*charged* kwa dola na *rate* ya dola huwa inapanda siku zote.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni sababu sasa hivi *tariffs* zile za muda mrefu na hivi sasa kuchajiwa kwa shilingi ukizingatia zile meli ni za Tanzania na ziko katika sehemu ya *local*?

Mheshimiwa Spika, la pili, kumekuwa na kilio kirefu sasa bandarini, hata leo hii pana *crane* pale imekuwa ikisumbua watu, baada ya miezi mitatu leo ndiyo imeondolewa, ni jambo la kupongeza kwa kuwa nauliza swali humu ndani. Lini Mheshimiwa Waziri atafanya ziara pale kuona hali ilivyo? Kuna usumbufu wa malipo; inachukua masaa matatu au mawili kulipa shilingi 10,000? Ni lini Mheshimiwa Waziri atafanya ziara hiyo kwenda kuona hali halisi ilivyo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri, Profesa Makame Mbarawa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa nini tuna-*charge* kwa dola? Bandarini pale sisi tunafanya biashara na watu wa kutoka nchi mbalimbali kama vile kutoka Tanzania, Rwanda, Burundi na pia Comoro. Lile eneo ambalo wanatumia wananchi hasa kutoka Zanzibar tunafanya biashara na watu wa Comoro ambao wote tunawa-*charge* kwa dola, lakini inategemea na *exchange rate*.

Mheshimiwa Spika, sasa kama mtu anataka kulipa dola anaweza kulipa kwa dola, kama anataka kulipa kwa

shilingi anaweza kulipa kwa shilingi. Leo tunaona tu kwa sababu dola kila siku inapanda, lakini naamini uchumi wetu utakapokua iko siku *currency* yetu itakuwa iko nzuri na tutaweza tutamani tulipe kwa dola kwa sababu itakuwa ni *cheaper* zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu kufanya ziara, ni mara nyingi nafanya ziara kwenye Bandari ya Dar es Salaam na ninategemea hata wiki inayokuja Mungu akipenda, nitafanya hivyo. Naomba tu nimwalike Mheshimiwa Jaku tuwe pamoja katika ziara yangu ili tuweze kuzungumza na wadau wengine jinsi gani tunavyoweza kutatua matatizo ya Bandari yetu ya Dar es Salaam kwa maslahi ya uchumi wan chi yetu.

**SPIKA:** Wizara ya Nishati na Madini, swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Ukonga.

Na. 73

### Umeme wa *REA* – Ukonga

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Jimbo la Ukonga lina shida kubwa ya umeme katika Kata zifuatazo; Kata ya Chanika (Ngwale, Nguvu Mpya, Virobo, Kidugalo, Yongwe, Lukooni, Vikongoro na Tungini); Kata ya Zingiziwa (Zogoali, Zingiziwa, Ngasa, Ngobedi, Somelo na Gogo, Lubakaya na Kimwani); Kata ya Majohe (Kivule na Viwege); Kata ya Buyuni (Zavala, Buyuni, Mgeule Juu, Nyeburu, Mgeule Chini, Kigezi, Kigezi Chini na Taliani); Kata ya *Pugu Station* (Bangulo, *Pugu Station* na Kichangani); Msongola (Yangeyange, Mbondole, Kidle, Mkera, Sangara, Kiboga, Uwanja wa Nyani, Kitonga, Mvuleni na Mvuti) na Kata ya Kivule (Bombambili). Maeneo hayo yote yanahudumiwa na Wilaya ya Kisarawe kama maeneo ya vijijini.

Je, ni lini maeneo hayo yatapata umeme wa *REA*?

**SPIKA:** Siku nyingine Mheshimiwa Mwita, haya maneno mengi haya unamwandikia tu Waziri huko, unatunga swali la Kibunge. Mheshimiwa Naibu Waziri, Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swai la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kidole, Bangulo, Kitonga, Mvuti na baadhi ya maeneo mengine pamoja na Msongole yalipatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Pili uliokamilika mwezi Disemba, 2016. Kazi ya kupeleka umeme katika maeneo hayo ilijumuisha pia vijiji vilivyokuwa vinatoka katika Wilaya ya Kisarawe ambapo pamoja na mambo mengine vimefungiwa transfoma 55 za kVA 50, kVA 100 na kVA 200; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 pia umejengwa kwa urefu wa kilometa 187.22 lakini njia ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 239.7 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja 1,083. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 5.3.

Mheshimiwa Spika, mitaa mingine iliyobaki ya Kata za Chanika, Zingiziwa, Majohe, Buyuni, *Pugu Station* pamoja na Msongola, zitapatiwa umeme kupitia Mradi wa *Urban Electrification* chini ya ufadhili wa Maendeleo wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, kazi hizi zinajumuisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 66.3, msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 336.7 pamoja na ufungaji wa transfoma 73 za kVA 200 na kVA 100. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 10.73 na utaunganishia wateja 7,083.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, tafadhali, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza naomba niseme tu kwamba nashukuru kwa ushirikiano ambao naupata kutoka pale *TANESCO*, Gongolamboto, Kisarawe na Mheshimiwa Naibu Waziri nikimpigia simu anapokea, siyo kama wengine walivyosema hapa.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Jimbo la Ukonga lina shida kubwa ya umeme, lakini pia kuna shida nyingine zimeongezeka, Ukonga kuna wajasiriamali wadogo wenye viwanda vidogo vya kusaga unga wa sembe na dona, lakini pia na chakula cha kuku; umeme unakatika sana katika eneo hilo. Kwa hiyo, naomba kama kuna utaratibu wa dharura, ufanyike ili kuzuia hiyo kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, eneo la Kitonga Sekondari, Mvuti Sekondari, Mbondole Sekondari, Bombambili Shule ya Msingi na Shule ya Msingi Nzasa II kuna visima vya maji havifanyi kazi kwa sababu kuna shida kubwa ya umeme katika eneo hilo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akawa na mkakati mahususi wa kuondoa kero katika maeneo haya ambayo ni maeneo muhimu kwa walimu, wanafunzi na jamii inayozunguka eneo hili? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemuni.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na mimi namshukuru Mheshimiwa Mbunge anavyofuatilia masuala ya wananchi wake wa Ukonga. Niseme tu, katika swali la kwanza kuhusu kukatika kwa umeme; katika maeneo ya Kisarawe hivi sasa tulikuwa tunajenga miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Gongolamboto na Kipawa ili wananchi wengi wafikiwe na umeme unaojitosheleza. Ujenzi wa utaratibu huo unaendelea na unakamilika mwezi wa Oktoba tarehe 22.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waitara kwamba mara baada ya kukamilika, tatizo la kukatika kwa umeme kwa maeneo ya Kisarawe, Gongolamboto, Mvuti pamoja na Chanika yatakwisha mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Ukonga yapo maeneo ambayo yanapata umeme kutoka eneo la Kisarawe na kwa maana hiyo yanahesabika kama yapo vijijini. Maeneo hayo ni pamoja na kama ambayo ametaja Mheshimiwa Waitara, ni Kitonga lakini yapo maeneo ya Namanga, Bombambili pamoja na Uwanja wa Nyani, yote hayo yanapata umeme kutoka Kisarawe. Kwa maana hiyo, visima vilivyopo katika maeneo hayo, yataunganishwa sasa na umeme wa Mradi wa *REA* ambao unakuja sasa ili wananchi waweze kupata maji kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa niaba ya wananchi wote kwamba Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu, pamoja na kupeleka umeme kwenye vitongoji na vijiji, utaunganisha pia miundombinu ya maji kote nchini.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waitara maeneo ya Kitonga, Uwanja wa Nyani, Msongole, Mvuti na Vijiji vingine ambavyo vina visima vitaunganishwa na mradi huu wa *REA*.

**SPIKA:** Waheshimiwa najua kabisa mambo ya umeme vijiji yaani kila mtu akisimama hapa, wapo watakaoorodhesha vijiji vingi kuliko hata Mheshimiwa Waitara hapa. Kwa hiyo, tuendelee na swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 74

### **Gharama ya Ujenzi wa Bomba la Gesi**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, gharama ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ni shilingi ngapi?



**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Kibunge, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara na Songo Songo Mkoani Lindi hadi Dar es Salaam ulianza kutekelezwa mwezi Juni, 2013 na kukamilika mwezi Oktoba, 2015. Ujenzi wa mradi huu ulihusisha ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi asilia yaani Madimba (Mtwara) pamoja na Songo Songo (Lindi) kwa gharama ya dola za Marekani milioni 349.51 na pia ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara na Songo Songo – Lindi hadi Dar es Salaam kwa gharama ya dola za Marekani milioni 875.72.

Mheshimiwa Spika, jumla ya gharama zote za mradi huu hadi kukamilika ni dola za Marekani milioni 1,225.23.

Mheshimiwa Spika, bomba lina uwezo wa kusafirisha gesi asilia futi za ujazo milioni 784 kwa siku na linaweza kufikia futi za ujazo milioni 1,002 kwa siku. Kwa sasa gesi inayosafirishwa ni futi za ujazo milioni 68.5 kwa siku.

**SPIKA:** Sasa kama ninavyowasisitiza Waheshimiwa Wabunge kuuliza maswali ya Kibunge, nanyi Mawaziri vilevile, maana swali la Mheshimiwa Tunza kauliza kifupi sana. Bomba la gesi Mtwara – Dar es Salaam, shilingi ngapi? Kwa hiyo, ilitakiwa jibu ni shilingi kadhaa, basi. Mmeanza kumpa *story*, mkaogelea na nini. Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kutokana na ripoti ya CAG mpaka sasa hivi inaonekana ni 6% tu ya gesi inatumika, inayosafirishwa na hilo bomba na uwekezaji huu ni wa pesa

nyingi. Nataka kujua Serikali imejipanga vipi kuhakikisha uwekezaji huu unaleta tija kwa Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa kuna utata mkubwa katika uwekezaji huu kujua gharama halisi: Je, Serikali ipo tayari kumtaka CAG afanye *special audit* katika uwekezaji huu? Nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza wewe hili swali, yaani ndiyo la leo hili, limechukua siku. Hata ambao walikuwa hawakufahamu wamejua yupo Mheshimiwa Tunza hapa Bungeni. (*Kicheko*)

Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa umakini mkubwa. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza bomba la kusafirisha mafuta au gesi kwa sasa kutoka Madimba (Mtwara) hadi Dar es Salaam ndiyo bomba kubwa tulilionalo kwa upande wa gesi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa sasa hivi gesi inayosafirishwa ni kati ya 6% hadi 10% ya uwezo wake na uwezo nimetaja ni milioni *cubic feet* 744. Sasa ni kwa nini? Bomba hilo lina upana wa inchi 36, ni kubwa; na mahitaji ya sasa ni megawati 668 tulizonazo kwa upande wa gesi, lakini miundombinu inayojengwa ndiyo mikakati sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunajenga miradi miwili ya kusafirisha gesi Kinyerezi I na Kinyerezi II. Kinyerezi I tunafanya *extension* ya kuongeza megawati 185 ili katika Kinyerezi I pekee zifikie 335.

Mheshimiwa Spika, kadhalika tunajenga mradi mwingine katika Kinyerezi II ambao utaweza kutoa megawati 240. Sasa miradi hii miwili ikikamilika, mahitaji makubwa ya gesi yataongezeka. Kwa hiyo, itazidi 6% hadi 10% na tuna matarajio inaweza kufikia asilimia 20 hadi 30.

Mheshimiwa Spika, miundombinu inayojengwa kuhitaji gesi, bado ni mingi; tunahitaji umeme wa kutosha. Kwa sasa hivi umeme hautoshi. Ni matarajio yetu kwamba mara baada ya miradi mingine, tutakwenda Kinyerezi III utakaoanza mwaka 2018 utakaohitaji megawati 600. Kwa hiyo, mahitaji ya gesi bado yatakuwa ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, lingine niseme mkakati mwingine, unapokuwa na gesi ya kutosha inakuruhusu kujenga miundombinu mingine kwa sababu una *stock*. Kwa hiyo, siyo hasara kuwa na gesi nyingi lakini kadhalika mikakati ya Serikali ni kuhakikisha kwamba hii gesi tunasafirisha kadri iwezekanavyo ili ichangie sana katika upatikanaji wa umeme. Mkakati wa Serikali ni kutumia gesi zaidi ili kuachana na mafuta ili kuwapunguzia mzigo wananchi, hilo ni katika ufafanuzi wa swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukaguzi, mahesabu ya Serikali hukaguliwa mara kwa mara, ni utaratibu wa kawaida. Kama ambavyo kila mwaka CAG hukagua, hata miradi hii ataendelea kuikagua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu, suala la ukaguzi wa miradi ni endelevu, CAG ataendelea kukagua ili hali halisi iendelee kufahamika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil, swali la nyongeza. Nimekuona.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kuna suala moja hajatoa ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji analalamika kwamba 6% za uzalishaji na gesi inayochukuliwa haitamfanya aweze kurejesha gharama za uwekezaji kwa kipindi cha miaka 25 kadri walivyokubaliana na Serikali; na Mheshimiwa hapa anasema kwamba kadri siku zinavyokwenda basi gesi nyingine itahitajika.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu, ni lini Serikali itamhakikishia mwekezaji kwamba bomba hili litatumika kwa asilimia 100 ili aweze kurejesha gharama zake ndani ya miaka 25, ikizingatiwa kwamba sasa hivi yupo kwenye mwaka wa 11? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali, una maslahi yoyote na huyo mwekezaji, maana umekaa kwa mwekezaji, huongelei Taifa wala nini? Kuna cha ku-*declare* au umeuliza tu kama Mbunge?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni kwa ajili ya Watanzania na wakazi wa Mtwara. *(Makofi)*

**SPIKA:** Aaah, huyo mwekezaji ni mkazi wa Mtwara eeh? Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme mradi ule ni wa Serikali kwa asilimia 100, hilo ni la kwanza kabisa. Kwa hiyo, unamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Hata hivyo, kama nilivyosema, mwaka gani tutaweza kupata gesi asilimia 100 inayozalishwa pale? Ni mradi ambao ni endelevu. Iko miradi mingine inajengwa Mtwara ambayo inaanza mwezi Machi mwakani ambayo tutaanza kuzalisha megawati 500 kwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba bado kuna muda wa kutosha, ifikapo mwaka 2020/2022 tuna matarajio kwamba gesi inayozalishwa katika Madimba tutaweza kuitumia kwenye miradi yetu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu miradi ni mingi, ifikapo mwaka 2022 matarajio kati ya asilimia 80 hadi 100 tutaanza kutumia gesi yote asilia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Swali la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Wawi.

Na. 75

### **Sera ya Diplomasia ya Uchumi**

**MHE. AHMED JUMA NGWALI** aliuliza:-

Tanzania ilibadilisha Sera yake ya Kibalozi ili kuendana na mazingira ya sasa ya kiuchumi duniani kwa maana ya kujiwekeza katika Diplomasia ya Uchumi (*Economic Diplomacy*).

(a) Je, ni lini Tanzania ilibadili Sera yake ya Mambo ya Nje ya awali na kujielekeza katika Sera ya Diplomasia ya Uchumi?

(b) Je, mwenendo ukoje kati ya sera hii na ile iliyokuwepo awali?

(c) Je, ni vigezo au vipimo gani vinavyotumika kupima Balozi zetu katika utekelezaji wa sera hii ya Diplomasia ya Uchumi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Wawi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mara baada ya Tanzania kupata uhuru mwaka 1961 na hata baada ya Muungano mwaka 1964, Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania iliweka msisitizo zaidi kwenye masuala ya kisiasa hususan kupigania uhuru wa nchi za Afrika zilizokuwa zinatawaliwa na wakoloni, kupunga ubaguzi wa rangi na ukoloni mamboleo.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Tanzania kwenye masuala ya uhusiano wa Kimataifa kabla ya mwaka 2001

uliongozwa na matamko mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa nchi na nyaraka kama vile Waraka wa Rais Namba 2 wa mwaka 1964. Tanzania ilifanikisha jukumu hilo kwa ufanisi mkubwa na kujijengea heshima mbele ya jamii ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha jukumu la kuzikomboa nchi za Afrika kutoka katika makucha ya ukoloni na vilevile kutokana na mabadiliko yaliyotokea duniani katika medani za kisiasa na uchumi ikiwemo kwisha kwa vita baridi, kuibuka kwa utandawazi, dhana ya demokrasia na uchumi wa soko, Tanzania ililazimika kubadili mwelekeo wa sera yake ya mambo ya nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, mwaka 2001 Serikali ilitunga sera mpya ya mambo ya nje ambayo imeweka msisitizo kwenye diplomasia ya uchumi. Sera hiyo ndiyo inayoendelea kutekelezwa hadi hivi sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza katika jibu langu kwenye kipengele (a), sera ya awali ya mambo ya nje ilijikita zaidi katika masuala ya kisiasa ambapo Tanzania ilishiriki kikamilifu kutafuta ukombozi wa nchi nyingi za Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sera ya Mwaka 2001 ya Mambo ya Nje ambayo utekelezaji wake umelenga zaidi kupata manufaa ya kiuchumi kutokana na mahusiano yake na nchi nyingine duniani, Tanzania imeshuhudia ongezeko kubwa la watalii waliotembelea nchi yetu; ongezeko kwenye biashara ya nje na uwekezaji, pamoja na kupatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu na misaada ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa sera ya sasa imejikita katika masuala ya kiuchumi, bado Tanzania inashirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika kulinda amani na usalama katika nchi mbalimbali duniani.

(c) Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kupima utendaji wa Balozi zetu ni pamoja na namna Balozi

anavyotimiza majukumu yake kama yanavyoainishwa katika *OPRAS* na Mpango Kazi wake wa mwaka pamoja na kutekeleza kwa weledi majukumu yake kama kuvutia wawekezaji kutoka nje, kutafuta masoko ya bidhaa zetu, kuvutia watalii, kutafuta teknolojia sahihi na rahisi, kutafuta misaada ya maendeleo na mikopo ya masharti nafuu na kuendelea kujenga sifa nzuri ya nchi yetu na mambo hayo yamewekwa katika kitabu chao cha *Ambassador's Handbook*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngwali, swali la nyongeza.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumetoka katika siasa ya uchumi na tumeingia katika sera mpya ya demokrasia ya uchumi, naomba niuize kwamba Serikali imejipanga vipi katika kuandaa wataalam katika kuhakikisha hiyo dhana halisi ya kufikia hiyo demokrasia ya uchumi inafikiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nauliza kutokana na hali mbaya za Balozi zetu ambazo kila mmoja anaelewa nadhani kwamba Balozi zetu hazipo katika hali nzuri, Serikali imejipanga vipi kupeleka bajeti na kuhakikisha kwamba bajeti hiyo inatosha kwa ajili kuhudumia Balozi ili waweze hasa hiyo mikakati kwa ajili ya kutekeleza hiyo diplomasia ya uchumi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Susan Kolimba.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusu Wizara imejipangaje katika kuandaa wataalam ambao wataweza kutekeleza diplomasia ya uchumi; kama tulivyokuwa tumeleza katika hotuba yetu ya bajeti, katika mpango wetu wa bajeti, katika kila Kitengo cha Wizara

tumeweka sehemu ambayo inaangalia mafunzo ya watumishi wetu na katika kila kitengo inaangalia kwamba ina idadi ya watumishi wangapi na wangapi watatakiwa kwenda kwenye *training* na *training* hizo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yanafanywa nje na ndani ya nchi. Kuna semina mbalimbali, wanahusishwa katika ushiriki wa Mikutano yetu ya Kimataifa, lakini vilevile wanapelekwa katika *training* ni za muda mrefu na zile za muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema katika utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi, haihusishi tu Wizara ya Mambo ya Nje, hili ni suala mtambuka, linagusa Wizara nyingine za kisekta na hata tunapojadili miradi ambayo imetafutwa kwa fursa kwa kupitia Wizara yetu, tunahusisha pia Wizara za kisekta na katika Wizara za kisekta tunatumia pia wataalam katika Wizara husika pamoja na Wizara yetu. Kwa hiyo, tumejipanga vizuri kama Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika suala la pili ambalo linahusu mkakati wa kusimamia na kuhakikisha kwamba bajeti iliyopangwa inakwenda; sisi kama Wizara tunajua kwamba tunawajibika, tunajua kuna watu ambao wanafanya kazi kwa ajili ya Serikali hii na kazi yetu kubwa kama Wizara ni kuhakikisha kwamba bajeti ambayo tumeiomba na imepitishwa katika Bunge hili inakwenda kwa wakati na tutakuwa tunaendelea kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, pia katika siku zijazo tutaendelea pia kuliomba Bunge hili kuhakikisha kwamba wanapitisha bajeti ambayo tunaiomba ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza hii diplomasia ya uchumi kwa ukamilifu zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh, swali la nyongeza kwenye eneo hilo.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, anaweza kutueleza hapa kwamba kuna chuo chochote kile ambacho



kinaendesha kozi ya ubobezi ya diplomasia ya kiuchumi hivi sasa? Kama hakipo, je, Serikali ipo tayari kutumia nafasi yake kushawishi *specifically* kuendesha kozi hizo bobeki katika kiwango cha *Masters* na *Ph.D* ili tupate hao watalaam wanaotakiwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Susan Kolimba.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, vyo vya ubobezi wa diplomasia viko vingi, lakini kama nilivyosema kwenye majibu ambayo niliongezea katika maswali ambayo ameliza Mheshimiwa Ngwali, nimesema kwamba katika bajeti ya Wizara, katika vitengo vyetu tumepanga bajeti ya kuhakikisha kwamba hao watumishi wanapata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu na mafunzo haya wanayapata kutoka kwenye Chuo cha Diplomasia, vilevile wanapata nje ya nchi ambako kuna mafunzo ambayo ni ya ubobezi pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Ally Saleh kwamba jambo hili Wizara inalitambua.

**SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu, leo hayupo kwenye kiti chake. Aah, leo amepanda daraja. Mwalimu endelea na swali.

Na. 76

### **Kufungua Ofisi ya Uhamiaji - Muhange**

**MHE. KASUKU S. BILAGO** aliuliza:-

Jimbo la Buyungu Wilayani Kakonko linapakana na nchi ya Burundi, hivyo raia wa nchi hizi mbili wanafanya baadhi ya shughuli za kibiashara na kijamii kwa kushirikiana kwa muda mrefu hata kabla ya Burundi kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(a) Je, ni lini Serikali itafungua Ofisi ya Uhamiaji katika kijiji cha Muhange iliyofungwa bila sababu za msingi?

(b) Je, kwa nini Warundi wakija kufanya biashara kwenye masoko ya ujirani mwema au kulima mashamba hukamatwa na kufungwa jela?

(c) Je, kwa nini Warundi 254 waliofungwa kwa makosa kama hayo wasirudishwe kwao ili kupunguza msongamano magerezani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Uhamiaji katika Kijiji cha Muhange ilifungwa kutokana na sababu za kiusalama baada ya nchi jirani ya Burundi kuingia katika machafuko miaka ya 1990. Hata hivyo Serikali itaangalia endapo mazingira ya sasa yanaruhusu kujenga Ofisi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazoruhusu wageni kuingia nchini, kuishi na kufanya kazi. Hivyo, wageni wote waingiapo nchini wakiwemo raia wa Burundi wanapaswa kuafuata sheria na taratibu zilizopo.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna msongamano wa wafungwa katika Magereza yetu nchini kutokana na sababu mbalimbali ambapo kwa sasa kuna jumla ya wafungwa 725, raia wa Burundi katika Mkoa wa Kigoma ambao wamefungwa kwa makosa mbalimbali.

Hata hivyo, ipo sheria inayoruhusu kumrudisha mfungwa kwao kwa yule ambaye sio Mtanzania. Sheria hiyo inaitwa *The Transfer of Prisoners Act (No. 10) of 2004* na Kanuni zake (*The Transfer of Prisoners Regulations of 2004*).

Mheshimiwa Spika, sheria hii inatumika pale tu mfungwa wa nchi nyingine anapoomba kumalizia sehemu kifungo chake kwenye nchi yake ya asili.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu alilotoa Waziri kuhusu usalama uliosababisha kufungwa kwa Ofisi ya Uhamiaji Muhange miaka ya 1990 si la kweli. Miaka zaidi ya 20 Muhange ni salama na hakuna ofisi pale, wananchi wako pale, ofisi nyingine zote za Serikali zipo, inakuwaje Ofisi ya Uhamiaji ndiyo ishindikane kuwepo Muhange kwa sababu za kiusalama?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Burundi ni miongoni mwa Nchi za Afrika Mashariki kama zilivyo Kenya, Rwanda na kadhalika. Mipaka inayopakana na nchi hizi wananchi wake wananufaika kwa kubadilishana biashara kama mipaka ya Tunduma, Sirari, Namanga na kadhalika, pale kwetu, Jimbo la Buyungu wapo Warundi wanaokuja asubuhi kulima mashamba na kurudi nyumbani au sokoni na kurudi jioni, lakini Warundi hao wamekuwa wakikamatwa, mbona wale wa Sirari, Namanga na kadhalika hawakamatwi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer* Masauni tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, nilipojibu swali langu la msingi nilieleza sababu zilizosababisha kituo kile kufungwa ni hali ya usalama Burundi, sio Tanzania. Kwa hiyo, hoja yake kwamba Muhange ni salama sio hoja ambayo nimejibu katika swali la msingi, ni kwa sababu ya hali ya machafuko Burundi ilivyoanza, ndiyo sababu ambayo nilijibu katika swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, ni kweli wananchi waliopo mipakani katika nchi yetu na nchi jirani, zikiwemo Burundi, Uganda, Rwanda na kadhalika, tumekuwa na mahusiano ya muda mrefu na ndiyo maana kuna utaratibu ambao upo kwa mujibu wa sheria zetu. Kuna utaratibu ambao upo kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji wa jinsi gani raia wa kigeni wanapaswa kuingia nchini na nini wafanye na ni aina gani ya viza wawe nayo. Na tunaendelea kusisitiza kwamba sheria hizi ambazo zimetungwa kwa maslahi ya Taifa letu wananchi wa nchi jirani waendeleo kuzitii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kumekuwa kuna utaratibu wa utoaji wa vibali maalum kwa wananchi ambao wanaishi mipakani kwa masafa yasioyozidi kilometa kumi ambavyo vinaitwa vibali vya ujirani mwema. Vibali hivi vinatolewa bila ya malipo ili kuweza kuhamasisha na kusaidia wananchi ambao wamekuwa wakiishi mipakani kuendelea kutekeleza shughuli zao wanapokuwa wanavuka mipaka kwa shughuli za kawaida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, kumekuwepo na ongezeko kubwa la jamii ya Warundi katika Kambi ya Ulyankulu kule Tabora, hali ambayo inatishia usalama wa raia na mali zao, lakini zaidi wazawa maeneo ya Ulyankulu. Je, unafahamu ongezeko hili na una mikakati gani ya ziada kuweza kukabiliana na tatizo hili ili ongezeko hili lisiendeleo tena?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na jitihada mbalimbali ambazo zinafanyika kuweza kuhakikisha kwamba

tunapunguza idadi ya wakimbizi katika makambi yetu, na ni shahidi hivi karibuni mmeona kuna zoezi la kurudisha wakimbizi ambao wanarudi Burundi kwa hiari yao ambalo linaendelea. Hii yote ni kwa sababu ya kazi kubwa ambayo Serikali yetu pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki imefanya katika kuhakikisha kwamba amani inarudi Burundi na wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao za kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, kitu ambacho nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kambi zetu zote za wakimbizi hivi tunavyozungumza, kuna pungufu la wakimbizi ambao wanaingia, lakini pia harakati za kurudisha wakimbizi Burundi zinaendelea kwa kasi kubwa sana. Niendeleo kumtoa wasiwasi, lakini vilevile niendeleo kuwaomba kuwa nasihi wananchi ambao wanaishi mipakani kuendelea kutoa ushirikiano wao kwa baadhi ya wale wakimbizi ambao bado wanahisi kwamba sio wakati muafaka wa kurejea Burundi kwa sasa hivi, kuendelea kuwa-*host* kama ambavyo tumekuwa tukifanya miaka yote mpaka pale ambapo wataamua kuondoka wote kwa pamoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Tunaaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Ussi Pondeza, Mbunge wa Chumbuni. Mheshimiwa Ussi.

Na. 77

### **Kuchelewa kwa Matokeo ya Uchunguzi wa Vinasaba**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJAD** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya matokeo ya uchunguzi yanayofanywa kwa kutumia mashine ya kutambua vinasaba (*DNA*) kutoka Zanzibar kutopatikana kwa wakati na kusababisha kesi mbalimbali kushindwa kusikilizwa kwa wakati muafaka zikiwemo za jinai kama ubakaji.

(a) Je, kwa nini matokeo ya uchunguzi yamekuwa yakichukua muda mrefu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wakati uchunguzi huo una umuhimu mkubwa katika kupambana na vitendo vya uhalifu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mashine za kutosha ili uchunguzi ufanyike kwa wakati kutokana na vitendo vya udhalilishaji wanawake na watoto kuendelea kuongezeka baina ya pande mbili za Muungano?

(c) Je, ni lini Hospitali ya Taifa Muhimbili itaweka utaratibu wa kuchunguza sampuli za Zanzibar kwa wakati kwa kutumia mashine ya kuchunguza vinasaba (DNA)?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Jimbo la Chumbuni, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sampuli za uhalali wa watoto kwa wazazi (*paternity case samples*) zinafanyika kwa wepesi zaidi kuliko sampuli za makosa ya jinai (*criminal case samples*) kwa sababu sampuli za *paternity* zinachukuliwa moja kwa moja toka kwa wahusika (*direct samples*) na hivyo kurahisisha uchunguzi wake endapo wahusika wa uchukuaji watachukua kwa umahiri na uhifadhi utafanyika kwa namna stahili. Aidha, sampuli za uchunguzi wa makosa ya jinai (*criminal case files*) zinachukuliwa toka maeneo ya matukio, kwenye *crime scene*, hivyo, uchunguzi wake unaweza kuchukua muda zaidi kutegemeana na aina ya sampuli na eneo zilipotoka.

(b) Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali katika kuongeza mashine za kutosha ili kuwezesha uchunguzi ufanyike kwa wakati kwa vielelezo vya makosa ya jinai, ikiwa ni pamoja na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na

watoto, Serikali imedhamiria kununua mashine tatu za vipimo vya vinasaba (*DNA*) ili vitumike katika maabara za kanda, na hivyo kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018.

(c) Mheshimiwa Spika, vipimo vya vinasaba (*DNA*) kwa ajili ya uhalali wa watoto kwa wazazi (*paternity*) na kesi za jinai (*criminal case*) vinafanywa na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na sio Hospitali ya Muhimbili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Chumbuni, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amenipatia, naomba kuulizwa swali, je, haoni sababu ya majibu ya vipimo kutoka Zanzibar ambako amesema huwa yanachukuwa muda mrefu kutokana na umbali yanapotoka. Lakini Zanzibar na Tanzania Bara, Dar es Salaam ambapo anapatikana Mkemia Mkuu kwa sasa hivi hakuna umbali, ni dakika 20 mpaka nusu saa inaweza kufika. Je, haoni kutoa kipaumbele kwa vipimo ambavyo vinatoka Zanzibar kupewa majibu ya haraka, kwa sababu watu wamekuwa wakipata matatizo ya kusubiri muda mrefu huku wengine wanakuwa wapo katika magereza kwa kusubiria *criminal cases* zao ziweze kupatiwa majibu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, tunaona kuna haja ya kutoa kipaumbele kwa sampuli za makosa ya jinai zinazotokea Zanzibar lakini ni ngumu sana kutoa kipaumbele kwa msingi huo kwa sababu kama ni kesi za jinai zipo nchi nzima na watu wa kila kona ya nchi hii wana haki ya kupata haki ya kusikilizwa kwenye mahakama zetu kwa wakati bila kucheleweshwa. Tunachokifanya kama Serikali kwa sasa, ili kupunguza ucheleweshwaji, ni kuongeza idadi ya mashine za kupima vinasaba ili kwa ujumla wake kupunguza

ucheleweshwaji kwa sampuli zote kutoka kila kona ya nchi yetu, Zanzibar ikiwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu wa fedha, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, tumetenga bajeti ya kununua mashine tatu mpya za vinasaba lakini pia tunaanzisha kituo cha kupima vinasaba pale Mbeya ambacho pia kitatusaidia kupunguza wingi wa *case files* kutoka kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na Kanda ya Kati ambazo zinaweza zikatimia huduma za maabara itakayokuwepo pale Mbeya badala ya kutumia maabara moja iliyopo kule Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji si wa makusudi, ucheleweshwaji ni wa kitaalam kwa sababu kuna vigezo vingi ambavyo vingepaswa kuwepo kabla sampuli hazijapatiwa majibu kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa haraka ikiwemo kujenga uwezo wa wachunguzi wetu wa makosa ya jinai kwa maana ya Jeshi la Polisi wa namna ya *ku-navigate* kwenye *crime scene* na kuchukua sampuli. Lakini pia namna ya kujua ipi ni sampuli ya maana na ipi sio sampuli ya maana kwenye kesi hii, lakini pia mlolongo wa mpaka sampuli kufika kwenye maabara nao ni mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwa sampuli kutoka Zanzibar ni lazima wachunguzi wakamilishe uchunguzi wao, wakusanye sampuli, wazipeleke kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kule Zanzibar naye aridhike kwamba sampuli zinajitosheleza ziweze kuletwa huku Dar es Salaam kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile lazima kuwe kuna ucheleweshwaji, majibu pia yana mlolongo huohuo kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali Maabara, kwenda mpaka kule. Na wataalam tulionao pia ni wachache, kwenda kutoa ushahidi kwenye kesi mbalimbali nchi nzima nayo pia ni sababu nyingine ya ucheleweshwaji.



Na. 78

### Tohara kwa Wanaume

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Tohara kwa wanaume imethibitika kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa kiasi kikubwa.

(a) Je, kwa nini Serikali isiagize tohara kuwa ya lazima kwa wanaume wote?

(b) Je, elimu kuhusu tohara imefikishwa kwa wananchi kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si rahisi kwa Serikali kuagiza tohara kuwa lazima kwa wanaume wote nchini japokuwa tohara ina faida kubwa sana kiasia kwa wananchi wetu. Wizara iliweka mikakati ya kubaini mikoa ya kipaumbele ambayo haina utamaduni wa kutahiri na ina kiwango kikubwa cha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kutoa huduma ya tohara kama afua rasmi. Mikoa hiyo ni 14 ambayo ni Iringa, Njombe, Tabora, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera na Musoma. Itakapofika mwezi Oktoba, 2017 mikoa mipya minne ambayo ni Singida, Kigoma, Mara na Morogoro itaongezwa na hivyo kufikisha idadi ya mikoa 17. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, elimu kuhusu tohara imefikishwa kwa wananchi kwa kiasi kikubwa ambapo Serikali kwa kushirikiana na wadau wake katika mikoa ya

kipaumbele imekuwa ikitoa elimu kabla na baada ya huduma ya tohara katika vituo vya kutolea huduma za afya na wakati wa huduma mkoba zinazotolewa ngazi ya jamii kupitia kampeni mbalimbali. Serikali iliendesha Kampeni kubwa ya Tohara maarufu kama Dondosha Mkono Sweta ambapo elimu kuhusu tohara ilitolewa kupitia matangazo na vipindi vya redio na televisheni, mabango, machapisho, vijarida mbalimbali, filamu na waelimisha rika.

**SPIKA:** Hili swali gumu hili, Mheshimiwa Hawa Ghasia, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kama vitabu vyetu vyote vya dini vinasisitiza tohara, na pia tafiti zinaonyesha katika maeneo ambayo hakuna tohara ya wanaume maambukizi ya UKIMWI ni makubwa kushinda viwango vya Kitaifa, sasa kwa nini Serikali inapata kigugumizi katika kulazimisha suala hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; kama magonjwa mengine yote yanapewa chanjo, yaani chanjo inakuwa ni lazima kwa ajili ya kuinga magonjwa haya, kwa nini tohara kwa upande wa wanaume isiwe lazima ili na yenyewe iwe kinga ya kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kupunguza gharama kubwa kwa Serikali ya kuhudumia ugonjwa huo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa hiyo Mheshimiwa Hawa, si wanasema kuongoza ni kuonyesha njia, kwa hiyo tuanze na hapa Bungeni au? Majibu tafadhali. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali inapata kigugumizi, Serikali haina kigugumizi chochote kwenye jambo hili. Tunachokifanya kwanza kwa ujumla ni lazima ieleweke dhana ya ridhaa, kwenye huduma za afya, kwenye huduma za tiba, kuna kitu kinaitwa *consent*, sasa kunaweza kukawa kuna ridhaa ambayo inatolewa kwa mtu

moja kwa moja kwenda hospitali yeye mwenyewe kwa ridhaa yake kwa sababu anaumwa na amefika hospitali. Pale hatutamuliza kama anaruhusu tukutibu kwa sababu yeye mwenyewe amekuja hospitali na kwa msingi huo anataka kutibiwa, kwa hiyo yule ameshatoa ridhaa ambayo ni ya yeye mwenyewe kutaka kwenda hospitali kwa sababu amefika hospitali kwa sababu anaumwa. Lakini kwenye mambo yote yatakayohusu upasuaji, vipimo, ni lazima pia kuwe kuna ridhaa kutoka kwa mgonjwa na kama mgonjwa hajitambui kutoka kwa ndugu zake, huo ndiyo msingi wa huduma za tiba duniani kote.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye suala hili la tohara, kwa sababu ni jambo la hiari kama vile ilivyo kwa matibabu mengine yote, ni lazima mtu atoe ridhaa yake ndiyo aweze kupatiwa huduma ya kufanyiwa tohara, na haiwezi hata siku moja kuwa ni jambo la lazima na kwa msingi huo, Serikali haina kigugumizi chochote kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie nafasi hii kutoa rai kwa akina mama wote nchini kutumia fursa ya kuwashawishi wenza wao watafute...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, kelele zimezidi sana, tutulie tu. Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea na majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa akina mama wote nchini kutafuta wakati muafaka wakiwa na wenza wao kuzungumza nao kwa upole, kwa heshima na upendo wa hali ya juu wale akina baba ambao wanashiriki nao tendo la ndoa ambao hawajafanyiwa tohara. Hii itasaidia kuwashawishi wanaume wao wenyewe kwa hiari yao waende kwenye vituo vinavyotoa huduma za tohara ama kwenye huduma mkoba ambazo zinazunguka kwenye mradi wetu kama nilivyosema hapo, kwa sababu tohara inapunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa kiwango cha asilimia 60, sio kitu kidogo, ni kitu kikubwa. Lakini pia tohara inaepusha maambukizi ya vinasaba vya *Human*

*Papilloma Virus (HPV)* ambavyo vimekutwa kwa zaidi ya asilimia 80 kwa akinamama ambao wana saratani ya shingo ya kizazi. Kwa hiyo, ni muhimu sana akina baba wakafanyiwa tohara. Na akina mama watumie fursa wakati muafaka wawasihi wenza wao waende wakafanyiwe tohara kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa chanjo ni lazima *why not* tohara? Nafikiri majibu yangu kwenye jibu langu la awali yanajitosheleza. Tohara hata kama ni kitu ambacho kingesaidia kupunguza maambukizi ya Saratani kama hivyo nilivyosema ama kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI lakini bado ili kumfanyia mtu ni lazima kuwe na hiari yake na hatuwezi kufanya vinginevyo.

**SPIKA:** Bado kuna maswali ya nyongeza Waheshimiwa? Sisi Dodoma tumeendelea tangu zamani wanawake, wanaume wote tu sisi. Mheshimiwa Khatib nakuona. (*Kicheko*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ulilolisema siyo geni kwasababu Bunge la Zimbabwe waliweka jando pale nje ya Bunge na Wabunge wakafanyiwa hili jambo kwahivyo tutaiga jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa vile tafiti zimeonyesha ukiachilia mbali faida ya kuepuka majanga ya UKIMWI kwa kufanya tohara kwa wanaume. Tafiti zimeonyesha kwamba wanaume waliotahiriwa wanakuwa *active* zaidi na wananogesha zaidi yale mambo. Je, katika hali hiyo, Wabunge Wanawake kupitia Bunge hili hamuoni mtoe ushahidi kidogo wa haya ili Wabunge waliokuwa hawajatahiriwa waige mfano huo? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Hilo nalifuta siyo swali. Mheshimiwa swali la mwisho la nyongeza nimekuona endelea. (*Kicheko*)

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kuna baadhi ya makabila wanatumia njia za kienyeji badala ya

kwenda kufanyia tohara vijana wao katika hospitali njia ambazo zinasababisha wakati wa kuwafanyia tohara wakati mwingine kutokwa na damu nyingi na kupoteza maisha. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu kuwapa elimu ili waweze kupeleka vijana wao katika hospitali zetu?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri kwa kifupi kuhusu kavukavu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni rai yetu kwenye Makabila ambayo yana utamaduni wa kufanya tohara za kiasili maarufu kama kavukavu kama ulivyosema kuwaomba watumie huduma hiyo ya kutoa tohara kwa kwenda kwenye hospitali na kufanyiwa huduma ya tohara ya kitabibu yaani *medical circumcision* ili kuepukana siyo kutokwa damu nyingi, lakini pia kuepukana na uwezekano wa kuambukizwa magonjwa mbalimbali kwa sababu kule wanakofanya tohara ya kiasili kuna uwezekano mkubwa wakachangia vifaa vya kufanyia tohara yenyewe na hivyo kuhamisha vimelea vya magonjwa, kwa mfano homa ya ini ama virusi vya UKIMWI kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine kwahiyo, nitumie jukwaa lako hili kutoa rai kwa Mangariba wote kwenye makabila ambao wanatoa tohara ya kiasili kuanza kutumia tohara ya kitabibu kwenye hospitali zetu.

**SPIKA:** Wizara ya Maji na Umwagiliaji swali la Mheshimiwajasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini.

Na. 79

### **Mradi wa Maji-Maruku**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Kuna mradi mkubwa wa maji wa siku nyingi pale Maruku (Kyolelo) ambao miundombinu yake mikubwa kama matanki, mabomba chini ya ardhi na vyanzo vyake ni vizuri

lakini kutokana na uchakavu mradi huo hautoi maji; mradi huo ulikuwa ukihudumia vijiji vitano katika Kata za Kanyangeneke na Maruku; kukarabati miundombinu iliyochakaa inaweza kugharimu kiasi kidogo cha fedha kama shilingi milioni 500 kwa kuhudumia vijiji vitano wakati mradi mmoja kwa kijiji kimoja wa miradi inayoendelea unagharimu zaidi ya shilingi milioni 800.

Je, Serikali haioni ni busara kuukarabati mradi huu haraka?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa Maji wa Maruku-Kanyangereko ni miongoni mwa miradi iliyoanza kujengwa baada ya Tanzania Bara kupata Uhuru mwaka 1961. Mradi ulijengwa na ulikamilika mwaka 1977 na kuanza kutoa huduma. Mradi huu ulikuwa ukiendeshwa na Serikali chini ya usimamizi wa Idara ya Maji ngazi ya Mkoa. Hadi kufikia mwaka 1983, mradi ulikuwa unafanya kazi lakini ulisimama kwasababu ya wananchi kutochangia fedha za uendeshaji na matengenezo ikiwa ni pamoja na kuhujumiwa kwa miundombu ya mradi. Aidha, wananchi hawakupewa elimu ya kutosha ya kutambua kuwa mradi huo ni wa kwao na wanatakiwa kuutunza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imewasilisha maombi Wizarani ya kukarabati mradi huu kupitia miradi ya maji iliyoko kando kando ya Ziwa Victoria itakayofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la maendeleo ya *JICA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba imepanga kutekeleza mradi huu kupitia Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP II*) na inatarajiwa kuwa mradi huu utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018

ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.278 kimetengwa kwa ajili ya Halmashauri ya Bukoba. Ukarabati wa mradi huo utatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jasson Rweikiza swali la nyongeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba lengo la Serikali ya CCM ni kuwapatia Wananchi wengi maji safi na salama kwa gharama nafuu na ndiyo maana kuna miradi ya vijiji vingi nchi nzima kila Halmashauri ya kupeleka maji kwa wananchi na miradi hii inagharimu takribani kila mradi shilingi milioni 700 au 800. Mradi huu ninaoulizia swali, ulikuwa unahudumia vijiji sita; vijiji hivyo ni Maruku, Butairuka, Bwizanduru, Bulinda, Butayaibega na Buguruka. Mradi huu kama ungekarabatiwa haraka ungegharimu kama shilingi milioni 500 au 400 kwahiyo ni gharama nafuu na maji yangepatikana kwenye vijiji vyote hivi pamoja na Chuo cha Kilimo cha Maruku, shule kadhaa zipo pale za sekondari na za msingi. Sasa Serikali haioni kama ni busara mradi huu ukarabatiwe haraka wananchi wapate maji safi na salama?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer* Lwenge.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba kuna umuhimu wa huo mradi kukarabatiwa ili uweze kutoa maji kwa namna jinsi ulivyokuwa umepangwa na kwenye jibu la msingi nimeeleza kwamba nia hiyo ipo na tayari Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 1.278 katika kuetekeleza miradi ya Halmshauri ya Bukoba lakini vipaumbele ni mradi upi wanaanza nao, wanaamua kule kule kwenye Halmshauri na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni sehemu ya Baraza la Madiwani katika kuweka vipaumbele na kwa sababu mradi huu tayari umeshakubaliwa na Serikali, kwa hiyo mimi ningeshauri kwamba upe kipaumbele ili tukarabati na hivyo vijiji anavyosema viweze kupata maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete nilikuona.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kuwa matatizo waliyonayo wananchi wa Bukoba Vijijini yanafanana moja kwa moja na matatizo waliyonayo Wananchi wa Chalinze na kwa kipindi kirefu sana wamesubiri maji na sasa hivi hawaoni kinachoendelea. Sasa swali langu, Mheshimiwa Waziri ni lini mkandarasi yule utamfukuza ili wananchi wa Chalinze wajue wanaanza upya? Swali langu la kwanza na swali la pili, nini mpango mkakati sasa wa kuwakwamua wananchi wa Chalinze? Ahsante sana.

**SPIKA:** Swali moja tu. Mheshimiwa Waziri majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli pale Chalinze kuna mradi Awamu ya Tatu ambao unatekelezwa na Kampuni moja kutoka India (OIA) na utendaji wake wa kazi hauridhishi na tulikuwa tumetoa muda kwamba mpaka mwezi wa kumi awe amefikisha mahali ambapo Serikali inaweza kumruhusu au kufuta mkandarasi yule. Tunafuatilia kazi hiyo kwa karibu sana, naomba nikuhakikishie Bunge hili kwamba ikifikia mwezi wa kumi na hakuna kazi ya maana inayoendelea pale, tutachukua hatua zaidi za kimkataba.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea waheshimiwa Wabunge na swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 80

### **Miradi ya Maji Kutoa Huduma Chini ya Kiwango**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Kuna miundombinu ya kusambaza maji safi na salama iliyokamilika lakini inatoa huduma chini ya kiwango cha ujenzi wake (*below design and built capacity*).



(a) Je, ni miradi mingapi ya maji safi na salama inayotoa huduma chini ya uwezo wa usanifu na ujenzi wake kutokana na vyanzo kupungua au kukauka maji?

(b) Je, ni hatua zipi zinachukuliwa kuepusha miradi mingine kukumbwa na matatizo kama hayo?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi iliyosanifiwa na kujengwa inaweza kutoa huduma ya maji chini ya kiwango kutokana an sababu mbalimbali ikiwemo uchakavu wa miundombinu iliyojengwa, ongezeko la matumizi, uharibifu wa miundombinu, kupungua au kukauka kwa vyanzo vya maji kunakoweza kusababishwa na uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za kibinadamu na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa takwimu hivi sasa jumla ya miradi 114 nchini kote imebainika kutoa huduma ya maji chini ya kiwango tofauti na ilivyosanifiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha miradi mingine kukumbwa na matatizo kama hayo, Wizara imeandaa na inatekeleza mkakati wa kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji wa mwaka 2014 na mpango wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi wa mwaka 2013 ili kuhakikisha vyanzo vya maji vinakuwa endelevu.

Mpango huo unatekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa kutoa elimu kwa wananchi ambao wananchi wanahamasishwa kutokufanya shughuli za kibinadamu katika umbali usiopungua mita 60 kutoka kwenye mito na vijito na mita 500 kutoka kwenye bwawa na kuondoa watu wote wanaofanya shughuli za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo vya maji na maeneo oevu kwa maeneo hayo kupandwa miti rafiki kwa ajili ya kurejesha uoto wa asili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Katika jibu lake la msingi amekiri kwamba kuna miradi 114 ambayo imekuwa haiendelei au imeharibika kabisa na katika miradi hiyo 114 mmojawapo ninaoufahamu mimi ni ule wa Kili Water kule Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali itahakikisha imekarabati mradi huo ili kuondoa adha ya Wanawake wa Tambarare ya Rombo kubeba ndoo za maji Alfajiri na mapema walio katika Kata ya kule Ngoyoni, Mamsera chini pamoja na wale ambao wako kule pembeni ya Ziwa Chala?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tambarare yote ya Mkoa wa Kilimanjaro imekumbwa na adha hii ikiwoko Wilaya ya Mwangi, Same Mjini mpaka kule Hedaru. Ni lini sasa Serikali itakamilisha ule mradi wa maji wa Ziwa la Nyumba ya Mungu ambao utapeleka maji kupitia Mwangi, Same, Hedaru mpaka Mombo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji *Engineer* Lwenge.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali kumpongeza sana Mbunge kwa maana kwamba anafuatilia kuona namna gani miradi hii inaweza kuathiri matumizi ya wananchi kwa maana kwamba maji yamekuwa yanapungua kwa namna hali ya hewa inavyobadilika. Kwa hiyo ni jambo ambalo ni la msingi lakini pia ni lazima tuchukue hatua. Hatua mojawapo ni lazima sisi sote tuhakikishe kwamba tunalinda vyanzo vya maji lakini pia tupande miti ambayo ni rafiki lakini pia tuvune maji ya mvua kwasababu rasilimali za maji zinapungua mwaka hadi mwaka kama hatuchukui hatua yoyote ya kukabiliana na tatizo hilo. *(Makofi)*

Sasa kuhusu mradi ambao unasema ni lini utakarabatiwa, Mkoa wa Kilimanjaro Serikali kwa mwaka huu wa 2017/2018 tumetengea shilingi bilioni 8.95 kwa ajili ya kumaliza miradi inayoendelea lakini pia kukarabati miradi ambayo ipo haifanyi kazi katika kiwango kwahiyo watumie fddha zile katika kuangalia vipaumbele na kuona kama wanaweza kukarabati kwa mwaka huu wa fedha vinginevyo wapange katika mwaka wa fedha unaofuata.

Kuhusu swali lake la pili, mradi wa Nyumba ya Mungu kupeleka maji Mwanga mpaka Same, sasa hivi mkandari huko mwanzo alikuwa anusua sua lakini sasa hivi anakwenda kwa kasi na nina uhakika kwamba mradi ule utakuja kukamilika lakini pia tumeanza na awamu nyingine ya kupeleka maji kule Same nayo Mkandarasi yupo *site* na kazi inakwenda vizuri. Serikali inafuatilia kwa nguvu zote ili miradi hii iweze kukamilika.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, Mbunge wa Songea Mjini. Mheshimiwa Gama tafadhali.

Na. 81

### **Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mradi wa Bwawa la Maji-Songea Mjini**

**MHE. LEONIDAS T. GAMA** aliuliza:-

Wananchi wangu wa Jimbo la Songea Mjini katika eneo la Matogoro, Mahiro, Lihira na Chemchem walitoa maeneo ya kilimo na makazi kwa SOUWASA ili kutengeneza bwawa la maji kwa Mji wa Songea toka mwaka 2003 na jumla ya wananchi 872 walifanyiwa uthamini wa mali na nyumba zao. Mwaka 2015 uthamini ulifanyiwa marejeo (*review*) na jumla ya kiasi cha shilingi 1,466,957,000 iliidhinishwa na Serikali kama madai halali ya wananchi hao lakini hadi leo ni miaka 14 imepita wananchi hao hawajapewa stahili zao.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kitendo hiki cha kutowalipa wananchi haki zao ni kuwaongezea umaskini wa kipato, malazi na kukosa uwezo wa huduma za matibabu na elimu?

(b) Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hao stahiki yao walipotakiwa kulipwa miaka mingi iliyopita?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, Mbunge wa Songea Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Serikali ililipa kiasi cha shilingi 20,695,051 kwa wananchi 64 kwa ajili ya fidia ya Wananchi waliopisha ujenzi wa miundombinu ya Bwawa la Ruhila. Wananchi hao ni wale ambao walikuwa nje ya mita 60. Wananchi 872 ambao walikuwa ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha Mto Ruhila walifanyiwa tathmini mwaka 2003. Kwa mujibu wa Sheria ya mazingira ya mwaka huo wa 2004 wananchi hao hawastahili kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, wananchi hao walitoa malalamiko yao kwa Serikali ambapo Serikali imepitia Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 na kuona kwamba ilitungwa wakati Wananchi wameshafanyiwa tathmini. Aidha, tathmini hiyo ilipitiwa upya mwaka 2015 na kubaini jumla ya shilingi 1,466,957,000 zinahitajika kulipwa fidia. Serikali imepanga kulipa fedha hizi fidia katika mwaka wa fedha 2018/2019.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gama.

**MHE. LEONIDAST. GAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Songea Mjini katika maeneo hayo niliyoyataja niishukuru sana Serikali kwa kutupa matumaini kwamba fidia hiyo italipwa kipindi cha bajeti ya fedha mwaka 2018/2019. Sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, katika eneo hilo wapo wananchi 157 ambao wanadai kwa namna moja ama nyingine majina yao yaliondolea kwenye eno la fidia. Sasa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, Serikali iko tayari kufuatilia ukweli juu ya wananchi hawa 157 ili ukweli ukijulikana walipwe fidia zao?

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wananchi wa aneo hilo pamoja na kupata maji kutoka hilo bwawa lililotengenezwa lakini bado kuna migogoro mingi kati yao na *SOUWASA*. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda Songea ili kukutana na wananchi wa eneo hilo ili kuwasiliza matatizo yao na kutatua? Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu ya Wananchi wa Songea Mjini Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inaipokea hiyo shukurani aliyoitoa, lakini kuhusu wananchi 157 ambao inaonekana wako nje ya wale 872 tutakwenda kufuatilia na ninamuomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili nitakwenda Songea, nitakwenda kuona hali halisi na tuweze kuchukua hatua kwa Wananchi wale ambao bado wanadai hiyo fidia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtaona muda wetu tunatakiwa tuanze mambo mengine. Kwanza niwataarifu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko safarini Dar es salaam kwa kazi nyingine muhimu za Taifa kwa jinsi hiyo mtaona Dawati pale aliyekaba-*row-off* ni Mheshimiwa Maghembe kwahiyo kwa mambo yote ya Kiserikali mnaweza mkamuona Mheshimiwa Profesa Maghembe kwa nafasi hiyo. Tunashukuru sana Mheshimiwa Maghembe kwa uwepo wako hapo.

Kuhusu wageni walioko Bungeni nianze na wageni walioko Jukwaa la Spika; kwanza kabisa Waheshimiwa Wabunge ninaye mgeni maalum kabisa naye si mwingine bali ni Spika wa Baraza la Wawakilishi-Zanzibar, Mheshimiwa Zubeir Maulid. (*Makofi*)

Karibu sana Mheshimiwa Zubeir. Huyu Mheshimiwa, mimi, yeye na Mheshimiwa Mhagama tulikuwa ndiyo Wenyeviti wa Bunge wakati wa Bunge la Tisa la Mheshimiwa Samwel Sitta, tulikuwa tukiitana pacha, kwa hiyo, pacha karibu sana. *(Makofi)*

Wako watu husemasema unajua Bunge la Tisa, Bunge la Kumi yalikuwa bora kuliko hili, hawajui kama na sisi tulikuwepokuwepo pale pale, kwa hiyo, sifa zote hizo na sisi tunazo, ushahidi ni huo, mwenzangu kule na mimi huku maana yake tulillelewa vizuri jamani. *(Makofi)*

Pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi ambao mmefuatana na Mheshimiwa Spika, naomba msimame pale mlipo. Karibuni sana. Wamekuja kwa ajili ya shughuli maalum ambayo tutawaeleza baadaye kidogo. *(Makofi)*

Pia wamefuatana na Ndugu Abubakar Mahmoud Iddi – Katibu wa Spika, karibu sana. *(Makofi)*

Vilevile tuna wageni nane wa Mheshimiwa Leonidas Gama ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Songea na Watendaji wa Halmashauri hiyo wakiongozwa na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea, Mheshimiwa Abdul Mshaweji. Waheshimiwa karibuni sana Dodoma, tunawakaribisha. *(Makofi)*

Baada ya kumaliza wageni wangu, sasa niendeleo na wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 30 wa Mheshimiwa Rehema Migilla ambaye ameapishwa leo ambao ni ndugu na jamaa zake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam waliokuja kushuhudia kuapishwa kwake wakiongozwa na baba yake Ndugu Juma Migilla. Wageni wa Mheshimiwa Migilla karibuni sana Dodoma, mmemleta, mmemfikisha sasa huyu ni wa hapa hapa. Ninyi baadaye mnaweza mkaondoka tu hakuna shida, yuko mikono salama kabisa. *(Makofi)*

Wageni 29 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa hapa hapa ambao

ni wanafunzi na Walimu kutoka Chuo cha Sila kilichopo Moshi Mkoani Kilimanjaro. Wanafunzi wale wa Sila, ooh, mmependeza kweli kweli. Karibuni sana wanafunzi kutoka Moshi, mmemwona na mama yenu Mheshimiwa Shally Raymond yuko hapa, natumaini baadaye mtaonana huko. *(Makofi)*

Wageni 135 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambao ni wanafunzi 130 wa Kidato cha Sita na Walimu watano wa Shule ya Sekondari ya Jamhuri ya Mkoani Dodoma. Oh, karibuni, hawa ni watoto wa nyumbani, yange yange. Wasiojua Jamhuri ni ile shule iko karibu na Uwanja wa Jamhuri pale pembeni. Karibuni sana watoto wetu mjifunze kuhusu Bunge. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma. Wale wanamaombi karibuni sana, tunawakaribisha muendeleo kutuombea ndugu zangu, tunahitaji sana maombi yenu. *(Makofi)*

Baada ya hayo, niseme machache yafuatayo. Kwanza hali ya Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge mwenzetu aliyeko katika Hospitali ya Nairobi anaendelea na matibabu vizuri, madaktari wake wanaendelea kumpa huduma na taarifa tunazopata zinatia moyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua kwa majeraha aliyoyapata kunahitajika operesheni kadhaa, madaktari wanaenda kwa awamu. Walifanya ile awamu ya kwanza hapa Dodoma, walipoenda kule Nairobi wakafanya awamu nyingine, sasa wanaendelea na awamu nyingine kufuatana na programu yao. Kwa ujumla wake tunamshukuru Mungu kwamba wanaendelea kumhudumia, yuko katika maumivu magumu sana na wakati mgumu lakini anaendelea kupata matibabu tuendeleo kumwomba, Mwenyezi Mungu ndiye muweza wa yote.

Waheshimiwa Wabunge, miongoni mwa wanazuoni huwa kuna mjadala usioisha wa nani mkubwa kati ya Serikali,

Mahakama na Bunge. Mjadala huo huwa hauishi kwa sababu mwisho wa siku kuna wanaofikiri au wanasema kwamba Serikali ndiyo mkubwa, kuna wanaofikiri na kusema Mahakama ndiyo mkubwa na wana sababu zao na ni za msingi kweli kweli na kuna wanaofikiri na kusema kwamba Bunge ndiyo mkubwa nao hao wana sababu zao nzito. Mimi sio mmoja wa waumini wa sababu zozote zile katika makundi hayo ikiwa ni pamoja ya hili la kwetu sisi kwa sababu ni mjadala mkubwa wenye sababu nyingi sana unafika mahali inategemea na nchi yenyewe ilivyo na mazingira yake.

Waheshimiwa Wabunge, wale ambao wanasema Bunge ni mkubwa, wao huwa sababu zao ni zifuatazo; kwa kifupi sana. Wanasema Bunge linatunga sheria, ndiyo maana ni mkubwa. Mahakama inatafsiri sheria zilizotungwa na Bunge, sasa wewe kama unaletewa halafu ndiyo unatafsiri basi aliyekuletea ndiyo mkubwa japo unaweza ukafuta baadhi yake, hao wanavyofikiri. Wanasema Serikali yenyewe inatekeleza sheria ambazo zimetungwa na Bunge, kwa hiyo Bunge ndiyo mkubwa, hao wanaofikiri hivyo, nimesema mimi siyo mmoja wao.

Kwa hiyo, mara nyingi lawana nyingi zinazotupwa kwa Bunge huwa zaidi ni kwa wale waofikiri kwa utaratibu huo. Kwa hiyo, hutupa lawana nyingi sana kwa Spika, kwa Bunge hata zile ambazo kwa kweli wakati mwingine siyo lazima sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla ningepomba tuwe makini sana tunapokuwa tunalizungumzia Bunge letu wenyewe na hasa tunapokuwa tunamweka Spika katika, Kiingereza wanasema *bad light* bila sababu kwa sababu kwa kufanya hivyo tunaibisha taasisi yetu. Kama ni la kweli sema, kama si la kweli si vizuri sana. Mimi huwa siyo mtu ninaye jibu jibu sana mambo, Mheshimiwa Zubeir Maulid yuko hapa na wengine mliokuwepo Bunge la Tisa, moja ya sifa za Mheshimiwa Sitta ni kwamba alikuwa anajibu papo kwa papo kwa kila jambo yaani anaanza nalo hilo hilo, sasa mimi huwa sijibu haraka kwa hiyo inachukua muda, kila mtu yuko vile alivyo.



Waheshimiwa Wabunge, upo upotoshaji mwingi ambao huwa unatembeatembea, huwa sijaribu kujibu kila mmojawapo lakini mengine haivumiliki. Kwa mfano, Mheshimiwa Kubenea mara kadhaa amekuwa akifanya vitu ambavyo kwa kweli vinafedhehesha taasisi yetu na wakati mwingine mimi mwenyewe. Kuna maneno ameyasemasema huko kwenye Makanisa asijue kwamba madhabahuni ni mahali Patakatifu inatakiwa useme ukweli mtupu, yeye anayasemasema tu. Kwa hiyo, kwa hayo aliyoyasema ambayo sitaki kuyarudia naagiza yafuatayo:-

(i) Kamati ya Mheshimiwa Adadi ambayo inashughulikia yale mambo yetu ya usalama wa Wabunge imuite haraka sana ili aende kuisaidia kwa sababu inaelekea anafahamu vizuri zaidi kuhusu yaliyompata Mheshimiwa Tundu Lissu na kadhalika. Kwa hiyo, aje aisaidie Kamati.

Moja, alilonituhumu mimi ni kwamba nimelidanganya Bunge kwa kutaja idadi chache za risasi ambazo zilipigwa kwenye gari la Mheshimiwa na wakati nasoma taarifa ile ambayo niliisoma kwa taratibu sana na kwa upole sana nilieleza idadi ya risasi na nikasema nukuu yangu ni kutoka kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma na nikamtaja na jina lake. Kwa hiyo, ukinituhumu mimi kwamba nimelidanganya Bunge ndugu yangu basi maiteni na yeye atakuwa anaelewa vizuri hizo risasi na aina ya bunduki kutaja, atawasaidia vizuri zaidi. Maana wakati mwingine tunashughulishwa hapa kumbe matatizo yako humu humu, yeye anaelewa vizuri zaidi. Kwa hiyo, maiteni haraka. *(Makofi)*

(ii) Haya ya Spika kwamba ni mwongo, hayo Kamati ya Maadili maiteni huyu huyu aende naye akathibitisha uongo wa Spika aliosema madhabahuni maana kausema kwenye Kanisa. Nafikiri tunajua wote jinsi ambavyo vitabu vyote vya dini vinasema usiseme uongo. Sasa Mheshimiwa Mbunge ukisema uongo tena madhabahuni hatuwezi kulichukulia kama ni jambo dogo.

Kwa hiyo, Kamati zote mbili zilishughulikie kwa kadri watakavyoona linafaa lakini tukianza na Kamati ya Adadi

kwa haraka. Kwa hiyo, popote pale alipo naagiza Katibu wa Bunge huyu Mheshimiwa atafutwe, aletwe kwenye Kamati ya Adadi kesho, kwa utaratibu wowote ule. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, katika lile nililosema la *supremacy*, wako waliokuwa wanasema Mheshimiwa Spika alikosea utaratibu alioutumia katika ku-*handle* zile ripoti mbili, moja ya Almasi na nyingine ya *Tanzanite*, kwa nini hakuleta ripoti zile ndani ya ukumbi wa Bunge. Ni vizuri kufikiri hivyo, wala hamna tatizo lakini inapokuwa baadhi ya mambo haya yanafanywa na Wabunge wazoefu inakupa shida kidogo.

Mheshimiwa Zitto Kabwe na yeye akatutuhumu sana na akatuweka kwenye picha moja mbaya sana katika jamii. Kwa hiyo, ni vizuri akapata nafasi ya kusikilizwa pia katika Kamati ya Maadili, huenda ana sababu za msingi. Kwa hiyo, naye kwa wakati muafaka naagiza aitwe katika Kamati ya Maadili, ahojiwe kwa lugha zile alizozitumia katika mitandao kuhusiana na mhimili wa Bunge kuwa umewekwa mfukoni na mhimili fulani. Kwa hiyo, hilo nalo aje awathibitishieni, aje na vielelezo vyake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa sababu tuna na Wabunge wageni, wengine tumewaapisha leo wanaweza wasielewe haya mambo, yanataka ukae hapa muda kidogo uweze kuyafahamu. Kamati mbalimbali za uchunguzi wa mambo au ufuatiliaji huundwa kufuatana na Kanuni kwa utaratibu tofauti tofauti. Kamati inaweza ikaundwa au Tume ikaundwa kutokana na pendekezo linalotokana na Kamati za kawaida za Bunge ambapo pendekezo mnakuwa mmelileta hapa, kwa maana hiyo, Spika huwahoji ninyi, je, mnaafiki hiyo Tume iundwe? Mlio wengi mnasema 'ndiyo' basi inaundwa.

Chombo hicho kikiundwa au Mbunge mmoja wewe umeleta hoja yako lakini Wabunge wakiikubali humu ndani kwa hiyo chombo kikaundwa kwa ajili ya kufuatilia jambo hilo au utaratibu mwingine wowote kwa maana hiyo, basi taarifa hiyo italetwa pale pale kwa sababu ninyi ndiyo

mliosema kwamba chombo hicho kiundwe kiende kikafuatilie jambo hilo, ndiyo utaratibu wetu wa Kibunge. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, katika jambo hili la Almasi na *Tanzanite* ni lini mlihojiwa ninyi Wabunge na mkaazimia kwamba paundwe Kamati za kufuatilia mambo haya? Ni lini Mbunge yeyote kati yenu alisimama na kusema kwamba tuunde Kamati Maalum kwa ajili ya kufuatilia Almasi au *Tanzanite*? Anaitwa nani jina lake?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ni mimi Spika niliona busara ya jambo hilo, nikasema mimi, nikaunda mimi na nikaeleza historia ya jambo lenyewe kidogo kwamba na Kamati itafanyaje kazi. Nikasema Kamati hizi ni Kamati za ushauri, siyo za uchunguzi, za ushauri, lengo lake ni kuishauri Serikali lakini ni Kamati za Spika, watanileta ushauri wao na mimi nikaeleza pale wakati naunda, moja niliunda baadaye ya pili nikaunda kama baada ya wiki mbili. Kila moja nikaeleza maneno yale yale, watafuatilia mambo haya, wataniletea taarifa na mimi nitaipa Serikali kwa kumpa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu akiwa amekaa hapa ili Serikali iweze kutekeleza, nilieleza utaratibu wote. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Kamati zote zimefanya kazi nzuri kwa niaba yetu, zimemkabidhi Spika badala ya Spika kuikabidhi Serikali kimya kimya ambapo msiofahamu utaratibu huo hawa upo kwa mliokuwepo Bunge lililopita. Mheshimiwa Chenge yuko hapa, iliundwa Kamati kupitia Kamati ya Bajeti na ripoti mbili zikatoka. Moja inaitwa *Chenge One*, nyingine inaitwa *Chenge Two*, alikabidhiwa Spika aliyekuwepo na yeye akakabidhi Serikali kimya kimya. Sijui kama mnafahamu hata nini kiliandikwa zaidi ya wale Wajumbe wa ile Kamati. Akina Mheshimiwa Selasini walikuwa ni Wajumbe wa Kamati ile halafu ikawa imeisha. Utaratibu ni ule ule lakini baada ya kukabidhi ikawa

imeisha, nimeileta, tumeweka hapo nje, tumewaambia Watanzania wote na tumeifikisha kwenye mamlaka na mamlaka inachukua hatua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, eti kwa hayo yote bado tena ulalamikiwe lakini waliopeleka kimya kimya, wakimya, ndiyo hayo Mabunge hayo. Kwa hiyo, atakwenda huko ataeleza Mheshimiwa Zitto na yeye, naye amekuwa mtoro sijui kuna nini, huko Kigoma Mjini mjue Mbunge wenu mtoro hapa Bungeni, Spika hana taarifa zake yuko wapi na anafanya nini na nina hakika yuko Tanzania hii hii lakini Bungeni haji, mlimchagua Kigoma asije hapa Bungeni? (*Makofi/Kicheko*)

La mwisho, katika niliyotaka kuyasema kidogo ni la Mheshimiwa Ally Saleh. Alisema jana, nilikuwa sipo lakini leo kwenye Taarifa ya Upinzani nimeona amerudia tena kwenye utangulizi maneno yale yale. Ndiyo yale yale ninayosema rafiki zangu wanapenda kweli kumtuhumu Spika, mimi nataka kusema hivi hebu kila mtu mum-*study* vizuri mumfahamu, *I'm a smart person up here, really*. Kwa hiyo, unapokuja ujipange vizuri kidogo siyo tu ufikiri kwamba huu ufupi huu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Saleh anasema Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imesononeshwa na uamuzi wa Mheshimiwa Spika wa kuridhia, uamuzi wa kuridhia ndiyo *hallmark* yaani *catch word* na ameendelea kulaumu sana humu ndani hotuba rasmi na jana alisema humu ndani. Sasa niseme, mimi hakuna uamuzi niliofanya wala hakuna kuridhia nilikokuridhia kuhusu mabadiliko ya uongozi wa *CUF* humu Bungeni.

Nadhani ni vizuri kuwa makini kidogo kama nilivyosema, wajibu wangu mimi ni kutangaza, mimi Mbowe akinileta hapa, nimemwondoa Waziri Kivuli fulani, nimemweka sijui fulani, mimi hapa natangaza tu yaani mimi huko kwenye kikao chenu cha CHADEMA au *CUF* mimi mualikwa? Mimi natangaza tu kwamba jamani kuna mabadiliko, ni hivi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sakaya amenileta mabadiliko, mimi nimeyatangaza. Sasa wapi nimeridhia,

wapi nimefanyaje mpaka mnaweka kwenye hotuba rasmi za Kambi, ndiyo maana nasema muwe mnajipanga jamani. *(Makofi/Kicheko)*

Hapa nachukua nafasi hii kutangaza tangazo lingine, Mwenyekiti wa Kamati ya CUF, Mheshimiwa Maftaha Nachuma anawatangazia Wabunge wa CUF kikao leo Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kusitisha shughuli hizi mchana saa saba. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nikitangaza msinituhumu, mimi natangaza. Ndiyo wajibu wangu sasa nani atangaze? La sivyo matangazo yenu na ninyi msiniletee tu kwamba matangazo ya vyama sasa vya Upinzani au ya kambi yasiwe yanatoka. Kwa hiyo, uamuzi wangu ni kwamba *portion* hiyo huyu atakayesoma hii Taarifa isisomwe lakini akiona ni busara aisome halafu na yeye kesho Maadili halafu tutaona njia jinsi ya kwenda maana nimeshawatahadharisha tayari. Simzuii, akiona bora asome *portion* hiyo asome, iko kwenye utangulizi, akiona niliyosema ni sawa basi airuke. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya maelezo hayo...

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mimi nataka kuondoka hapa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, tumalizane kwanza.

**SPIKA:** Kama iko Miongozo Naibu ataichukua, tunapishana na Mheshimiwa Naibu hapa.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 67(7), leo asubuhi kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Silinde, Mbunge wa Momba aliliza Swali Na. 70. Swali lake lilihusiana na Shule za Jumuiya wa Wazazi CCM na kwamba katika Jimbo lake kuna shule ambayo ni miaka mingi haina wanafunzi. Mheshimiwa Spika, katika maswali ya nyongeza alimpatia mmojawapo swali la nyongeza ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya wa Wazazi wa CCM na akalijibia swali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, wote tunafhamu kwa kina kwamba kabla ya Mfumo wa Vyama Vingi tulichangia maendeleo ya Watanzania kupitia shule pamoja na viwanja vya michezo. Kwa muda mrefu sasa mali hizo ambazo CCM inamiliki zimekuwa kwenye nafasi mbaya ya kimtazamo kwa maana ya uchakavu. Naomba mwongozo wako kama inafaa kuishauri CCM kama wanaweza wakarudisha mali hizo kwenye Halmashauri zetu ili ziweze kusaidia wananchi kama kusudio la kwanza kabisa lilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako juu ya suala hili kwa sababu ni maeneo mengi wewe mwenyewe unafhamu tunahitaji shule na Mheshimiwa Silinde amelizungumzia vizuri sana kwamba wanahitaji majengo kwa ajili ya *form five*. Tunaonaje tukaizungumzia hili na hasa utupe mwongozo kama watu wa Momba wanaweza wakaendelea kuitumia ile shule badala ya kuitumia kisiasa na majibu ya kisiasa yaliyojibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba mwongozo wako kwa maelezo ambayo yametolewa hapa mapema na Mheshimiwa Spika ambaye alikuwa amekalia Kiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza wakati inatolewa hoja ya dharura hapa na Mheshimiwa Hussein Bashe mimi nilivyoelewa na huenda na wenzangu Waheshimiwa Wabunge walielewa hivyo ni kwamba sisi tulizungumza Kamati ya Ulinzi na Usalama ifanyie kazi masuala ya kiulinzi katika nchi hii *in totality* lakini Mheshimiwa Spika alivyozungumza hapa ni kama anazungumzia ulinzi wa Wabunge peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilivyoelewa na nikaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hussein Bashe ni kwamba tunazungumza mambo ya Ulinzi na Usalama wa nchi kwa sababu kuna matukio ambayo yametokea kwa Wabunge wenzetu lakini kuna mengine yametokea katika vyombo vingine huko mtaani kwa raia wa kawaida. Kwa hiyo, hiki chombo kina ulazima wa kushughulikia na kupata taarifa mbalimbali za ulinzi na usalama wa Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili naomba mwongozo wako, haya mambo ya wenzetu viongozi na Wabunge wa Chama cha Wananchi *CUF* yameleta kizungumkuti sana hapa Bungeni. Nilisikia matangazo yanatolewa ya mabadiliko ya viongozi lakini pia hata upangaji wa viti hapo mbele wako Mawaziri na Naibu Mawaziri Vivuli wa *CUF* ambao walipaswa *wa-take the first row* kwenye ukaaji wa viti hivyo, hilo jambo halijazingatiwa, wamepangwa vinginevyo, kwamba Wabunge wa kawaida wamepangwa kule mbele na wale Mawaziri na Naibu Mawaziri Vivuli wamepangwa huku nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchanganyiko huo naomba mwongozo wako, nyie kama Bunge hapa Bungeni mnamtambua kiongozi gani wa Chama cha Wananchi *CUF* ili tujue matangazo haya mbalimbali ambayo tunaelekezana mnapokea kutoka kwa nani? Ningeomba unipe mwongozo wako ili tujue kwamba huyo mnayemtambua kama Bunge, kama kiongozi wa Chama cha Wananchi *CUF* hapa Bungeni ni nani ili tujue matangazo hayo ni halali au siyo halali?

**NAIBU SPIKA:** Sawa, umeshaeleweka, Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi nasimama kwa kanuni ya 68(7). Kuna tabia ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara, kwa mfano, jana kama umeona katika *television* ya *ITV* kwenye taarifa ya habari, kuna tabia kwamba Wakuu wa Wilaya, Askari wetu wanakwenda katika vile vijiji ambavyo vinaonekana kwamba vipo katika hifadhi, nyumba zinachomwa, huku wananchi wakiwa wamesimama wamebeba malaika wa Mungu, watoto wadogo wanaangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona ile kwa kweli hatuko salama kwa sababu siyo jambo zuri malaika wa Mungu wale nyumba zinachomwa wanalala nje kwa sababu tu eti watu wako katika hifadhi. Naomba mwongozo wako hivi Serikali haioni njia mbadala ya kuwahamisha wale wananchi ambao wanaonekana wako katika hifadhi tena wakati mwingine ni baada ya kutangazwa upya kwamba hayo maeneo ya hifadhi yamewakuta wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, je, mahakama...

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo ni mmoja. Mheshimiwa Hawa Ghasia atakuwa wa mwisho.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka tu kutoa taarifa kwa aliyeomba mwongozo wa kwanza kwamba wakati tunaingia katika Mfumo wa Vyama Vingvi vya Siasa kulikuwa na sheria na taratibu na pia iliainishwa mali zipi zimeenda Serikalini na zipi zinabaki kwenye chama. Kwa hiyo, kama Wilaya yako wana shida na mali za Chama cha Mapinduzi...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.



**MHE. HAWA A. GHASIA:** Waende wakakiombe Chama cha Mapinduzi ili Chama cha Mapinduzi kione kama kuna haja ya kuwapa au la, badala ya kuja ndani ya...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia naomba ukae, Kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa Waitara.

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma zote hiki kitabu chote ni Kanuni kinaeleza kwamba anatakiwa asijibu...

**NAIBU SPIKA:** Kanuni iliyovunjwa, soma Kanuni ya 68(1) inakupa maelekezo taja Kanuni iliyovunjwa, ukishasema Utaratibu ni lazima utaje Kanuni, taja kanuni iliyovunjwa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni iliyovunjwa ni ya 68(7), tunaomba mwongozo kwako siyo kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naendelea kutoa taarifa kwamba wakati tunaingia katika Mfumo wa Vyama Vingi mwaka 1992, mgawanyo wa mali uliainisha zipi zinabaki ndani ya chama na zipi zinaenda Serikalini. Sasa kama Wilaya imeona jengo la Chama cha Mapinduzi ambalo labda wanalipenda waende wakaombe kwenye Chama cha Mapinduzi na siyo kuja kuomba ndani ya Bunge. Haiwezekani nyumba ya Hawa Ghasia ukamwombe Janet Mbene wakati Hawa Ghasia mwenyewe yupo. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nampa tu taarifa kwamba akaombe Chama cha Mapinduzi na siyo kuja kuomba Bungeni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo kadhaa hapa. Mwongozo wa kwanza umeombwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ametoa

maelezo kuhusu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Silinde kuhusu Shule za Wazazi zinazomilikiwa na CCM na kwamba kwenye Jimbo la Mheshimiwa Silinde kuna shule ambayo haina wanafunzi.

Kwa maelezo aliyoyatoa amesema kwamba, kwa kuzingatia watu wote nchi hii kabla ya Mfumo wa Vyama Vingi walichangia ikiwa ni pamoja na kuchangia mali zilizo chini ya CCM. Kwa mawazo yake Mheshimiwa Mwakagenda anasema CCM warudishe mali kwenye Halmashauri ili ziweze kusaidia wananchi na kwamba majibu yaliyotolewa hapa ni kana kwamba yametolewa kisiasa.

Kwa hivyo, kwa kifupi alikuwa anaomba mwongozo juu ya hayo majibu yaliyotolewa kuhusu hizi mali. Sasa nadhani kwanza tukumbuke siku zote kwamba Mheshimiwa Spika alishatoa mwongozo hapa kuhusu mwongozo unaoweza kuombwa juu ya majibu ya swali fulani na maelezo ya mwongozo huo ni kwamba anayepaswa kuomba mwongozo kuhusu majibu yaliyotolewa kuhusu swali fulani anapaswa kuwa ni yule mwenye swali. Kwa sababu hiyo, mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Mwakagenda maana yake ni kwamba swali lilijibiwa kikamilifu ndiyo maana mwenye swali hajauliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waitara ameomba mwongozo kuhusu maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Spika na ameeleza kwamba Mheshimiwa Spika maelezo aliyoyatoa yanahusu ulinzi wa Wabunge pekee na si ulinzi wa watu wote kwa ujumla kama ambavyo hoja iliwahi kuletwa hapa na Mheshimiwa Bashe na yeye kwa maelezo yake Mheshimiwa Waitara akaiunga mkono akijua kwamba itakuwa inajadili ulinzi wa watu wote na si Wabunge pekee.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo huu uliombwa na Mheshimiwa Waitara inabidi nipate maelezo yale aliyokuwa ameyatoa tayari Mheshimiwa Spika ndiyo niweze kujua kitu gani halisi kilisemwa. Kwa hivyo, mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Waitara utatolewa hapo baadaye.

Mheshimiwa Mbarouk ameomba mwongozo kuhusu taarifa ya habari ya *ITV* kwamba ilionyeshwa kuna nyumba zilikuwa zinachomwa ambazo ni za vijiji vilivyopo kwenye hifadhi. Mheshimiwa Mbarouk naomba uisome vizuri hiyo kanuni uliyotumia kusimama hapo inataka jambo liwe limefanyika hapa Bungeni ndiyo liweze kutolewa mwongozo na Kiti. Kwa hivyo, nyumba hazijachomwa hapa na wala hakukuwa na hoja hapa ndani kuhusu kuchomwa nyumba asubuhi ya leo kwamba unaiombea mwongozo. Kwa hiyo, maelezo yangu ni hayo kuhusu mwongozo wa Mheshimiwa Mbarouk.

Mheshimiwa Hawa Ghasia hakuomba mwongozo yeye alitoa maelezo ambayo nadhani mtu ambaye yanamhusu yameshamfikia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI- KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria  
Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2017 [The Written Laws  
(Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2017]**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2017 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2017] sasa Usomwe kwa Mara ya Pili na Bunge lako Tukufu liujadili na hatimaye liupitishe kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema sisi waja wake na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo huku tukiendelea kutimiza wajibu wetu wa kikatiba kwa ajili ya maslahi ya Watanzania na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Spika kwa uwezo wake mkubwa, hekima na busara katika kuongoza Bunge hili akisaidiwa na wewe Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Pia nampongeza kwa kuunda Kamati Maalum ambazo zilichunguza na kushauri juu ya mfumo bora wa uchimbaji, usimamizi, umiliki na udhibiti wa biashara ya madini ya almasi na *tanzanite* hapa nchini. Kwa hakika Bunge hili limeshiriki ipasavyo katika kulinda maliasili za nchi kwa maslahi ya Watanzania wote na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamisi Juma kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Wizara ya Katiba na Sheria ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kumpatia ushirikiano katika utendaji wa kazi zake na tunamwomba kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumjalilia afya njema, busara, hekima na ujasiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa majeraha na maumivu aliyoyapata baada ya kupigwa risasi mnamo tarehe 7 Septemba, 2017. Pamoja na juhudi kubwa za Madaktari, tunamwomba kwa Mwenyezi Mungu amwezeshe kupona mapema. Tunalaani vitendo na matukio ya aina hiyo katika nchi yetu. Kwa kuwa kwa sasa tukio hili linapelelezwa na Jeshi la Polisi na kama ulivyolieleza Bunge hili, nashauri tuendelee kusubiria upelelezi unaofanywa, tunaamini Jeshi la Polisi kwa umakini na ufanisi watakamilisha upelelezi huo mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naishukuru Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Jimbo la Kibiti na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa michango na kazi nzuri waliyoifanya katika kuboresha Muswada huu baada ya kukutana na wadau waliofika mbele ya Kamati hiyo. Ushauri wa Kamati umetusaidia kuboresha Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ambalo tumeliwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2017*] unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria 11 na kufuta sheria moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha utekelezaji wa sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa kutumia sheria hizo na kuongeza masharti mengine ili kuleta uwiano kati ya sheria zinazorekebishwa na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya, kuongeza vifungu vipya na kufuta sheria moja. Sheria zinazorekebishwa kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, Sura ya 273 [*The Dar es Salaam Water and Sewerage Authority Act, Cap. 273*];

(ii) Sheria ya Elimu, Sura ya 353 [*The Education Act, Cap. 353*];

(iii) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 [*The Law of the Child Act, Cap. 13*];

(iv) Sheria ya Madini, Sura ya 123 [*The Mining Act, Cap. 1233*];

(v) Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili na Rasilimali za Nchi ya Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, of 2017*];

(vi) Sheria ya Petroli, Sura ya 392, [*The Petroleum Act, Cap. 392*];

(vii) Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413 [*The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, Cap. 413*];

(viii) Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 [*The Tanzania Communication Regulatory Authority Act, Cap. 172*];

(ix) Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Tanzania, Sura ya 219 [*The Tanzania Foods, Drugs and Cosmetic Act, Cap.219*];

(x) Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355 [*The Urban Planning Act, Cap. 355*]; na

(xi) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 [*The Value Added Tax Act, Cap. 148*].

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Muswada unapendekeza kufuta Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji, Sura ya 138 [*The Rufiji Basin and Development Authority Act, Cap.138*].

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una Sehemu kuu Kumi na Tatu ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, Sura ya 273, [*The Dar es Salaam Water and Sewerage Authority Act, Cap. 273*]. Kifungu cha sita (6) cha sheria hiyo kinaainisha masharti yanayohusu majukumu ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya DAWASA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya nne (4) ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kifungu hicho kirekebishwe kwa kuongezwa majukumu ambayo hayajaainishwa katika sheria ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu mapya yanayopendekezwa kuongezwa ni pamoja na kutoa huduma ya maji safi na maji taka katika eneo la DAWASA, kufunga, kukagua, kusafisha, kuondoa na kubadilisha mita inayohusiana na usambazaji wa maji safi, kukata maji katika eneo lolote, kuzalisha na kuuza maji kwa ujumla kwa wauzaji wa rejereja, kutoa utaalum kwa vikundi vya jumuiya yaani *community organizations* na kusaidia jamii kuanzisha vikundi vya kijamii kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Marekebisho haya yanalenga kuboresha na kuimarisha utendaji kazi wa DAWASA kwa kuainisha majukumu hayo katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Elimu, Sura ya 353 [*The Education Act, Cap.353*]. Kifungu cha 15 cha sheria hiyo kinaainisha masharti kuwa Kamishna wa Elimu hatatoa kibali cha kuanzisha shule chini ya sheria hiyo hadi mmiliki wa shule awe na kibali cha umiliki wa shule ya aina hiyo kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya elimu au kibali hicho kiwe hakijafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya sita (6) ya Muswada huu inapendekeza kuwa kifungu hicho kifutwe. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha kazi hiyo ya kiutendaji kutekelezwa na Kamishna wa Elimu badala ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16 cha sheria hiyo kinaweka masharti kuhusu kuthibitisha wamiliki wa shule na kuainisha mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya elimu katika mchakato huo, ikiwa ni pamoja na kuelekeza namna ya kufanya maombi, kutoa kibali cha umiliki wa shule na kufuta kibali hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya saba (7) ya Muswada inapendekeza Vifungu vidogo vya (3), (4), (5) na (7) vya Kifungu hicho cha 16 virekebishwe kwa kufuta neno 'Waziri' popote linapoonekana katika vifungu hivyo na badala yake kuweka neno 'Kamishna'. Kama ilivyoelezwa awali, lengo la marekebisho haya ni kuwezesha jukumu hilo la kiutendaji kuhusu utendaji wa utoaji wa vibali kwa wamiliki wa shule kutekelezwa moja kwa moja na Kamishna wa Elimu badala ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii inapendekeza pia marekebisho katika Kifungu cha 60(1) cha Sheria ya Elimu ambacho kinaainisha makosa mbalimbali chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya nane (8) ya Muswada inapendekeza kuwa, Kifungu cha 60(1)(a) kirekebishwe kwa kufuta neno 'Waziri' na kuweka badala yake neno 'Kamishna'. Aidha, Kifungu cha 60(1)(b) kinafutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti kuwa, itakuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kuendesha shule pasipo kupata kibali cha umiliki au umeneja wa shule kinachotolewa na Kamishna wa Elimu. Sheria ilivyo sasa inaweka masharti kuwa, kibali hicho kinatolewa na Waziri mwenye dhamana ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuainisha masharti hayo na masharti yaliyotangulia katika Muswada huu ambapo imependekezwa kuwa masuala ya kiutendaji kuhusu vibali vya umiliki wa shule yatekelezwe na Kamishna wa Elimu badala ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 (*The Law of The Child Act, Cap. 13*). Marekebisho



yanayopendekezwa katika Ibara ya 10 ya Muswada ni kufuta na kuandika upya tafsiri ya maneno, Kituo cha Kulelea Watoto Wachanga (*crèche*) na Kituo cha Kulelea Watoto Mchana (*Day Care Centre*), inayoainishwa katika Kifungu cha tatu (3) cha sheria hiyo. Sheria ilivyo sasa inaeleza pamoja na mambo mengine kuwa vituo hivyo viwili vinasajiliwa kwa ajili ya kupokea na kutunza watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza kuwa, Kituo cha Kulelea Watoto Wachanga (*crèche*) kisajiliwe kupokea na kutunza watoto ambao umri wao ni chini ya miaka miwili na Kituo cha Kulelea Watoto Mchana (*Day Care Centre*) kisajiliwe kupokea na kutunza watoto ambao umri wao haupungui miaka miwili na hauzidi miaka mitano. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha tafsiri inayotofautisha maneno hayo ili kuwezesha sheria hiyo kutekelezeka kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123 (*The Mining Act, Cap 21*). Kifungu cha 21 cha sheria hiyo kama kilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya 2017 kinaanzisha Tume ya Madini ambayo pamoja na mambo mengine ina mamlaka ya kushtaki na kushtakiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tume hiyo ni taasisi ya Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo Mshauri Mkuu wa Serikali na taasisi zake kwa masuala yote ya kisheria na kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 59(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977 yaani Katiba kuwa Mwanasheria Mkuu ana haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika Mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza Kifungu hicho cha 21 kirekebishwe ili kuongeza masharti yatakayompatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali haki ya kuingilia katika shauri lililofunguliwa na au dhidi ya Tume kwa kuiwakilisha Tume hiyo Mahakamani katika shauri husika pale inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Tume imepewa wajibu wa kumfahamisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale inaposhtakiwa au kushtaki Mahakamani. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali katika Tume hiyo kuanzia hatua ya awali ya shauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Maliasili na Rasilimali za Nchi, 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017*). Sheria ilivyo sasa haielezi wazi kama madini na mafuta ni miongoni mwa maliasili na rasilimali zilizoainishwa katika tafsiri ya maneno *natural wealth and resources* iliyoko katika Kifungu cha tatu (3) cha sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, basi, Ibara ya 14 ya Muswada huu, kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza Kifungu hicho kirekebishwe kwa kuongeza madini na mafuta kuwa miongoni mwa maliasili na rasilimali zilizoainishwa katika tafsiri ya maneno hayo *natural wealth and resources*. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha wazi katika sheria kuwa, madini na mafuta ni maliasili na rasilimali inayosimamiwa ipasavyo na masharti ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Petroli, Sura ya 392 (*The Petroleum Act, Cap. 392*). Kifungu cha 47(6) cha sheria hiyo kama kilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya 2017, kinaweka masharti kuwa mkataba wa mafuta chini ya sheria hiyo hautaanza kufanya kazi hadi uridhiwe kwanza na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu hicho kwa namna kilivyoandikwa kinapingana na masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Maliasili na Rasilimali za Nchi ya Mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017*) na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu maliasili za nchi ya mwaka 2017 (*The Natural Wealth and*

*Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*), ambazo zinaainisha kuwa Bunge linaweza kupitia (*review*) mikataba iliyoingiwa na Serikali kuhusiana na maliasili na rasilimali za nchi na siyo kutoa kibali cha kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Ibara ya 16 ya Muswada huu inapendekeza Kifungu hicho kidogo kifutwe. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya sheria hizo kuhusiana na nafasi ya Bunge katika hatua ya mikataba hiyo na hivyo kuliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri ipasavyo Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kuifuta Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji, Sura ya 138 (*The Rufiji Basin Development Authority Act, Cap.138*) kama inavyoonekana katika Ibara ya 17 ya Muswada. Mapendekezo haya yanatokana na ukweli kuwa, majukumu ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji (*RUBADA*) yanatekelezwa na taasisi nyingine. Aidha, mabadiliko ya kiseru yameifanya *RUBADA* kukosa umuhimu wa kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mapendekezo ya kufuta sheria hiyo, Ibara ya 18 ya Muswada inaainisha masharti kuwa, mali na madeni ya *RUBADA* vitahamishiwa kwenye Wizara yenye dhamana na maendeleo na mipango na kwamba Waziri mwenye dhamana ya maendeleo na mipango baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya kilimo atachapisha katika Gazeti la Serikali taarifa kuhusu mali zilizohamishiwa katika Wizara na taasisi nyingine za Serikali. Lengo la mapendekezo haya ni kuainisha namna masuala ya mali na madeni ya *RUBADA* yatakavyoshughulikiwa baada ya kufutwa kwa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatma ya watumishi wa Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza kuwa watumishi

wanaohitajika watahamishiwa katika Wizara, Taasisi au Idara za Serikali kwa mujibu wa sheria zinazosimamia Utumishi wa Umma na kwa masharti na maslahi ambayo si chini ya yale waliyokuwa nayo kabla ya kuhamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mtumishi hatahamishiwa ofisi ya umma atastahili kulipwa mafao yake kwa mujibu wa sheria zinazosimamia masharti ya utumishi wake kabla ya kuachishwa. Mapendekezo haya yanalenga kuainisha hatma na haki ambazo mtumishi wa *RUBADA* atastahili kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya mwisho katika sehemu hii ni kuweka masharti kuwa mikataba, hati, makubaliano yaliyoingwiwa kabla ya kufutwa kwa sheria hiyo yataendelea kutumika na yanaweza kutekelezwa na/au dhidi ya Wizara, Taasisi au Idara husika ya Serikali kama inavyoelezwa katika Ibara ya 20 ya Muswada. Aidha, mwenendo au shauri dhidi ya mali na madeni yaliyohamishwa katika Wizara, Taasisi au Idara za Serikali au mtumishi aliyehamishwa yanaweza kuendelea kutekelezwa na/au dhidi ya Serikali, Taasisi au Idara za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mapendekezo haya ni kuwezesha mikataba, hati, makubaliano na shauri husika kuendelea hadi yatakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhubiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413 (*The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, Cap. 413*). Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 3 cha sheria hiyo kwa kuandika upya tafsiri ya maneno '*Internal Review Committee*' na '*standards*' kwa lengo la kuweka tafsiri itakayoweza maneno hayo kueleweka vyema na hivyo kuboresha utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ibara ya 23 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 16A

ambacho kinaainisha masharti kuwa Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) baada ya kupokea taarifa kuhusu kiwango cha tozo ambacho kimekosewa au baada ya kubaini kosa hilo inaweza kufanya marejeo yaani *review* ya tozo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, inapendekezwa kuwa *SUMATRA* inaweza kusitisha (*suspend*) tozo zilizothibitishwa hadi maombi ya mlalamikaji kuhusu tozo husika yatakapofanyiwa kazi na kutolewa mwongozo. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha *SUMATRA* kushughulikia ipasavyo malalamiko kuhusu makosa katika kukadiria viwango vya tozo zake na hivyo kuhakikisha kuwa tozo stahili ndiyo inayolipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 30 cha sheria hiyo, kinaainisha masharti yanayohusu majukumu na mamlaka ya Baraza (*SUMATRA Consumer Constructive Council*). Ibara ya 24 ya Muswada inapendekeza kifungu hicho kirekebishwe kwa kuongeza utafiti kwenye masuala yanayoathiri maslahi ya watumiaji kuwa miongoni mwa majukumu ya Baraza hilo. Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha Baraza hilo kushughulikia ipasavyo masuala yanayowaathiri watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, mapendekezo ya kuongeza adhabu katika vifungu vya 38(3) na 40(1) vya sheria hiyo ambayo yalikuwa katika Ibara ya 23 na Ibara ya 26 za Muswada yameondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 (*The Tanzania Communication Regulatory Authority Act, Cap. 172*). Ibara ya 28 ya Muswada inapendekeza Kifungu cha tatu (3) cha sheria hiyo kirekebishwe kwa kufuta tafsiri ya maneno 'Mkurugenzi wa Divisheni' (*Divisional Director*) na badala yake kuweka neno 'Mkurugenzi' (*Director*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Kifungu cha 14(1),(2) na (3) ambapo maneno 'Mkurugenzi wa Divisheni' yametumika kinarekebishwa kwa kuweka 'Mkurugenzi' badala ya 'Mkurugenzi wa Divisheni'. Hata hivyo, vifungu hivyo vidogo vimefutwa na kuandikwa upya ili visomeke na kueleweka vizuri zaidi kama inavyoonekana katika Ibara ya 29 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuweka katika sheria cheo cha Mkurugenzi ambacho kinawiana na muundo wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Tanzania, Sura ya 219 (*The Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act, Cap.219*). Ibara ya 31 ya Muswada huu inapendekeza kurekebisha Kifungu cha tatu (3) cha sheria hiyo kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya maneno 'kifaa tiba' (*medical device*).

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuweka tafsiri inayoeleweka vizuri zaidi na hivyo kuiwezesha sheria kutekelezeka ipasavyo kwa kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti uchunguzi wa afya na vifaa vya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine katika sehemu hii ni kurekebisha Kifungu cha 105(1)(a) cha sheria hiyo, ambacho kinaweka masharti kuhusu uteuzi wa wachunguzi chini ya sheria hiyo. Marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 32 ya Muswada ni kuwaongeza 'Wataalam wa Maabara ya Afya' (*Health Laboratory Practitioners*) kuwa miongoni mwa wataalam wanaoweza kuteuliwa kuwa wachunguzi. Marekebisho haya yataimarisha uchunguzi kwa kuwa masuala ya kimaabara yatachunguzwa na wataalam husika katika tasnia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mipango Miji, Sura 355 (*The Urban Planning Act, Cap.355*). Ibara ya 34 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 6A ili kuweka masharti kuhusu uteuzi wa Wapanga Miji (*Town Planners*). Kifungu hicho kipya kinaelekeza kuwa Katibu Mkuu mwenye dhamana ya mipango miji atateua Wapanga Miji ambao watamsaidia Mkurugenzi wa Mipango Miji kutekeleza majukumu yake kwenye Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Muswada unaainisha vigezo vitakavyotumiwa na Katibu Mkuu katika kufanya uteuzi huo kuwa ni pamoja na sifa stahiki, ujuzi na uzoefu katika kupanga miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 34 inapendekeza pia kuongeza Kifungu cha 6B ambacho kitampatia Mkurugenzi wa Mipango Miji mamlaka ya kukasimu majukumu yake kwa Wapanga Miji ili kumsaidia kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hiyo. Kwa ujumla, lengo la marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu hii ni kuboresha utekelezaji wa sheria hiyo na kuimarisha upangaji miji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 (*The Value Added Tax Act, Cap. 148*). Ibara ya 36 ya Muswada huu kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho yafuatayo katika Kifungu cha sita (6) cha sheria hiyo:-

(i) Kifungu kidogo cha 6(2) kinafanyiwa marekebisho ili kubainisha mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kutoa msamaha wa Kodi ya VAT kupitia hati itakayotangazwa katika Gazeti la Serikali kwa miradi ya Serikali itakayogharamiwa na fedha za Serikali na misaada ya wahisani au mikopo nafuu endapo mikataba baina ya Serikali na wafadhili imeweka sharti la utoaji wa msamaha wa Kodi ya VAT kwa mradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inatoza kodi miradi inayogharamiwa na Serikali na Waziri wa Fedha na Mipango hana mamlaka ya kusamehe kodi husika. Aidha, sheria imeweka sharti kwa miradi inayofadhiliwa na wahisani kulipa Kodi ya VAT kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma ndani ya nchi na baadaye kodi husika kurejeshwa baada ya TRA kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisha haya, kwanza, ni kuwezesha miradi inayofadhiliwa na Serikali au wafadhili kutekelezwa kwa wakati kwa kuwa uzoefu umeonesha kuwa utaratibu wa kutoza Kodi ya VAT kwa miradi hiyo unachelewesha kwa kiwango kikubwa ukamilishaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hatua hii itaondoa malalamiko ya wafadhili mbalimbali na hivyo kuweka mazingira bora kwa wahisani hao wa maendeleo kuendelea kutoa misaada yao kwenye miradi mbalimbali kwa ustawi wa nchi.

(ii) Kifungu Kidogo cha 6(3) kinapendekeza kuweka sharti ili msamaha utakaotolewa chini ya kifungu cha 6(2) ufutwe endapo bidhaa au huduma iliyopewa msamaha wa Kodi ya VAT itatumika na mtu mwingine ambaye hakukusudiwa kufaidika na msamaha husika. Aidha, endapo msamaha husika utatumika kinyume na utaratibu, mradi au kampuni iliyopewa msamaha itawajibika kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la pendekezo hili ni kuhakikisha kwamba msamaha utakaotolewa unatumika kwa miradi ya Serikali iliyokusudiwa na hivyo kuzuia ukwepaji kodi kupitia utaratibu huu wa utoaji wa msamaha.

(iii) Kifungu cha 6(4) kinapendekeza kuweka masharti kwamba Hati ya Msamaha wa Kodi itakayotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango ibainishe bidhaa na huduma



zinazosamehewa Kodi ya VAT, tarehe ya kuanza kutumika kwa msamaha husika na muda wa kumalizika kwa msamaha huo.

(iv) Vifungu vya 6(5) na 6(6) vinapendekeza kuweka utaratibu kwa Waziri wa Fedha na Mipango kuunda Kamati ya Wataalam itakayokuwa na jukumu la kutoa ushauri kuhusu maombi ya misamaha, namna ya kusimamia misamaha husika na kuweka utaratibu wa usimamizi wa matumizi ya misamaha itakayotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hiyo, itaundwa na wawakilishi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, TAMISEMI na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, endapo Kamati itahitaji utaalum wa aina fulani wakati wa uchambuzi wa maombi ya misamaha yatakwawasilishwa itaweza kumwalika mtu mwenye utaalum huo katika vikao vyake.

(v) Kifungu cha 6(8) kinapendekeza kuweka tafsiri ya maana ya miradi itakayogharamiwa na Serikali (*Project Funded by the Government*) ambayo itafaidika na misamaha husika ikiwemo miradi ya miundombinu ya maji, usafirishaji, gesi na nishati, majengo, utoaji wa huduma za afya na elimu kwa umma na vituo vya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Muswada unapendekeza pia marekebisho katika Kifungu cha saba (7) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuondoa sharti kwa miradi inayofadhiliwa na wahisani kupitia mikopo nafuu au misaada kulipa kwanza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa/ huduma zinazonunuliwa hapa nchini na kudai marejesho ya kodi hiyo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hii sasa itapewa msamaha wa Kodi ya VAT na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kwa mamlaka aliyonayo chini ya Kifungu cha 6(2),(3),(4),(5),(6) na (7) kinachopendekezwa kupitia Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, Muswada huu unapendekeza kufuta Aya ya tisa (9) ya Sehemu ya Kumi na Moja ya Jedwali la sheria hiyo na kuiandika upya ili misamaha ya Kodi ya VAT kwa miradi ya wahisani iweze kutolewa tu chini ya kifungu cha sita kinachopendekezwa kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya hii kwa sasa imeainisha msamaha wa Kodi ya VAT kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya miradi ya wafadhili ambao mikataba yake na Serikali ina sharti la utoaji wa misamaha ya kodi pamoja na misamaha kwa taasisi za kidiplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kutokana na masharti mapya ya Kifungu cha 6(2), (3), (4), (5), (6) na (7) ambayo yanapendekezwa kupitia Muswada huu, Aya hiyo haina umuhimu wa kuendelea kuwepo kwani iwapo ingebakia ingeleta mgongano na vifungu hivyo vipya na hivyo kusababisha ugumu katika usimamizi wa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo haya kuhusu Muswada huu wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 wa mwaka 2017 na naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Muswada huu katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu ili hatimaye marekebisho husika yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NAMBA 3 WA MWAKA 2017 (THE WRITTEN LAWS MISCELLANEOUS AMENDMENTS) NO. 3, 2017 KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI

ISSN 0856 – 01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*SPECIAL BILL SUPPLEMENT*

*No. 5*

*3rd September, 2017*

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 5 Vol. 98 dated 3<sup>rd</sup> September, 2017*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT (NO.3) 2017

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section*

*Title*

PART I  
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendments of certain written laws.

PART II  
AMENDMENT OF THE DAR ES SALAAM WATER AND  
SEWERAGE AUTHORITY ACT,  
(CAP.273)

3. Construction .
4. Amendment of section 6.

PART III  
AMENDMENT OF THE EDUCATION ACT,  
(CAP.353)

5. Construction.
6. Amendment of section 15.
7. Amendment of section 16.
8. Amendment of section 60.

PART IV  
AMENDMENT OF THE LAW OF THE CHILD ACT,  
(CAP.13)

9. Construction.
10. Amendment of section 3.

PART V  
AMENDMENT OF THE MINING ACT,  
(CAP.123)

11. Construction.
12. Amendment of section 21.

PART VI  
AMENDMENT OF THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES  
(PERMANENT SOVEREIGNTY) ACT,  
(ACT NO. 5 OF 2017)

13. Construction.
14. Amendment of section 3.

PART VII  
AMENDMENT OF THE PETROLEUM ACT,  
(CAP.392)

15. Construction
16. Amendment of section 47

PART VIII  
REPEAL OF THE RUFJI BASIN DEVELOPMENT AUTHORITY ACT,  
(CAP.138)

17. Repeal of Cap.138.
18. Vesting of Assets and liabilities.
19. Employees of the Rufiji Basin Development Authority.
20. Deeds, bonds, agreements and instruments.

PART IX  
AMENDMENT OF THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT  
REGULATORY AUTHORITY ACT,  
(CAP.413)

- 21. Construction.
- 22. Amendment of section 3.
- 23. Amendment of section 16A.
- 24. Amendment of section 30.
- 25. Amendment of section 38.
- 26. Amendment of section 40.

PART X  
AMENDMENT OF THE TANZANIA COMMUNICATION REGULATORY  
AUTHORITY ACT,  
(CAP.172)

- 27. Construction.
- 28. Amendment of section 3.
- 29. Amendment of section 14.

PART XI  
AMENDMENT OF THE TANZANIA FOOD, DRUGS AND COSMETICS ACT,  
(CAP.219)

- 30. Construction.
- 31. Amendment of section 3.
- 32. Amendment of section 105.

PART XII  
AMENDMENT OF THE URBAN PLANNING ACT,  
(CAP.355)

- 33. Construction.
- 34. Amendment of section 6A.

PART XIII  
AMENDMENT OF THE VALUE ADDED TAX ACT,  
(CAP.148)

- 35. Construction.
- 36. Amendment of section 6.



- (p) to facilitate the community to form community organizations in collaboration with local government authorities;" and
- (b) re-naming paragraphs (k) and (l) as paragraphs (q) and (r) respectively.

PART III  
AMENDMENT OF EDUCATION ACT,  
(CAP.353)

- Construction  
Cap.353
5. This Part shall be read as one with the Education Act, hereinafter referred to as the "principal Act".
- Amendment of  
section 15
6. The principal Act is amended in section 15(1), by-
- (a) deleting paragraph (a); and
  - (b) renaming paragraphs (b) to (f) as paragraphs (a) to (e) respectively.
- Amendment of  
section 16
7. The principal Act is amended in section 16, by deleting the designation "Minister" wherever it appears in subsections (2), (3), (4), (5) and (7) and substituting for it the designation "Commissioner".
- Amendment of  
section 60
8. The principal Act is amended in section 60(1), by-
- (a) deleting the designation "Minister" appearing in paragraph (a) and substituting for it the designation "Commissioner".
  - (b) deleting paragraph (b) and substituting for it the following:
    - "(b) manage any school without having been approved as owner or manager or in either case continues to manage the school after the withdrawal of his approval."

PART IV  
AMENDMENT OF THE LAW OF THE CHILD ACT,  
(CAP. 13)

- Construction  
Cap. 13
9. This Part shall be read as one with the Law of the Child Act, hereinafter referred to as the "principal Act".
- Amendment of  
sections 3
10. The principal Act is amended in section 3, by deleting the definitions of the terms "crèche" and "day-care centre" and substituting for them the following:
- "crèche" means an early childhood development establishment registered for purpose of providing child care for children below the age of two years for the day or a substantial part of the day, with or without fees;
  - "day care centre" means an early childhood development establishment registered for the purpose of receiving and providing child care for children of the age of not less than two years but not exceeding the age of five years for the day or a substantial part of the day with or without fees;"

PART V  
AMENDMENT OF THE MINING ACT,  
(CAP. 123)

Construction  
Cap. 123                    **11.** This Part shall be read as one with the Mining Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of  
section 21                    **12.** Section 21 of the principal Act is amended-

(a) by inserting immediately after subsection (2) the following new subsection:

"(3) Notwithstanding preceding provisions of this section, the Attorney General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by or against the Commission.

(4) Where the Attorney General intervenes in any matter pursuant to subsection (3), the provisions of the Government Proceedings Act, shall apply in relation to the proceedings of that suit or matter as if it has been instituted against the Government.

(5) The Commission shall have the duty to notify the Attorney General of any impending suit or intention to institute a suit or matter for or against the Commission."

(b) by renumbering subsections (3) to (7) as subsections (5) to (10) respectively.

PART VI  
AMENDMENT OF THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES  
(PERMANENT SOVEREIGNTY) ACT,  
(ACT NO. 5 OF 2017)

Construction  
Act No. 5 of 2017                    **13.** This Part shall be read as one with the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, herein after referred to as the "principal Act".

Amendment of  
section 3                    **14.** Section 3 of the principal Act is amended in the definition of the term "natural wealth and resources" by inserting immediately after the words "water resources" appearing in the third line the words "mineral resources and petroleum resources".

PART VII  
AMENDMENT OF THE PETROLEUM ACT,  
(CAP. 392)

Construction  
Cap. 392                    **15.** This Part shall be read as one with the Petroleum Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of  
section 47                    **16.** The principal Act is amended in section 47, by deleting subsection (6).



PART VIII  
REPEAL OF THE RUFJI BASIN DEVELOPMENT AUTHORITY ACT,  
(CAP.138)

Repeal of  
Cap.138

**17.** The Rufiji Basin Development Authority Act, is hereby repealed.

Vesting of Assets  
and liabilities

**18.**-(1) Consequent upon the repeal of the Rufiji Basin Development Authority Act, all assets, interests, rights, privileges, liabilities or obligations vested in Rufiji Basin Development Authority shall be vested in the Ministry responsible for development and planning.

(2) The Minister responsible for development and planning in consultation with the Minister responsible for Agriculture may, by notice published in the Gazette, determine the assets and liabilities to be allocated to the Ministry and to other government institutions or departments.

(3) Where any question arises as to whether any particular property, or any particular asset, interest, right, privilege, liability or obligation has been transferred to or vested in accordance with provisions of subsection (1), a certificate under the hand of the Minister responsible for development and planning shall be conclusive evidence that the property, asset, interest, right, privilege, liability or obligation was or was not so transferred or vested.

Employees of  
the Rufiji Basin  
Development  
Authority

**19.**-(1) Employees or staff of the Rufiji Basin Development Authority who are necessary for the purposes of the Ministry or government institutions or departments shall, subject to laws and procedures governing public service be transferred to public offices on such terms and conditions not less favorable than those applicable to them before the transfer.

(2) Every employee or staff of the Rufiji Basin Development Authority whose service is not transferred to public office shall be paid terminal benefits in accordance with the applicable laws and regulations governing the terms and conditions of his service immediately before the termination.

(3) An employee or staff who is deemed to be employed or transferred to public office shall continue to be a member of a statutory, voluntary pension or any other superannuation scheme in accordance with the laws and regulations governing the scheme.

Deeds, bonds,  
agreements and  
instruments  
Cap. 138

**20.**-(1) All deeds, bonds, agreements, instruments and working arrangement subsisting immediately before the repeal of the Rufiji Basin Development Authority Act, transferred to the Ministry or to government institutions or departments shall continue in full force and shall be enforceable by or against the Ministry or government institutions or departments.

(2) Any proceeding or cause of action relating to the property, rights and liabilities transferred to the Ministry or to government institution or departments under this Part or to any employee transferred, may be continued and shall be enforced by or against the Ministry, government institutions or departments.

PART IX  
AMENDMENT OF THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY ACT, (CAP. 413)

- Construction  
Cap. 413
- 21.** This Part shall be read as one with the Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, hereinafter referred to as the "principal Act".
- Amendment of  
Section 3
- 22.** The principal Act is amended in section 3, by deleting the definitions of the terms "Special Review Committee" and "standards" and substituting for them the following new definitions-
- " "Internal Review Committee" means the Committee appointed by the Authority pursuant to section 26; and
- "standards" includes the standard relating to safety and service delivery established by the Authority."
- Addition of new  
section 16A
- 23.** The principal Act is amended by adding immediately after section 16 the following new section:
- "Power to review or suspend rates or charges
- 16A.**-(1) The Authority may, upon receiving information on an error in the rates of charges or on its own motion recognizing an error in the rates or charges review such rates or charges.
- (2) The Authority may suspend approved rates or charges pending determination of an application of an aggrieved party on such rates or charges.
- s
- Amendment of  
section 30
- 24.** The principal Act is amended in section 30(1), by adding immediately after paragraph (e) the following new paragraph:
- "(f) to conduct research on matters affecting interests of consumers of a regulated subsector;"
- Amendment of  
section 38
- 25.** The principal Act is amended in section 38, by deleting subsection (3) and substituting for it the following:
- "(3) A person who contravenes or fails to comply with rules made under this section, commits an offence and is liable on conviction to a fine of not less than three million shillings but not exceeding fifty million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding three years or to both."
- Amendment of  
section 40
- 26.** The principal Act is amended in section 40, by deleting subsection (1) and substituting for it the following:
- "(1) A person who contravenes or fails to comply with a provision of this Act, commits an offence and shall, upon conviction, be liable to a fine of not less than ten million shillings, but not exceeding fifty million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding three years or to both."

PART X  
AMENDMENT OF THE TANZANIA COMMUNICATION  
REGULATORY AUTHORITY ACT,  
(CAP. 172)

Construction  
Cap. 172

**27.** This Part shall be read as one with the Tanzania Communication Regulatory Authority Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of  
sections 3

**28.** The principal Act is amended in section 3, by deleting the definition of the term “Divisional Director” and substituting for it the following:  
“Director” means a Director appointed under section 14;”

Amendment of  
sections 14

**29.** The principal Act is amended in section 14, by deleting subsections (1), (2) and (3) and substituting for them the following:  
“(1) There shall be employed by the Authority, such number of Directors with respective responsibilities as may be assigned by the Authority.  
(2) A director appointed under subsection (1), shall be a person who has proven knowledge and appropriate experience in matters related to electronic communication sector.  
(3) A Director shall hold office for a term of five years and may, subject to satisfactory performance, be eligible for re-appointment for another term as the Authority deems necessary”.

PART XI  
AMENDMENT OF THE TANZANIA FOOD, DRUGS AND COSMETICS ACT,  
(CAP. 219)

Construction  
Cap. 219

**30.** This Part shall be read as one with the Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of  
section 3

**31.** The principal Act is amended in section 3, by deleting the definition of the term “medical device” and substituting for it the following:  
“medical device” means any instrument, apparatus, laboratory equipment and reagent, implement, machine, appliance, implant, in vitro reagent or calibrator, software, material or other similar or related article which is intended by manufacturer to be used alone or in combination for human beings or other animals, for the following purpose of-

- (a) diagnosis, prevention, monitoring treatment or alleviation of diseases or compensation for an injury;
- (b) investigation, replacement, modification, support, the anatomy or of a physiological process;
- (c) supporting or sustaining life;
- (d) control of conception; or
- (e) providing information for medical or diagnostic

purposes by means of vitro examination or specimen derived from the human body or other animal, except that it does not achieve its primary intended action in or on the human body by pharmacological, immunological or metabolic means.

Amendment of section 105

**32.** The principal Act is amended in section 105(1)(a), by adding immediately after the word "practitioner," the words "health laboratory practitioners".

PART XII  
AMENDMENT OF THE URBAN PLANNING ACT,  
(CAP.355)

Construction Cap. 355

**33.** This Part shall be read as one with the Urban Planning Act, hereinafter referred to as the "the principal Act".

Addition of section 6A

**34.** The principal Act is amended by adding immediately after section 6 the following new sections:

"Appointment of Town Planners

**6A.**(1) There shall be appointed by the Permanent Secretary of the Ministry such number of Town Planners, who shall assist the Director in the performance of his duties and exercise powers vested upon him by this Act at Zonal or other appropriate levels as may be required.

(2) The Permanent Secretary shall in appointing a Town Planner under this section, ensure that the appointed person is a person of proven probity with qualification, skills and practical experience in urban planning.

Delegation of powers by Director

**6B.** The Director may, in performing his functions under this Act, delegate some of his functions to the Town Planner and such delegation shall be published in the *Gazette*."

PART XIII  
AMENDMENT OF THE VALUE ADDED TAX ACT,  
(CAP.148)

Construction Cap.149

**35.** This Part shall be read as one with the Value Added Tax Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 6

**36.** The principal Act is amended in section 6, by deleting subsection (2) and substituting for them the following new subsections-

"(2) Notwithstanding the provisions of subsection (1), the Minister may, by order in the *Gazette*, grant value added tax exemption on importation by the Government entity or supply to the Government entity of goods or services to be used solely for-

- (a) implementation by a Government entity of a project funded by donor funds or concessional loan through an agreement between the Government of the United Republic of Tanzania and another government, donor or lender:

Provided that, such agreement provides for value added tax exemption on such goods or services; or

- (b) relief of natural calamity or disaster.

(3) The Minister may, for the purpose of this section,-

- (a) appoint a technical Committee which shall advise the Minister on the granting and monitoring of exemption; and
- (b) prescribe procedures for purposes of monitoring utilization of exemption granted under this section.

(4) The exemption granted in this section shall cease to have effect and the value added tax shall become due and payable as if the exemption had not been granted if the said goods or services are transferred, sold or otherwise disposed off in any way to another person not entitled to enjoy similar privileges as conferred under this Act.

(5) The order issued by the Minister under subsection (2), shall specify goods or services that are eligible for exemption, commencement and expiry date of the exemption."

---

## OBJECTS AND REASONS

---

This Bill proposes to amend twelve written laws, namely the Dar es Salaam Water Sewerage Authority Act, (Cap.273), the Education Act, (Cap.353), the Law of the Child Act, (Cap.13), the Mining Act, (Cap.123), the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (No. 5 of 2017), the Petroleum Act, (Cap.392), the Rufiji Basin Development Authority Act, (Cap.138), the Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, (Cap.413), the Tanzania Communication Regulatory Authority Act, (Cap.172) and the Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act, (Cap.219), the Urban Planning Act, (Cap.355) and the Value Added Tax Act, (Cap.148).

This Bill is divided into Thirteen Parts.

Part I deals with Preliminary Provisions which includes the title of the Bill and the manner in which the proposed amended laws are amended in their respective Parts.

Part II of the Bill proposes to amend the Dar es Salaam Water and Sewerage Authority Act, Cap. 273 it is proposed to amend section 6 by adding add the functions of DAWASA in order to address the challenges that have emerged in the implementation of its activities.

Part III proposes the amendment of the Education Act, (Cap. 353). Section 15 is amended by deleting paragraph (a) so as to allow the operational functions of approval of schools to be done by the Commissioner instead of the Minister. Section 16 is also amended in subsections (3), (4), (5) and (7) by providing powers to the Commissioner for Education to make or withdraw an approval of any school which is not in compliance with the conditions specified under the Act. Section 60(1) is equally amended by imposing penalties to any person who operates a school in contravention with the provisions of the Act.

Part IV of the Bill proposes amendment to the Law of the Child Act, (Cap.13). This Part amends section 3 by deleting the definitions of the terms "crèche" and "day-care centre" and replacing them with new definitions respectively. The aim of introducing the new definition is to remove existing ambiguities regarding the meaning of the two terminologies as used in the Act.

Part V of the Bill proposes amendment of the Mining Act, (Cap.123). Section 21 of the Act is amended so as to enable the Attorney General to intervene in any suit or matter instituted for or against the Commission. In the same spirit, the duty to notify the Attorney General on the intention to institute a suit or matter is imposed on the Commission. These proposals intend to protect the interest of the Government in such proceedings or matters.

Part VI of the Bill proposes amendment to the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (No. 5 of 2017). Section 3 of the Act is amended in the definition of the term “natural wealth and resources” with a view to adding the terms “mineral resources” and “petroleum resources” which are missing in the definition.

Part VII of the Bill proposes amendment to the Petroleum Act, (Cap. 392). Section 47 is amended by deleting subsection (6).

Part VIII of the Bill proposes to repeal the Rufiji Basin Development Authority Act, (Cap.138). The existing legal reforms have undermined the importance of RUBADA as its functions can now be performed by other Government institutions. In order to reduce the burden to the Government, it is important for the RUBADA to be abolished. Hence this Part proposes to repeal the Rufiji Basin Authority Act. It also deals with the transfer of assets and liabilities of RUBADA to other government entities.

Part IX of the Bill proposes amendment to the Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, (Cap. 413). Section 3 is amended by deleting and replacing certain definitions as used in the Act. Section 16A is proposed to enable the Authority to review any tariffs and charges imposed under this Act. Section 30 is amended so as to introduce a new function of the Authority relating to researching on matters affecting interest of consumers. Sections 38 and 40 propose enhancement penalties for contravention of the provisions of the Act.

Part X proposes to amend the Tanzania Communication Regulatory Authority Act, (Cap.172). Section 3 is amended by deleting the definition of the term “Division Director” and substituting for it the term “Director” which corresponds with the institution’s organization structure. Section 14 is also amended in subsections (1), (2) and (3) in order to provide qualification and tenure of office of the Director. Under this proposal, the Director shall hold office for a term of five years renewable for one more term.

Part XI proposes amendment to the Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act, (Cap.219). Section 3 is amended by replacing the definition of the term “medical device” with a view to accommodating other laboratory equipment and reagent which are not covered in the existing definition. Amendment of this section intends to put in place mechanisms for control of diagnostics and medical devices. Section 105(1) (a) is amended by integrating health laboratory practitioners as persons eligible for appointment or authorization under that section.

Part XII provides amendment to the Urban Planning Act, (Cap. 355). It is proposed to introduce a new section 6A for purposes of empowering the Director of

Urban Planning to delegate some of his power and functions to the town planners in order to assist him in the performance of his duties under the Act.

Part XIII of the Bill proposes to amend the Value Added Tax Act, (Cap.148) in section 6. These amendments intend to enable the Minister responsible for finance to grant exemption in respect of projects funded by donor funds or concessional loans whose agreement provide for such value added tax exemption.



---

## MADHUMUNI NA SABABU

---

Muswada huu unakusudia kurekebisha sheria kumi na mbili zikijumuisha Sheria ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, (Sura ya 273), Sheria ya Elimu, (Sura ya 353), Sheria ya Mtoto, (Sura ya 13), Sheria ya Madini, (Sura 123), Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, (Sura ya 435), Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Rasilimali za Nchi, (Na. 5 ya Mwaka 2017), Sheria ya Petroli, (Sura ya 392), Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bodi la Mto Rufiji (Sura ya 138), Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, (Sura ya 413), Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, (Sura ya 172), Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi, (Sura ya 219), Sheria ya Mipango Miji (Sura ya 355) na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, (Sura ya 148).

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Tatu.

Sehemu ya Kwanza inaweka masharti ya awali ikijumuisha jina la Muswada na masuala ya utangulizi.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, (Sura ya 273) kwa kukifanyia marekebisho kifungu cha 6 kwa lengo la kuongeza majukumu ya DAWASA ili kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utendaji wake.

Sehemu ya Tatu inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Elimu, (Sura ya 353). Kifungu cha 15 kinarekebisha kwa kuondoa aya ya (a) ili kuruhusu kazi za kiutendaji za kuthibitisha shule ziweze kutekelezwa na Kamishna badala ya Waziri. Kifungu cha 16 kimerekebisha kwenye vifungu vidogo vya (3), (4), (5) na (7) ili kumpa mamlaka Kamishna wa Elimu kutoa kibali cha kuendesha shule. Kifungu cha 60(1) kimerekebisha kwa kuweka adhabu kwa mtu yoyote ambaye atakayeendesha shule bila kuzingatia masharti ya sheria hii.

Sehemu ya Nne inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mtoto, (Sura ya 13). Sehemu hii inarekebisha kifungu cha 3 kwa kuandika upya tafsiri ya maneno “kituo cha kulelea watoto wachanga” na “kituo cha kulelea watoto mchana”. Dhumuni la kuandika upya tafsiri ya maneno haya ni kuondoa utata baina ya tafsiri hizo na kuweta ufafanuzi zaidi.

Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Madini, (Sura ya 123). Kifungu cha 21 cha Sheria hiyo kinarekebisha ili kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati mashtaka au madai dhidi ya Tume. Kwa msingi huo, Tume imepewa wajibu wa kumtaarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu kusudio la kufungua mashtaka au madai. Lengo la marekebisho haya ni kulinda maslahi ya Serikali.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Rasilimali za Nchi (Na. 5 ya Mwaka 2017). Kifungu cha 3 cha Sheria hii kinafanyiwa marekebisho katika tafsiri ya msamiati “natural wealth and resources” ili kujumuisha rasilimali za Madini na Mafuta ambazo zinakosekana katika msamiati huo.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Petroli, (Sura ya 392). Kifungu cha 47 cha Sheria hiyo kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu kidogo cha (6).

Sehemu Nane ya Muswada inapendekeza kuifuta Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa **Bonde** la Mto Rufiji (Sura ya 138). Hivyo mapendekezo haya yanatokana na majukumu ya Kisheria ya RUBADA kutelekezwa na Taasisi nyingine. Aidha, mabadiliko ya kisera yameifanya RUBADA kukosa umuhimu wa kuendelea kuwepo. Vile vile, sehemu hii inatamkwa bayana kufutwa kwa Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji. Aidha, inaainisha kuhusu uhamishaji wa mali na madeni ya RUBADA na masuala ya ajira za Watumisni ambapo inapendekezwa kuwa wahamishiwe kwenye Mamlaka nyingine za Umma.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhubiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, (Sura ya 413) kifungu cha 3 kimerekebishwa kwa kufuta baadhi ya tafsiri na kuongeza tafsiri nyingine ili kufafanua maneno yaliyotumika katika Sheria. Vile vile sehemu hii inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 16A ili kuwezesha Mamlaka kurejea tozo na ada zilizotozwa chini ya sheria hii. Kifungu cha 30 kinarekebishwa ili kuongeza jukumu jipya la Mamlaka la kufanya utafiti kwenye masuala yanayohusu maslahi ya walaji. Kifungu cha 38 na 40 vinafanyiwa marekebisho ili kuhuisha adhabu zinazotolewa kwa makosa chini ya Sheria hii.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, (Sura ya 172). Kifungu cha 3 kimerekebishwa kwa kufuta tafsiri ya neno "Mkurugenzi wa Divisheni" na badala yake kuwa "Mkurugenzi" cheo ambacho kinawiana na Muundo wa Taasisi. Aidha, kifungu cha 14 kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1), (2) na cha (3) kwa lengo la kuweka sifa za Mkurugenzi na muhula wa Mkurugenzi. Kwa mujibu wa mapendekezo haya, Muhula wa Mkurugenzi utakuwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuendelea tena kwa kipindi kingine kama hicho.

Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Madawa na Vipodozi, (Sura ya 219). Kifungu cha 3 kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya maneno "kifaa tiba". Marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu hiki yanalenga kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti uchunguzi wa afya na vifaa vya uchunguzi. Sehemu hii inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 105(1)(a) kwa lengo la kuwawezesha watendaji wa maabara (health laboratory practitioners) kufanya kazi kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

Sehemu ya Kumi na Mbili inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mipango Miji, (Sura, 355). Kifungu kipya cha 6A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kumruhusu Mkurugenzi wa Mipango Miji kukasimu mamlaka yake na majukumu yake kwa wapanga mji ili waweze kumsaidia katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria husika.

Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, (Sura ya 148). Kifungu cha 6 cha Sheria hiyo kinafanyiwa marekebisho kwa lengo la kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha, kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye miradi inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo au mikopo yenye masharti nafuu ambayo mikataba husika ina masharti ya kutoa misamaha hiyo.

Dodoma,  
.....Agosti, 2017

**PALAMAGAMBA J.A.M KABUDI**  
*Waziri wa Katiba na Sheria*

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI, MINISTER FOR CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, (NO.3), 2017"

(Made under S.O. 84(3))

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act (No.3), 2017 is amended as follows:

- A:** In Clause 4, by-
- (a) deleting the word "operate" appearing in proposed paragraph (k) and substituting for it the word "provide";
  - (b) deleting the word "supply" appearing at the end of the proposed paragraph (l) and substituting for it the words "water and sewerage services"; and
  - (c) deleting the proposed paragraph (m) and substituting for it the following:  
" (m) disconnect the supply of water or sewerage services from any premises or to diminish, withhold or divert the services through or by means of any pipe or fitting wholly or in part;".
- B:** In Clause 10, by deleting the word "not exceeding" appearing in the definition of the term "day care centre" and substituting for it the word "below".
- C:** In Clause 14, by deleting the whole of that Clause and substituting for it the following:  
"Amendment of section 3                      **14.** Section 3 of the principal Act is amended in the definition of the term "natural wealth and resources" by deleting the words "and fauna, flora" and substituting for them the words "mineral resources, petroleum resources, flora and fauna,".
- D:** By deleting Clauses 25 and 26.
- E:** By deleting Clause 36 and substituting for it the following:  
"Amendment of section 6                      **36.** The principal Act is amended in section 6, by deleting subsection (2) and substituting for it the following new subsections:
- "(2) Notwithstanding the provision of subsection (1), the Minister may, by order published in the *Gazette*, grant value added tax exemption on imports by a Government entity or supply to a Government entity of goods or services to be used solely for-
- (a) implementation of a project funded by-
    - (i) the Government; or
    - (ii) concessional loan or grant through an agreement between the Government of the United

Republic of Tanzania and another government, donor or lender of a concessional loan:

Provided that, such agreement provides for value added tax exemption on such goods or services; or

(b) relief of natural calamity or disaster.

(3) The exemption granted under this section shall cease to have effect and the value added tax shall become due and payable as if the exemption had not been granted if the said goods or services are transferred, sold or otherwise disposed of in any way to another person not entitled to enjoy similar privileges as conferred under this Act.

(4) The order issued by the Minister under subsection (2), shall specify goods or services that are eligible for exemption, commencement and expiry date of the exemption.

(5) The Minister may, for the purpose of this section and upon such terms and conditions as may be required-

(a) appoint a technical Committee which shall advise the Minister on the granting and monitoring of exemption; and

(b) prescribe procedures for purposes of monitoring utilization of exemption granted under this section.

(6) The Committee appointed under subsection (5), shall comprise of representatives from the following institutions:

(a) the Ministry responsible for finance and planning;

(b) the Attorney General's Office;

(c) the Ministry responsible for Local Government; and

(d) the Tanzania Revenue Authority.

(7) The Committee may co-opt any person with special knowledge or skills to provide expertise on a particular matter as may be required by the Committee.

(8) In this section, "project funded by Government" means a project financed by the Government in respect of-

- (a) transport, water, gas or power infrastructure;
- (b) buildings for provision of health or education services to the public; or
- (c) a centre for persons with disabilities."

Dodoma,  
.... September, 2017

**PJAMK**  
*MoCLA*



**NAIBU SPIKA:** Tutaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenijalia mimi afya njema, kukujalia wewe pamoja na Wabunge wote wa Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 wa Mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments*) No. 3, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ninao muda wa kutosha na taarifa yangu mimi ni fupi; ninazo shukrani zangu tatu naomba uniruhusu niweze kuzitoa. Kwa heshima kubwa kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kuniteua mimi Mohamed Omary Mchengerwa kuwa Mjumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi na Ushauri iliyokuwa ikichunguza na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu madini ya *tanzanite* lakini pia nimshukuru sana kwa kumteua Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo kuwa Mjumbe wa Kamati Maalum ya Mheshimiwa Spika kuhusu uchunguzi na ushauri wa madini ya almasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi huu unaonyesha imani kubwa aliyonayo kwetu na kwa Kamati yote ya Katiba na Sheria katika kusimamia maslahi ya nchi hii na wananchi waliotutuma katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuridhia Kamati yangu ya Katiba na Sheria kupitia sheria hizi 12, ambazo kwa namna ya kipekee nimshukuru yeye kwa kusikia kilio cha wanyonge hususan wapiga kura wangu wa Jimbo la Rufiji kwa kuridhia kuifuta

*RUBADA*; ikiwa ni miongoni mwa baadhi ya sheria ambazo siku ya leo zinafutwa na nyingine kufanyiwa marekebisho kutokana na upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ukombozi mkubwa kwa wananchi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa ili twende sawasawa, haya maelezo unayoyasoma yapo kwenye taarifa yako tuliyonayo wengine ama hayapo.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni *preamble*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, kwa kanuni zetu unasoma kile ulicholeta ndiyo maana unaambiwa unasoma; kwa hiyo, tusomee hicho ambacho umetuletea tafadhali.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu tarehe 5 Septemba, 2017 baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Nane wa Bunge hili ili ufanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 8 Septemba, 2017, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Joyce Ndalichako kwa niaba ya mtoa hoja ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mawaziri wengine wanaoguswa na maeneo mbalimbali ya Muswada huu walifika mbele ya Kamati iliyoketi Dodoma na kutoa maelezo kuhusu malengo na madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho mbalimbali katika sheria husika kwa madhumuni ya kuondoa upungufu ama kasoro zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na timu ya Mawaziri na Manaibu Waziri kufika mbele ya kamati yangu, kulikuwa na watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya taasisi mbalimbali



za Serikali zinazoguswa na mabadiliko yanayopendekezwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ni matokeo yalifikiwa kati ya Kamati ya Katiba na Sheria na Serikali kuhusu maeneo mbalimbali yanayofanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya Maji Safi na Maji taka Dar es Salaam Sura Na. 273
- (ii) Sheria ya Elimu Sura ya 353
- (iii) Sheria ya Mtoto Sura ya 13
- (iv) Sheria ya Madini Sura ya 123
- (v) Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Sura ya 435
- (vi) Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Rasilimali za Nchi Na. 5, Mwaka 2017
- (vii) Sheria ya Petroli, Sura ya 392
- (viii) Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji Sura 138
- (ix) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413
- (x) Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172
- (xi) Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura ya 219
- (xii) Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355
- (xiii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 na kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya nane (8) na Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayowapa wananchi nafasi ya kushiriki katika masuala mbalimbali yanayowahusu, Kamati iliwaalika wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwa kutumia nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu. Naomba kutambua mchango wao kama ifuatavyo: -

Chama cha Mawakili Tanganyika, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (*TABOA*), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania pamoja na Chama cha Mawakala wa Forodha Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo na Madhumuni ya Muswada. Maelezo ya jumla ya Muswada huu yapo katika taarifa ya mtoa hoja, Waziri wa Katiba na Sheria ambayo tayari imesomwa hapa mbele yako na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pamoja na maelezo, malengo na madhumuni ya Muswada yaliyomo kwenye Muswada kuanzia ukurasa wa 14 mpaka 17 na kwa faida ya muda naomba nisirudie tena maelezo haya na sehemu hii naomba yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huu, naomba sasa nijielekeze katika uchambuzi wa jumla wa Muswada huu. Kamati kwa umakini mkubwa ilipitia vifungu vyote 36 ya Muswada huu na kujiridhisha na dhima na muundo wa muswada. Kamati ilijiridhisha kwamba vifungu vingi vya Muswada ni vifungu vya kimuundo na havikuwa na madhara katika maudhui ya Muswada (*construction provision*). Kwa mfano, katika kifungu cha 36 cha Muswada, vifungu karibu 25 havikuwa na tatizo lolote katika maudhui ya Muswada pamoja na kifungu cha 1, 2, 3, 5, 6, 7, 8 na vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya marekebisho katika Muswada huu ni ya kawaida na hayakuleta mjadala wowote kati ya Kamati na Serikali. Kwa mfano marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Dar es Salaam, Sheria ya Elimu, Sheria ya Mtoto, Sheria ya Madini, Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Rasilimali za Nchi Na. 5 ya Mwaka 2017, Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Dawa, Vipodozi na Sheria ya Mipango Miji. Kamati ilikubaliana na

mapendekezo ya Serikali kuhusu marekebisho ya sheria hizi kwa sababu zilizotajwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijielekeza katika Sheria ya Petroli, ufutwaji wa Sheria ya *RUBADA*, Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Nchi Kavu na Majini na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Katika sheria hizi, yapo maeneo ambayo Kamati ilitaka maelezo ya ziada kuhusu marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa maelezo ya ziada kuhusu maeneo yaliyorekebisha katika sheria hizi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji katika kifungu cha 16 cha Muswada kinachobadilisha kifungu cha 47(6) cha Sheria ya Petroli. Kamati imekubaliana na Serikali kwamba mabadiliko haya yanakusudia kutoa nafasi kwa Bunge kuisimamia vizuri Serikali na hasa kwa kuzingatia utekelezaji wa mikataba mbalimbali ambayo Serikali imekuwa inaingia na wawekezaji mbalimbali katika sekta ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge litapitisha mikataba ya namna hii, hakutakuwa tena na dhana ya *checks and balance* kati ya mihimili hii ya dola hivyo kulifanya Bunge kuwa sehemu ya makosa au matatizo yoyote yanayotokana na mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufutwaji wa Sheria ya *RUBADA*, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utaratibu wa kisheria uliowekwa kuhusu mali na madeni ya mamlaka pamoja na maslahi ya wafanyakazi wa mamlaka na hasa kipindi cha mpito (*transition period*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho yaliyokusudiwa katika Sheria ya *SUMATRA* hasa kifungu cha 23, 25 pamoja na kifungu cha 26 vya Muswada huu, Kamati ilihitaji maelezo ya ziada kutoka *SUMATRA* kuhusu uhalali wa tozo (*fine*) katika marekebisho hayo ambayo inapanda kutoka shilingi laki tano mpaka *fine* isiyopungua shilingi milioni tatu na isiyozidi shilingi milioni 50 kwa makosa yaliyotajwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Kamati ilitaka kufahamu mamlaka aliyonayo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye miradi inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo au mikopo yenye masharti nafuu ambayo mikataba husika ina masharti ya kutoa misamaha hiyo. Katika sheria hii, Kamati ilitaka kujiridhisha na namna Waziri husika atakavyounda Kamati ya Wataalam (*Technical Committee*) ambayo itamshauri Waziri kuhusu utoaji na ufuatiliaji wa misamaha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano ya kina kati ya Serikali na Kamati, Serikali ilikubali kuyafanyia kazi marekebisho na mapendekezo ya Kamati na kuyajumuisha katika jedwali la marekebisho kama ilivyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na hasa katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na Sheria ya *SUMATRA*. Kwa msingi huu naomba sasa nijielekeze katika maoni na ushauri wa Kamati kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kutokana na uchambuzi huo, kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufutwaji wa Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji (*RUBADA*). Kwa kuwa Serikali ya awamu ya Tano inachukua hatua za kutosha katika kuboresha taasisi za umma kama ambavyo ilifuta Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma mwezi wa Tano mwaka huu, Kamati inaishauri kwamba madeni yanayoachwa na taasisi inayovunjwa yasihamishiwe katika taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri iundwe Ofisi ya Taifa ya Madeni (*National Debts Management Office*) ambayo itakuwa na jukumu la kurithi na kusimamia madeni yote ya Taifa. Utaratibu huu utumike hata katika kusudio la kuvunja mashirika mengine kama Shirika la Umma la *RAHCO*. Utaratibu huu umetumika pia katika nchi nyingine za jirani kwa mfano Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maslahi ya Wafanyakazi Yazingatiwe. Kamati inashauri kwamba maslahi yote yanayohusiana na ajira za wafanyakazi wote wa Mamlaka ya RUBADA yazingatiwe na hasa katika kipindi hiki cha mpito na kwamba kila atakayeachishwa kazi alipwe sawasawa na mkataba wake wa kazi na taratibu, Sheria za Ajira na Utumishi wa Umma;.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili pia tunapenda kuishauri Serikali yale mashamba na viwanja vya wananchi wa Rufiji pia virejeshwe kwa wananchi wa Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*). Kamati inaishauri Serikali kuandika tena kifungu cha 25 pamoja na kifungu cha 26 vya Muswada ili viseme kwa uwazi (*expressly*) kwamba vimekusudia kutoa adhabu iliyotajwa katika vifungu hivyo kwa makosa yatakayotendeka katika vyombo vya usafiri baharini ambavyo vipo chini ya *Mercantile Shipping Act* ya mwaka 2003 na sio kwa makosa yanayotendeka katika usafiri wa nchi kavu ambayo yapo chini ya Sheria ya *Transport Licensing Act* ya mwaka 1973.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Kamati imewahi kushauri siku za nyuma na hasa katika taarifa yake kuhusu uridhaji wa mikataba ya kazi ya Mabaharia Tanzania, ni muda muafaka sasa wa kuboresha sekta ya usafiri majini kwa kuwa na taasisi moja ya upande wa Tanzania Bara itakayosimamia sekta ya usafiri wa majini kama ilivyo Zanzibar ambayo kuna Mamlaka ya Usafiri Majini (*Zanzibar Maritime Authority*). Ni vyema sasa sekta ya usafiri wa nchi kavu na ile ya majini kila moja iwe na sheria ya taasisi yake ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa sekta hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono marekebisho katika kifungu kipya cha 16(a) kifungu kidogo cha pili ambayo yanalenga kutoa nafasi kwa mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa mamlaka husika kufungua kesi na asitozwe fine yoyote mpya mpaka hapo kesi husika

itakapoamuriwa. Hii itatoa nafasi kwa pande zote mbili kuendelea kutumia viwango vya tozo zilizopo mpaka maamuzi yatakapotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inaitaka *SUMATRA* kuwashirikisha wadau wote wa sekta ya usafiri inayokusudia kufanya mabadiliko ya Sheria ya *SUMATRA* au sheria yoyote inayohusiana na usafiri wa majini au nchi kavu na hasa kupitia Baraza lake la Mashauriano (*SUMATRA Consultative Council*). Hii itasaidia kupunguza misugvano ya mara kwa mara kati ya *SUMATRA* na wadau wa sekta ya usafirishaji hasa wamiliki wa mabasi na malori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebicho Katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Kamati Maalum ya Kumshauri Waziri kuhusu misamaha ya kodi iundwe na watalaam waliobobea katika fani ya maeneo tofauti ili kujenga uwezo wa Kamati katika kumshauri Waziri husika kuhusu misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inaelekeza *Tanzania Revenue Authority (TRA)* kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017/2018 ambayo ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2017. Sheria hii imeondoa tozo ya kodi ya ongezeko ya thamani kwa mizigo inayokwenda nchi za nje (*transit goods*). Hata hivyo, mizigo hii imekuwa ikitozwa kodi ya ongezeko la thamani kama imekaa bandarini kwa zaidi ya siku 30 za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza muda wa siku ya mizigo ya namna hii kukaa bandarini ili kuepusha hatari ya kulipa kodi ya ongezeko la thamani kwa mawakala na wamiliki wa mizigo hiyo kama ilivyo kwa nchi nyingine kama vile Afrika Kusini ambayo muda wa kisheria ni siku 180

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa

kibali ili Kamati yangu ya Katiba na Sheria iweze kuufanya uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue na kuwashukuru wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na wajumbe waalikwa wote walioshiriki katika kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba majina yao yote ya namna ambavyo walishiriki wajumbe wangu wa Kamati ya Katiba na Sheria yaingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru watumishi wote wa Ofisi yako ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kasilillah kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Anjelina Sanga, Mkurugenzi wa Idara ya Sheria ya Bunge, Ndugu Pius Mboya, Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) Ndugu Hanifa Masaninga, Makatibu wote wa Kamati yangu waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndugu Danford Mpelumbe, Ndugu Leocardo Kapongwa na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rahel Masima kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha kwamba taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA  
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI, (NA. 3) WA MWAKA  
2017, THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)  
BILL, NO. 3 OF 2017 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2017 [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.3) Act of 2017.

**1.2 Mheshimiwa Spika**, kwa heshima naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunituua mimi binafsi pamoja na Mheshimiwa Tusker Mbogo Mb, kuwa Wajumbe wa Kamati yako maalumu kuhusu biashara ya madini ya Tanzanite. Uteuzi huu unaonyesha imani uliyonayo kwetu na kwa Kamati yote ya Katiba na Sheria katika kusimamia maslahi ya nchi hii na Wananchi waliotutuma katika Bunge hili Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016 Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu Tarehe 05 Septemba, 2017 baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Nane wa Bunge ili iufanyie kazi, na mnamo tarehe 08 Septemba, 2017, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako kwa niaba ya Mtoa Hoja ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mawaziri wengine wanaoguswa na maeneo mbalimbali ya Muswada huu walifika mbele ya Kamati iliyoketi Dodoma na kutoa maelezo kuhusu Malengo na Madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria husika kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.



**Mheshimiwa Spika**, pamoja na timu ya Mawaziri na Manaibu Waziri kufika mbele ya Kamati, kulikua na watendaji mbalimbali kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali zinazoguswa na mabadiliko yanayopendekezwa katika Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ni matokeo yaliyoafikiwa kati ya Kamati na Serikali kuhusu maeneo mbalimbali yanayofanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, (Sura ya 273);
- (ii) Sheria ya Elimu (Sura ya 353),
- (iii) Sheria ya Mtoto (Sura ya 13),
- (iv) Sheria ya Madini (Sura 123),
- (v) Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji (Sura ya 435),
- (v) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Rasilimali za Nchi (Na. 5 ya Mwaka 2017),
- (vi) Sheria ya Petroli (Sura ya 392),
- (vii) Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bodi la Mto Rufiji (Sura ya 138),
- (viii) Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sura ya 413),
- (ix) Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Sura ya 172),
- (x) Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi (Sura ya 219),
- (xi) Sheria ya Mipango Miji (Sura ya 355) na
- (xii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sura ya 148).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 na kuzingatia matakwa ya Ibara ya Nane na Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano inayowapa wananchi nafasi ya kushiriki katika masuala mbalimbali yanayowahusu, Kamati iliwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika

mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**1.4** Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao:-

- i) Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS),
- ii) Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA),
- iii) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF),
- iv) Chama wa Mawakala wa Forodha Tanzania (TAFFA),

## **2.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Jumla ya Muswada huu yapo katika taarifa ya Mtoa Hoja, Waziri wa Katiba na Sheria iliyosomwa leo hapa Bungeni pamoja na maelezo ya Malengo na Madhumuni ya Muswada yaliyomo kwenye Muswada kuanzia Ukurasa wa Kumi na nne mpaka wa Kumi na Saba na kwa faida ya muda naomba nisirudie tena maelezo haya na sehemu hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Kwa msingi huu Mheshimiwa Spika naomba sasa nijielekeze katika Uchambuzi wa Jumla wa Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika Katika Sehemu Kuu Kumi Tatu. Sehemu ya kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Muswada, na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, (Sura ya 273) kwa kukifanyia marekebisho Kifungu cha 6 kwa lengo la kuongeza majukumu ya DAWASA ili kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utendaji wake.

Sehemu ya Tatu inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Elimu, (Sura ya 353). Kifungu cha 15 kinarekebishwa kwa kuondoa aya ya (a) ili kuruhusu kazi za kiutendaji za kuthibitisha Shule ziweze kutekelezwa na Kamishna badala ya Waziri. Kifungu cha 16 kimerekebishwa kwenye vifungu vidogo vya (3), (4), (5) na (7) ili kumpa Mamlaka Kamishna wa Elimu kutoa kibali cha kuendesha Shule. Kifungu cha 60(1) kimerekebishwa kwa kuweka adhabu kwa Mtu yoyote atakayeendesha Shule bila kuzingatia masharti ya Sheria hii.

Sehemu ya Nne inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mtoto, (Sura ya 13). Sehemu hii inarekebisha kifungu cha 3 kwa kuandika upya tafsiri ya maneno “kituo cha kulelea watoto wachanga” na “kituo cha kulelea watoto mchana”. Dhumuni la kuandika upya tafsiri ya maneno haya ni kuondoa utata baina ya tafsiri hizo na kuweka ufafanuzi zaidi.

Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Madini, (Sura ya 123). Kifungu cha 21 cha Sheria hiyo kinarekebishwa ili kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati mashtaka au madai dhidi ya Tume. Kwa msingi huo, Tume imepewa wajibu wa kumtaarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu kusudio la kufungua mashtaka au madai. Lengo la marekebisho haya ni kulinda maslahi ya Serikali.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Rasilimali za Nchi (Na. 5 ya Mwaka 2017). Kifungu cha 3 cha Sheria hii kinafanyiwa marekebisho katika tafsiri ya msamiati “natural wealth and resources” ili kujumuisha Rasilimali za Madini na Mafuta ambazo zinakosekana katika msamiati huo.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Petroli, (Sura ya 392). Kifungu cha 47 cha Sheria hiyo kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta Kifungu kidogo cha (6).

Sehemu Nane ya Muswada inapendekeza kuifuta Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji (Sura ya 138).

Hivyo mapendekezo haya yanatokana na majukumu ya Kisheria ya RUBADA kutelekezwa na Taasisi nyingine. Aidha, mabadiliko ya kisera yameifanya RUBADA kukosa umuhimu wa kuendelea kuwepo. Vile vile, sehemu hii inatamkwa bayana kufutwa kwa Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji. Aidha, inaainisha kuhusu uhamishaji wa mali na madeni ya RUBADA na masuala ya ajira za Watumisni ambapo inapendekezwa kuwa wahamishiwe kwenye Mamlaka nyingine za Umma.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, (Sura ya 413) Kifungu cha 3 kimerekebisha kwa kufuta baadhi ya tafsiri na kuongeza tafsiri nyingine ili kufafanua maneno yaliyotumika katika Sheria. Vile vile sehemu hii inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 16A ili kuwezesha Mamlaka kurejea tozo na ada zilizotozwa chini ya Sheria hii. Kifungu cha 30 kinarekebisha ili kuongeza jukumu jipya la Mamlaka la kufanya utafiti kwenye masuala yanayohusu maslahi ya walaji. Kifungu cha 38 na 40 vinafanyiwa marekebisho ili kuhuisha adhabu zinazotolewa kwa makosa chini ya Sheria hii.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, (Sura ya 172). Kifungu cha 3 kimerekebisha kwa kufuta tafsiri ya neno "Mkurugenzi wa Divisheni" na badala yake kuwa "Mkurugenzi" cheo ambacho kinawiana na Muundo wa Taasisi. Aidha, Kifungu cha 14 kinarekebisha katika Kifungu kidogo cha (1), (2) na cha (3) kwa lengo la kuweka sifa za Mkurugenzi na muhula wa Mkurugenzi. Kwa mujibu wa mapendekezo haya, Muhula wa Mkurugenzi utakuwa kipindi cha Miaka Mitano na anaweza kuendelea tena kwa kipindi kingine kama hicho.

Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Madawa na Vipodozi, (Sura ya 219). Kifungu cha 3 kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya maneno "kifaa tiba". Marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu

hiki yanalenga kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti uchunguzi wa afya na vifaa vya uchunguzi. Sehemu hii inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 105(1)(a) kwa lengo la kuwawezesha watendaji wa maabara (health laboratory practitioners) kufanya kazi kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

Sehemu ya Kumi na Mbili inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mipango Miji, (Sura, 355). Kifungu kipya cha 6A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kumruhusu Mkurugenzi wa Mipango Miji kukasimu Mamlaka yake na majukumu yake kwa wapanga Mji ili waweze kumsaidia katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria husika.

Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, (Sura ya 148). Kifungu cha 6 cha Sheria hiyo kinafanyiwa marekebisho kwa lengo la kumpa Mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha, kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye miradi inayofadhiliwa na Wadau wa maendeleo au mikopo yenye masharti nafuu ambayo mikataba husika ina masharti ya kutoa misamaha hiyo.

### **3.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati kwa umakini mkubwa ilipitia Vifungu vyote Thelathini na Sita vya Muswada huu na kujiridhisha na dhima na muundo wa Muswada. Kamati ilijiridhisha kwamba Vifungu vingi vya Muswada ni Vifungu vya Kimuundo na havikua na madhara katika Maudhui ya Muswada (Construction Provisions). Kwa Mfano, Katika Vifungu 36 vya Muswada, Vifungu karibia Ishirini na Tano havikua na tatizo lolote katika maudhui ya Muswada. Kwa mfano Kifungu cha 1,2,3,5,6,7,8 na vinginevyo.

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya marekebisho katika Muswada huu ni ya kawaida na hayakuleta mjadala wowote kati ya Kamati na Serikali. Kwa mfano, marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, Sheria

ya Elimu, Sheria ya Mtoto, Sheria ya Madini, Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Rasilimali za Nchi (Na. 5 ya Mwaka 2017), Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Madawa na Vipodozi na Sheria ya Mipango Miji. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu marekebisho ya Sheria hizi kwa sababu zilizotajwa na Mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijielekeza katika Sheria ya Petroli, Ufutwaji wa Sheria ya RUBADA, Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Nchi Kavu na Majini, na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Katika Sheria hizi yapo maeneo ambayo Kamati ilitaka maelezo ya ziada kutoka Serikalini kuhusu marekebisho yanayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitoa maelezo ya ziada kuhusu maeneo yanayorekebisha katika Sheria hizi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji. Katika Kifungu cha 16 cha Muswada, kinachobadilisha Kifungu cha 47, Kifungu kidogo cha 6 cha Sheria ya Petroli, Kamati imekubaliana na Serikali kwamba mabadiliko haya yanakusudia kutoa nafasi kwa Bunge kuisimamia vizuri Serikali na hasa kwa kuzingatia utekelezaji wa Mikataba mbalimbali ambayo Serikali imekua inaingia na Wawekezaji mbalimbali katika Sekta ya Mafuta. Kama Bunge litapitisha Mikataba ya namna hii hakutakua tena na dhana ya **“Checks and Balances”** kati ya Mihimili hii ya Dola na hivyo kulifanya Bunge kuwa sehemu ya makosa au matatizo yoyote yanayotokana na Mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ufutwaji wa Sheria ya RUBADA, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utaratibu wa Kisheria uliowekwa kuhusu mali na madeni ya Mamlaka pamoja na maslahi ya Wafanyakazi wa Mamlaka na hasa kipindi hiki cha mpito (Transitional period).

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu marekebisho yaliyokusudiwa katika Sheria ya SUMATRA, hasa Kifungu cha 23, 25 na 26 cha Muswada Kamati ilihitaji maelezo zaidi kutoka SUMATRA kuhusu uhalali wa tozo/faini katika marekebisho haya kupanda kutoka Shilingi laki Tano mpaka faini isiyopungua

Shilingi Milioni Tatu na isiyozidi Milioni 50 kwa makosa yaliyotajwa Kisheria.

**Mheshimiwa Spika**, katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Kamati ilitaka kufahamu Mamlaka aliyonayo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye miradi inayofadhiliwa na Wadau wa maendeleo au mikopo yenye masharti nafuu ambayo Mikataba husika ina masharti ya kutoa misamaha hiyo. Katika Sheria hii Kamati ilitaka kujiridhisha na namna Waziri husika atakavyounda Kamati ya Wataalamu (Technical Committee) ambavyo itamshauri Waziri kuhusu utoaji na ufuatiliaji wa Misamaha hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano ya kina kati ya Serikali na Kamati, Serikali ilikubali kuyafanyia kazi baadhi ya mapendekezo ya Kamati na kuyajumuisha katika Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na hasa katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na Sheria ya SUMATRA.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huu ninaomba sasa nijielekeze katika Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Ujumla.

#### **4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatwa kama ifuatavyo:-

#### **4.1 UFUTWAJI WA SHERIA YA MAMLAKA YA UENDELEZAJI WA BONDE LA MTO RUFUJI (RUBADA)**

- Kwa kuwa Serikali ya awamu ya tano inachukua hatua za kutosha katika kuboresha Taasisi za Umma kama ambavyo ilifuta Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma Mwezi wa Tano Mwaka huu, Kamati inashauri kwamba madeni yanayoachwa na Taasisi inayovunjwa yasihamishiwe katika Taasisi nyingine. Kamati inashauri iundwe Ofisi ya Taifa ya madeni (National Debts Management Office) ambayo itakua na jukumu la kurithi na kusimamia madeni

yote ya Taifa. Utaratibu huu utumike hata katika kusudio la kuvunja Mashirika mengine ya Umma kama RAHCO. Utaratibu huu unatumika katika nchi nyingine kama Kenya.

- Maslahi ya Wafanyakazi yazingatiwe: Kamati inashauri kwamba maslahi yote yanayohusiana na ajira za Wafanyakazi wote wa Mamlaka ya RUBADA yazingatiwe na hasa katika kipindi hiki cha mpito na kwamba kila atakayeachishwa kazi alipwe sawa sawa na Mkataba wake wa kazi na taratibu, Sheria za ajira na Utumishi wa Umma Tanzania.

#### **4.2 KUHUSU SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI WA NCHI KAVU NA MAJINI (SUMATRA)**

Kamati inaishauri Serikali kuandika tena Vifungu vya 25 na 26 vya Muswada ili viseme kwa uwazi (Expressely) kwamba vimekusudia kutoa adhabu iliyotajwa katika Vifungu hivyo kwa makosa yanayotendeka katika vyombo vya Usafiri baharini ambavyo vipo chini ya Merchantile Shipping Act ya Mwaka 2003 na siyo kwa makosa yanayotendeka katika usafiri wa Nchi kavu ambayo yapo chini ya Sheria ya Transport Licensing Act ya mwaka 1973.

- Kama ambavyo Kamati imewahi kushauri siku za nyuma na hasa katika Taarifa yake kuhusu uridhaji wa Mkataba wa Kazi za Mabaharia Tanzania, ni muda muafaka sasa wa kuboresha Sekta ya Usafiri Majini kwa kuwa na Taasisi moja upande wa Tanzania bara itakayosimamia Sekta ya Usafiri wa Majini kama ilivyo Zanzibar ambapo kuna Mamlaka ya Usafiri Majini (Zanzibar Maritime Authority). Ni vema Sekta ya Usafiri wa nchi Kavu na ile ya Majini kila moja iwe na Sheria na Taasisi yake ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Sekta hizi.
- Kamati inaunga mkono marekebisho katika Kifungu kipya cha 16A (2) ambayo yanalenga kutoa nafasi kwa Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka husika kufungua kesi na asitozwe faini yoyote mpya mpaka hapo kesi husika itakapoamuliwa. Hii itatoa nafasi kwa pande zote mbili



kuendelea kutumia viwango vya tozo vilivyopo mpaka maamuzi yatakapotolewa.

- Kamati inaitaka SUMATRA kuwashirikisha wadau wote wa Sekta ya usafiri inapokusudia kufanya mabadiliko ya Sheria ya SUMATRA au Sheria yeyote inayohusiana na usafiri wa majini au nchi kavu na hasa kupitia baraza lake la mashauriano. (SUMATRA consultative council). Hii itasaidia kupunguza misuguano ya mara kwa mara kati ya SUMATRA na wadau wa sekta ya usafirishaji hasa wamiliki wa mabasi na malori.

### **4.3 MAREKEBISHO KATIKA SHERIA YA KODI YA ONGEZECO LA THAMANI**

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba Kamati Maalumu ya kumshauri Waziri kuhusu misamaha ya Kodi iundwe na Wataalamu waliobobea kutoka katika fani na maeneo tofauti tofauti ili kujenga uwezo wa Kamati hiyo katika kumshauri Waziri husika kuhusu Misamaha hiyo ya kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaelekeza TRA kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo ilianza kutumika tarehe 1/7/2017. Sheria hii imeondoa tozo ya kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mizigo inayokwenda nchi nyingine (Ancillary/Transit Goods).Hata hivyo mizigo hii imekua ikitozwa kodi ya Ongezeko la Thamani kama imekaa bandarini kwa muda wa siku 30 za Kisheria. Kamati inaishauri Serikali kuongeza muda wa siku za mizigo ya namna hii kukaa bandarini ili kuepusha hatari ya kulipa kodi ya Ongezeko la thamani kwa mawakala na wamiliki wa mizigo hiyo kama ilivyo kwa nchi nyingine kama Afrika Kusini ambapo muda wa Kisheria ni siku 180.

### **5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia uchambuzi Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba niwatambue na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe Waalikwa wote walioshiriki katika kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha.

**Naomba Majina ya Wajumbe walioshiriki kwenye uchambuzi wa Muswada huu yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).**

- 1.Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa,Mb -Mwenyekiti
- 2.Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti
- 3.Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
- 4.Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb - Mjumbe
- 5.Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe
- 6.Mhe. Makame Mashaka Fom, Mb - Mjumbe
- 7.Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe
- 8.Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb - Mjumbe
- 9.Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
- 10.Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe
- 11.Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe
- 12.Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe
- 13.Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe
- 14.Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe
- 15.Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
- 16.Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
- 17.Mhe.Ussi Pondeza, Mb - Mjumbe
- 18.Mhe.Wanou Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
- 19.Mhe.Tusker Mbogo,Mb - Mjumbe
- 20.Mhe. Ally Salehe Ally,Mb - Mjumbe
- 21.Mhe. Zainab Katimba,Mb - Mjumbe Mwalikwa

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kasilillah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati

za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Masaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Mkurugenzi wa Idara ya Sheria ya Bunge Ndg. Pius Mboya, Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga Makatibu Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Dunford Mpelumbe, Ndg. Leocardo Kapongwa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**

**KATIBA NA SHERIA NDOGO**

**SEPTEMBER, 12 2017**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria.

**MHE. ALLY SALEH ALLY (K.n.y. MHE. TUNDU A.M LISSU - MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisha ya Sheria Mbalimbali Namba 3 wa Mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni kuhusu Muswada huu naomba kulaani tukio la kupigwa risasi mchana kweupe kwa Waziri Kivuli wa Sheria na Katiba ambaye pia ni Mnadhimu wa Kambi yetu Mheshimiwa Tundu Antipas Mughwai Lissu, mchana wa tarehe 7 Septemba, 2017 wakati akitoka Bungeni kutekeleza wajibu wake wa uwakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipolaani tukio kama hilo ambalo limempata Mbunge mwenzetu, tutakuwa

hatujatenda haki kwa kuwa mlolongo wa matukio ya utekaji na uvamizi ambayo mengi yameripotiwa na kuzungumzwa hapa Bungeni ni dhahiri kuwa kati yetu hakuna aliye salama; awe wa upinzani au upande wa chama kilichopo madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu inayofuata naiamini kama nilivyoandika lakini sitaisoma kwa ajili ya amri ya Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelezo ya Jumla Kuhusu Muswada. Muswada huu ulichapishwa tarehe 3 Septemba, 2017 kwenye Gazeti la Serikali Namba 4, Juzuu ya 98 ambapo ni siku mbili kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Bunge ambao umeletwa kwa hati ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Saba wa Bunge lako Tukufu tulipitisha sheria mbalimbali kwa kile kilichoitwa vita kuu ya rasilimali za nchi. Moja ya sheria zilizowasilishwa wakati huo ilikuwa ni Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ikiwemo Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 pamoja na Sheria za Kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Muswada wa Sheria Mbalimbali, ilipitishwa pia Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili (*The Natural Wealth Resources Permanent Sovereignty Act, 2017*). Wakati wa mjadala wa Miswada hiyo kwenye Mkutano wa Saba, tulieleza bayana kutoridhishwa na tabia ya Serikali kuleta miswada katika Bunge lako Tukufu kwa Hati ya Dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwasilishaji kwa Hati ya Dharura, kuwa na kibali kwa mujibu wa Kanuni za Bunge ni wazi kwamba dhana hiyo inaminya uhuru wa kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge kukosa muda wa kufanya tafakuri ya kina kuhusu Miswada ya Sheria iliyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuletwa kwa sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili ya mwaka 2017, kama moja ya sheria ambazo zinafanyiwa marekebisho na Muswada huu ni ishara kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani ilikuwa sahihi kupinga kupitishwa kwa sheria kwa Hati ya Dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni ishara kuwa ndani ya wiki nane (miezi miwili) baada ya kutungwa sheria hizo na kuanza kutumika, zinaletwa tena kufanyiwa marekebisho hapa Bungeni. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshtushwa na itifaki au sheria za kimataifa zilizowasilishwa hapa Bungeni katika Mkutano huu wa Bunge ambazo msingi wa utaratibu wa utatuzi wa migogoro inayotokana na itifaki au mikataba au sheria hizo ifanyike katika vyombo au mabaraza ya uamuzi ambayo yako nje ya Tanzania. Jambo hili ni kinyume cha sheria ambayo imepitishwa katika Bunge hili miezi miwili iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi wa hili ninalolisema ni mkataba wa kuanzisha kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe ambapo Ibara ya 13(2) mgogoro wa pande zinazohusika na Mto Songwe unapelekwa kwenye Baraza la SADC, jambo ambalo ni kinyume cha Sheria ya Mamlaka za Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili ya Mwaka 2017 ambayo sisi Bunge tumepitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hivi karibuni zilifanyika shamrashamra za kuzindua ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Kijiji cha Chongoleani Mkoani Tanga ambapo katika Mkutano huo wa Nane wa Bunge lako Tukufu, mkataba wa ujenzi wa bomba hilo umewasilishwa kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine katika mkataba huo wa bomba la mafuta, Ibara ya 19(2) ambapo endapo kukitokea mgogoro, mgogoro huo

utapelekwa katika Baraza la Usuluhishi la London ikiwa ni pamoja na pande zote kukubaliana na maamuzi ya Baraza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuletwa kwa marekebisho haya mara nyingine tena na kwa njia ya dharura tena, ni ishara kuwa hakuna uratibu mzuri wa shughuli za kiutendaji miongoni mwa taasisi za Serikali. Haiwezekani ndani ya miezi miwili Serikali hiyo hiyo iwe imesahau kuwa yapo masharti ambayo kwa sasa yanatufunga kwenye masuala ya utatuzi wa migogoro inayohusiana na rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Muswada. Sehemu ya Pili ya Muswada, Kifungu cha Tatu na Nne kinafanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Maji safi na Majitaka Jijini Dar es Salaam (*DAWASA*) Sura ya 273. Katika marekebisho hayo, Serikali inasema kuwa inaiongezea majukumu *DAWASA* ili kutatua changamoto za kila mara wanazokumbana nazo. *DAWASA* pamoja na Shirika la Maji safi na Majitaka Dar es Salaam (*DAWASCO*) zinafanya kazi kwa ushirikiano isipokuwa mmoja ni mmiliki wa miundombinu na mwingine ni mwendeshaji wa miundombinu hiyo ya huduma za majisafi na majitaka kwa Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Kibaha na Bagamoyo Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaleta mkakati wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam na si kuiongezea *DAWASA* majukumu. Ikumbukwe kuwa tatizo la majitaka katika Jiji la Dar es Salaam ni kubwa sana na madhara yake ni makubwa ikiwa ni athari za kimazingira na kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam halihitaji siasa nyepesi za kufanya usafi kila Jumamosi kama inavyofanywa hivi sasa. Jiji la Dar es Salaam linahitaji mkakati madhubuti wa kushughulikia kero ya maji taka. Masuala ya kufunga maduka na shughuli za kibiashara kila Jumamosi kwa maelekezo ya Mkuu wa Mkoa ni fikra nyepesi, wakati kuna tatizo kubwa la namna ya kusimamia masuala ya majitaka jijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa DAWASA inatoa huduma ya majitaka kwa wateja 20,000 kwenye jiji la watu zaidi ya milioni nne. Aidha, miundombinu ya majitaka ni mibovu na kwa sasa imekuwa ya muda mrefu wakati kuna ongezeko kubwa la idadi ya watu. Vile vile mabwawa ya kupokea na kuhifadhi majitaka kutoka kwenye majumba ya watu ni ya zamani na kwa sasa yameshakuwa katikati ya makazi, mathalani mabwawa ya Mabibo na Mikocheni, hivyo kuwa kero kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta mpango wa majitaka Jijini Dar es Salaam na majiji mengine ili kuzuia kupatwa na majanga ya kiafya. Kinga ni bora kuliko tiba. Tiba si kuelekeza miundombinu ya majitaka baharini ambapo hilo pia ni kuzidisha matatizo na magonjwa ya milipuko kwani fukwe zetu zinatakiwa kuwa safi na salama muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123. Marekebisho haya yanafanyika ili kumuwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kwenye mashtaka au madai dhidi ya tume ikikumbukwa kuwa Tume ya Madini ilianzishwa katika marekebisho ya Sheria ya Madini katika Mkutano wa Saba wa Bunge.

Kumuwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kwenye mashauri dhidi ya tume katika Sheria ya Madini ni kuongeza urasimu katika utoaji haki nchini huku ikizingatiwa kuwa kuishtaki Serikali kuna mlolongo mkubwa wa masharti ya kisheria na kwa hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa Serikali inakwepa mifumo ya kawaida ya utoaji haki kwa kuongeza urasimu. Kambi Rasmi ya Upinzani iliwahi kueleza kwa kina kuhusu suala la kumpa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia mashauri hata katika taasisi ambazo kimsingi uundwaji wake unatoa haki kwa mamlaka hiyo kushtaki na kushtakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Petroli. Katika Mkutano wa Saba wa Bunge, Serikali iliwasilisha Muswada

wa Sheria Mbalimbali (*Special Supplement No. 4 of 2017*) ambapo pamoja na mambo mengine, Sheria ya Petrol iliifanyiwa marekebisho katika kifungu cha 47 kwa kuongeza kifungu kidogo cha tano na cha sita. Kifungu kidogo cha sita kilichoongezwa kinasomeka kama ifuatavyo na naomba nikinukuu:-

*“Notwithstanding the provision of this Act and any other Written Law, the Agreement under subsection (1) shall only enter into force upon approval by the National Assembly”*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi kifungu hiki kinatoa masharti kuwa makubaliano yote yanayohusiana na masuala ya petroli hayatakuwa na nguvu ya kisheria mpaka yatakaporidhiwa na Bunge. Ni mwezi wa pili sasa tokea Sheria ya Petrol ifanyiwe marekebisho na kuongeza Kifungu kidogo cha sita na kulipatia Bunge mamlaka ya kuridhia mikataba yote ambayo inahusiana na rasilimali ya mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhoji hapa ni kuwa; ni jambo gani limesababisha Serikali kufanya tena marekebisho ya kifungu hicho na kuondoa mamlaka kwa Bunge? Marekebisho ya sheria mara nyingi huletwa baada ya mamlaka za Serikali kupata uzoefu wa utekelezaji wa sheria husika. Suala la kuhoji hapa ni kuwa; ni uzoefu gani ambao Serikali imepata ndani ya miezi miwili baada ya kutungwa kwa kifungu hiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma sehemu ya madhumuni ya sababu za muswada huo, hakuna maelezo yoyote ya sababu zilizopelekea Serikali kuondoa kifungu 47(6) cha Sheria ya Petrol ambacho kililipa Bunge lako mamlaka ya kupitia mikataba ya rasilimali ya petroli kabla ya kusainiwa na Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inaliomba Bunge lako tukufu kukataa pendekezo hili la Serikali; ni lazima sasa Bunge liwe na wivu wa kulinda mamlaka yake. Rejea maoni ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia sheria husika hapa Bungeni. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji (*RUBADA*) Sura ya 138. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina tatizo na mapendekezo hayo ambayo kwa ujumla yote yanafuta uwepo wa Mamlaka ya *RUBADA*. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa Mamlaka hii ya Bonde la Rufiji ilikuwa haina tofauti na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma kwa sababu kwa muda mrefu *RUBADA* lililalamikiwa kuwa dalali kwenye ardhi za wananchi wanaoishi katika bonde hilo, jambo ambalo ni kinyume kabisa na dhana ya uanzishwaji wa mamlaka hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2016/2017, aliweka bayana makampuni makubwa ya kigeni ambayo yamehodhi ardhi na baadhi ya makampuni hayo yakipata ardhi hiyo kwa mgongo wa *RUBADA*. Naomba ninukuu sehemu ya hotuba hiyo:-

*“Mheshimiwa Spika, aidha, Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Rufiji (RUBADA) imetuhumiwa kuwa imekuwa kifanya kazi ya ukuwadi kwa makampuni ya kigeni kutoa ardhi bila kuzingatia taratibu na kusimamia utekelezaji wa ahadi za wawekezaji wanazotoa kwa wananchi katika vijiji mbalimbali.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pendekezo la Muswada huu, ni dhahiri kuwa Serikali imeona kuwa hakuna haja ya uwepo wa watu hao ambao mara kadhaa wamekuwa wakilalamikiwa na wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa kwa sasa haitoshi kuifuta *RUBADA* pekee bali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu malalamiko ya wananchi wanayoituhumu kupora ardhi zao na hatua stahiki kwa wote waliohusika zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nimepata majina hapo ya wachangiaji kutoka vyama vyote, kwa hiyo kwa uwiano tutakaokuwa nao leo nitaanza kuita majina ya wachangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na naomba niungane na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani upande wa Katiba na Sheria kwa kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu alipaswa kuwa hapa, hili ni eneo lake la kitaaluma, lakini kwa sababu ya mipango ya watu wabaya katika Taifa hili hayupo pamoja nasi. Mungu aendelee kumpa nguvu apate nafuu na kupona haraka ili aweze kuchukua jukumu lake muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema, wale ambao wamemuumiza Mheshimiwa Lissu kwa kiwango kile kama ni kijana ambaye hajapata mtoto asipate kabisa na kama ni mtu ambaye ana familia asiisaidie familia yake, *a-paralyse* kila mahali na apate mauti makubwa sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye hoja...

## T A A R I F A

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, kuna taarifa. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, kwa mujibu wa Kanuni ya 154, Mheshimiwa Spika alishatoa pole, kwa hiyo wengine hatuna budi kuacha kuendelea kutoa pole.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, kabla sijakuuliza kama unaikubali hiyo taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, hizi Kanuni tunakumbushana humu ndani kila wakati na ili mijadala yetu iende vizuri, lazima tufuate utaratibu tuliojiwekea wenyewe. Hapa sikutaka kukatisha hata wasoma hotuba, hotuba zao zote zimekuwepo na hayo mambo na nilishakumbusha kuhusu Kanuni hii, sasa tukisema kwamba tutaendelea kuvunja Kanuni tulizojitungia wenyewe inaleta shida kidogo, tufuate utaratibu tuliojiwekea sisi wenyewe.

Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba muda wangu ulindwe na naomba niendelee kwenye hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hoja yangu ya kwanza iko pale kwenye mabadiliko katika Sheria ya Elimu. Nataka nitoe tu ushauri kwamba ni kweli kwamba kama sasa hivi kabla haya marekebisho hayajaja Bungeni kumekuwa na malalamiko mengi sana ya wamiliki wa shule na vituo vya kulelea watoto hata vile vya watu binafsi, kuna masharti mengi sana na mzunguko mrefu kwelikweli ambayo vilevile yanapelekea sura kama kuna mazingira ya rushwa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti yaliyopo kwa watu kumiliki shule binafsi ni makubwa kuliko shule za Serikali. Kwa hiyo nashauri Wizara hii ya Elimu na Waziri mwenye dhamana ajielekeze kusimamia shule za Serikali ziwe bora zaidi, hizi za *private* zinakufa zenyewe tu kwa sababu wananchi walio wengi, maskini, wanategemea shule za Serikali kwa sababu ni bei nafuu zaidi. Hilo ni jambo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; masharti yale yaliyotolewa, ni lazima masharti ya kuanzisha vituo vya kulelea watoto wadogo na wale wenye miaka miwili mpaka mitano vizingatie pia maeneo ya wamiliki kwa sababu unategemea

kuna mtu ana eneo dogo unamtaka awe na ekari saba ndipo awe na kituo hicho, kitu ambacho kwa kweli hakiwezekani. Sheria zifuatwe, mazingira yatofautiane kutoka eneo na eneo kulingana na upatikanaji pia wa ardhi. Hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni hii habari ya *DAWASA*. Bahati nzuri mimi ni Mbunge kutoka Ukonga - Dar es Salaam, ni waathirika wakubwa wa eneo hili. Kwanza kuna mkanganyiko mkubwa kati ya *DAWASA*, *DAWASCO* na halmashauri zetu. Nadhani hata kabla ya kuleta hii sheria ni muhimu mkaangalia, *issue* hapa sio kuongeza majukumu ya *DAWASA*, suala la msingi ni kwamba miradi ambayo *DAWASA* wameanzisha mingi haijakamilika, shughuli ambazo wamepewa hazijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna mwingiliano mkubwa wa mamlaka hizi tatu, kwamba kuna miradi ipo ya *DAWASA*, kuna miradi ipo ya *DAWASCO* na kuna shughuli ambazo zinafanya halmashauri zetu. Kwa hiyo ni lazima kuwe na utaratibu mzuri ambao kimsingi jambo likianzishwa liwe linamalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili la miradi mbalimbali iliyopo ambayo watu wameshakula fedha. Kuna miradi mingi sana imeanzishwa imekufa watu wanakula fedha hawawajibishwi, hawachukuliwi hatua mbalimbali. Maana yake ni kwamba tunaendelea kukosa maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini imetolewa hoja hapa ya Kambi ya Upinzani kwamba majitaka Dar es Salaam ni shida kubwa, mvua ikinyesha dakika mbili tu kila mahali panafurika na wananchi ambao si wastaarabu ndio wanatumia muda huo kwenda kufungulia maji machafu kuingia mtaani. Kwa hiyo tunaugua sio kwa sababu kila Jumamosi ufunge maduka na labda niseme vizuri, sijui kama hata Waziri wa Fedha ameshafuatilia, hii jambo la kufunga maduka Dar es Salaam kwa kweli kwetu ni shida kubwa kweli kweli. Hivi unatumia akili gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mwananchi, mama lishe au baba lishe anafungua asubuhi, ana *dustbin* pembeni amepika chapati, ni siku ya Jumamosi watu wanaweza wakanunua maandazi yao, chapati zao muda ule unamwambia afunge mpaka saa nne na hawa watu hawafanyi usafi. Kwa hiyo wanafunga maduka hata ya dawa, sasa kama umepata shida usiku umeugua unahitaji huduma ya dawa unaambiwa duka lazima lifungwe, hilo duka si chafu. Kwa nini asiangalie mtu ambaye kwa kweli ni mchafu ndiye awajibishwe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii ni amri ambayo tumejaribu kuangalia sijui imeandikwa kwenye sheria gani. Sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali utusaidie mambo kama haya, unapoleta mabadiliko hata kauli za viongozi ambazo hazipo kwenye sheria yoyote katika nchi hii leta tuingize kwenye sheria kama ni lazima. Ili basi mtu akisoma, wananchi wanaenda wanaangalia hivi imeandikwa wapi, Rais amesema wafanye usafi kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi, amekuja Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akaongeza ya kwake, Mkuu wa Wilaya ataongeza ya kwake, sasa hii nchi inaendaje kweli. Kila mtu ni amri tu kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mnavyozungumza habari ya maji Dar es Salaam kuna shida kubwa pia hii ambayo inasababishwa mwende muifayie marekebisho, muhimu zaidi. Kwa hiyo cha muhimu hapa ni kuiwezesha hii *DAWASA* ifanywe wajibu wake; kwamba mvua ikinyesha miundombinu iwe imetengenezwa, imerekebishwa, maji yana maelekezo yake; hicho kitu kwa kweli hakijafanyika na imekuwa ni sehemu ya shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia hapa, hii Sheria ya Petroli hakuna sehemu hapa imetajwa gesi, labda mtanisaidia baadaye, hivi ukizungumza maliasili, gesi haimo? Maana umezungumza hapa madini na petrol, gesi ni sehemu ya maliasili pia, lakini hapa naona kwamba hajizungumzwa. Hata hivyo, imeelezwa jambo ambalo itabidi mtujibu, kwamba juzi na amesema Mheshimiwa Tundu

Lissu wakati akiwa mzima wa afya hapa ndani, kwamba hizi sheria ambazo zinakuja kwa *speed* kubwa na ukiona Kamati hii, si kwamba naituhumu, Kamati imesema inaunga mkono hata mambo mengine haitaki kuangalia kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule Mheshimiwa Mwenyekiti ameenda ameandika maelezo yake kuhusu fidia, kuteuliwa kwenye Kamati, mambo ya msingi hawajaangalia, wangetueleza wao kama Kamati ya Sheria hii ilikuja juzi hapa tukasema imekuja kwa dharura. Kuna mambo mengi nchi hii ambayo tunafanya sasa yaani nguvu kubwa inayotumika leo ya makinikia na vitu vingine vyote ni dharura hii hii imetufikisha hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii Kamati imeshauri nini Serikali kwamba kipindi kijacho hii habari ya dharura tuache, tuzingatie utaratibu tupokee ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, usiangalie chama chake, sura yake, uwezo wake, angalia hoja Mezani. Dharura imetuumiza, imeligharimu Taifa hili na hii tabia inaendelea kujirudia, lakini Kamati wameona muhimu kuandika kujisifia kwenye taarifa yake pale mwanzoni. Naomba ushauri muhimu ukazingatiwe, kwamba ni muhimu waangalie, mambo ya msingi ambayo tumesema yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nimeliona hapa ambalo Msemaji wa Kambi Rasmi amelizungumza ni kitendo cha kuondoa nguvu ya Bunge. Tuliomba kwamba kama sheria; hata mambo ya msamaha wa kodi; kama sheria inarekebishwa, basi Bunge, kwa sababu mikataba hii ambayo mingi imeingiwa katika Taifa hili mikubwa ya mabilioni ya fedha, Bunge limekuwa likinyimwa haki ya kuipitia na kuishauri Serikali vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukaona kuingiza kipengele hiki cha kulazimisha mkataba huo mkubwa uletwe humu Bungeni ili tupate fursa ya kuona sheria hiyo na mikataba mbalimbali. Sasa tena ndugu zangu mnaleta hoja ya kusema muondoe Bunge lisiwe na uwezo wa kuweza kuhoji, hii na yenyewe ni sehemu ya tatizo kubwa zaidi. Ninyi

wenyewe mnasema tunamuunga mkono Rais ili sasa Bunge liwe na meno, Bunge liwe na nguvu kumbe ilikuwa ni *kanyaboya*, ilikuwa ni uongo tu, mmezunguka miezi miwili, mmerudi mnafuta tena fursa ya Bunge kupata sheria mbalimbali na kupata fursa ya kuweza kujadili vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi tukubali, nimeona kuna maneno kuondoa msamaha wa kodi, ni kweli kwamba kuna baadhi ya miradi; hata kule Dar es Salaam tumeathirika; miradi mingi imekwama kwa sababu kuna fedha ya ziada inatakiwa ilipwe ili fedha zitoke kuja kwenye miradi ya maendeleo, lakini shida kubwa iliyopo ni ustaarabu wa Mawaziri hawa ambao tunawateua katika Taifa hili, kwamba wakipata fursa ya kutoa msamaha wa kodi; hatujamsahau Daniel Yona hapa na mmemfunga sijui kifungo cha aina gani kile, yupo; lakini na yeye alitoa msamaha na wengine juzi wamewajibishwa; kwamba wamepuuzia hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachoomba ni kwamba, unaposema Waziri apewe nafasi ya kutoa dhamana, hata kama ataunda Kamati; yaani Waziri ndiye anayepaswa kushauriwa, lakini Waziri huyo huyo ndiye anayepaswa aunde Kamati ambayo itamshauri. Yaani mimi Waitara nataka ushauri sasa, halafu Waitara anatafuta watu wake wanaunda Kamati ya kwake Waitara, ndio wanamshauri, halafu Waitara akipewa ushauri na watu wa Kamati aliyounda anaamua kutoa msamaha wa kodi, sijui hiyo imekaaje.

Kwa hiyo hapa ndipo mahali ambapo kuna mianaya ya rushwa, ndiyo watu wanapitisha *deal/zao*, anatengeneza watu ambao anawajua; kwa hiyo lazima kiwe chombo kingine ambacho hiyo Kamati ya kumshauri Waziri ikishaundwa nani ana-*cross check*? Maana yake haioneshi kwamba itakuja kwenye Kamati yoyote wala itakuja kwenye Bunge hili. Ili sasa umdhibiti Waziri kwamba kutoa msamaha iwe kweli kuna ulazima na mradi ambao ni mkubwa ambao una maslahi makubwa katika Taifa hili ndipo nafasi itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, ikigundulika kwamba Waziri ametoa msamaha kijanja kijanja ambapo yeye mwenyewe ananufaika Sheria iwepo ya kumwajibisha huyu Waziri Waziri kwa mujibu wa Sheria zilizopo, ndipo itamdhibiti; ili ifike mahali mtu akipewa hii nafasi aogope. Kwamba ni kweli mimi nataka nitoe msamaha, huu msamaha ni *genuine*? Una maslahi mapana ya Taifa langu? Je, yeye ni nani ambaye anaweza kumhoji. Haya ni mambo ya masingi sana ambayo yanaweza kuzingatiwa ili haki iweze kutendeka

*Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninachosema hapa tunajadili Wizara ya Sheria na Katiba; kuna mambio ambayo hatuwezi kuacha kuyasema hapa kwenye mjadala huu. Tunapokuwa tunasema kwamba kuna mtu wetu ambaye yeye ni Mwanasheria na ni mtaalam aliyebobea Mheshimiwa Tundu Lissu na alipaswa atushauri vizuri hapa amelala kitandani, maana yake ili tumuenzi Tundu Lissu, haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani...* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara. Waheshimiwa Wabunge, nashindwa kuelewa kwa nini mambo haya, huyo Mheshimiwa Tundu Lissu huwa anakuwepo Bungeni hapa kila siku? Ama unajaribu kusema nini? Tafadhali, nadhani wewe umekwishakuchangia haya mengine yote uliyozungumza hayaingii kwenye *Hansard*, kwa sababu naona unatakla kuleta hoja ambazo hazipo sasa hivi.

Mheshimiwa Tundu Lissu kuhudhuria kwake Bunge ni yeye anapanga siyo wewe unayeitisha *recall* pale kujua kwamba mara ngapi anakuwepo humu Bungeni, kwa hiyo hata leo huna hakika kama angekuwepo ama asingekuwepo. Mimi na wewe siyo Miungu kwa hivyo hatujui

Mheshimiwa Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada ulio



mbele yetu. Awali ya yote napenda nitoe utangulizi kama ambavyo muswada huu unavyosema ni marekebisho ya Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi tu nataka niwape tahadhari Waheshimiwa Wabunge kwamba moja ya majukumu yetu makubwa ni kutunga Sheria na tunapoifanya kazi hii mimi ningependekiza kwamba tuwe makini kwa maana kwamba tuache mitazamo yetu ya vyama, tuangalie wananchi wetu wametuleta hapa tufanye nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi? Uwepo wa hii Sheria ambayo imetungwa kwenye Bunge lililopita leo tunakuja kufanya marekebisho inaonesha kwamba ni jinsi gani hatuko makini katika kazi hii. Ningeomba sana hasa hasa Waheshimiwa Wabunge wa Chama tawala maana wao wanapitisha hizi Sheria kwa sababu tu Serikali ndiyo imeleta wao wanaona ni sahihi kupitisha kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi huku tukisema kwamba hili jambo si sahihi tunakuwa tunaonekana kama sisi ni wapingaji tu. Mimi nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kwamba kuletwa kwa Sheria ambayo tumeipitisha mwezi uliopita leo inaletwa kuifanyia marekebisho, hatuko makini katika kazi hii na tutahukumiwa kwa hili. Huo ni utangulizi nilikuwa naomba niweke sawa jambo hili. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikirejea kwenye *point* hii ya *RUBADA*; naunga mkono kufutwa kwa hii Mamlaka ya Mto Rufiji lakini napingana kidogo na mawazo ya Kamati. Kamati wamesema kwamba wameridhika na hili jambo la ufutwaji wa hii lakini je, ni Taasisi gani imetajwa rasmi kwamba ndiyo itashughulika na majukumu yote yaliyokuwepo *RUBADA*, maana hapa mimi nimepitia nimeona kwamba Serikali itachukua jukumu hili, lakini haijatajwa hata Wizara ipi itashughulikia sasa, kama ni Wizara ya Ardhi,, Wizara ya Maliasili na Wizara gani hasa *specific* haijatajwa kwamba majukumu yale ya *RUBADA* yataelekezwa wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati imependekeza uwepo na Ofisi ya madeni ina maana kwamba hiyo fisi itashughulika na mambo ya madeni tu lakini hii *RUBADA* ilikuwa na shughuli nyingi na hata haya Mashirika mengine ambayo yamependekezwa hapa, kwamba *RAHCO* nayo ielekezwe huko. Hata hivyo, hii *RAHCO* haikushughulika na masuala ya madeni tu yaani jambo ambalo ilikuwa inashulika nayo ni suala siyo la madeni peke yake ambayo yanatakiwa yarithiwe na hii Kampuni au Taasisi hiyo itakayoshughulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona ingetajwa *specific* kwamba hiyo Serikali ambayo imeshauriwa iundwe Ofisi ya madeni, basi siyo madeni peke yake na majukumu mengine yote ambayo yalikuwa yanafanywa na *RUBADA* au na hilo Shirika ambalo litafutwa basi ielekezwe huko. Hilo ndilo lilikuwa jambo ambalo nilikuwa nashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka vile vile nijielekeze kwenye upande wa *DAWASCO* au *DAWASA*. Tatizo la maji taka na maji safi kwa mji wa Dar es salaam si tatizo la *DAWASCO* au *DAWASA tu*, hili ni tatizo la Wizara nzima, kwamba tuko makini kiwango gani katika kuipatia fedha au kufanya utaratibu ili twende na wakati; kwa sababu Jiji la Dar es salaam linakuwa na ongezeko la watu siku hadi siku; sasa, Wizara ina mikakati gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwamba suala a kuiongezea majukumu *DAWASCO* au *DAWASA* si *solution* pekee, kwa sababu *solution* pekee ni kuchunguza kwa nini *DAWASCO* imeshindwa kuetekeleza majukumu yake? Hapo ndipo ambapo Wizara au Serikali kwa ujumla wake walitakiwa waiangalie; kwa sababu lengo la marekebisho haya ya Sheria hizi ndogo ndogo lengo ni kuboresha ili jamii au wananchi wapate huduma ambayo inakusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unapokwenda kuongezea majukumu *DAWASCO* ukaona ndiyo *solution* pekee badala ya kuangalia ni kwa nini tumefeli katika nyanja hiyo, nafikiri hili si jambo sahihi zaidi. Nafikiri kwamba badala

ya kuiongezea DAWASCO majukumu kama ambavyo imetajwa hapa, ipo haja sasa pengine hata kutengeneza taasisi nyingine ambayo itahusika moja kwa moja na masuala haya ya maji safi na maji taka kwa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, sina mambo mengi sana zaidi tu napenda kusema kwamba, naunga mkono mia kwa mia maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, tuyazingatie. Mara zote nataka nirejee Waheshimiwa Wabunge mjue kwamba jukumu letu ni kutunga sheria, haya mambo ya hati za dharura hayatatufikisha popote na sana sana yatatuondolea umakini wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nielekeze masikitiko yangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sijui anajisikiaje kama miezi miwili iliyopita alileta Muswada hapa na ukapitishwa na Bunge leo anauleta tena kuja kuurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliteuliwa kuwa Mawaziri miaka iliyopita wakakosea kidogo inawezekana walishauriwa vibaya na Wanasheria leo wako matatani. Kwa nini huyu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na yeye asiwajibishwe? Ameiaibisha Serikali lakini unaleta Sheria ambazo zinakuja kuja ku-*contradict* na Sheria zingine ambazo zinakuja baadaye. Naamini Sheria hizi zote ambazo zinaletwa huku zinapitia mezani kwako, unazipitia.....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali zungumza na Kiti.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali anazipitia. Wiki iliyopita hapa tulikuwa tunapitisha Songwe

*Convention* na ibara ya 13(3) ilikuwa ina-*contradict* na Sheria ambayo tuliipitisha hapa miezi mwili iliyopita ya *sovereignty of state*. Sheria ile Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati anai-*present* hapa alitetea sana akasema na huu ndiyo utaratibu mzuri wa kulinda rasilimali na Maliasili za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ikaletwa hapa Songwe *Convention* tukaipitisha lakini ndani yake ina Ibara ya 13(3) inayosema kwamba usuluhishi utakwenda kufanywa na *SADC*, halikadhalika leo imekuja kuwa tena vile. Kwa hiyo kwangu naona kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajitathmini kwa namna gani anaishauri Serikali.

Mheshimiwa MNaibu Spika, nikubaliane sana na pendekezo la kuifuta *RUBADA*. Mimi nikiwa kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye Wizara ya Maji mwaka jana kwenye hotuba yangu nilizungumzia, mwaka huu nikaizungumzia; hata juzi wakati nasoma maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Songwe *convention* nilizungumzia namna gani *RUBADA* inalitia hasara Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kufanya majukumu yake *RUBADA* ikawa madalali watu wengi wameongea. Sisi ambao tunapita mara kwa mara pale Rufiji kwenda Lindi na kurudi tunapatwa na wivu kuona namna tunavyoshindwa kulitumia bonde la Rufiji ili kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde lina maji, lina ardhi yenye rutuba inayostawi mzao mbalimbali lakini inafika wakati leo nchi hii tunalalamika kwamba nchi ina njaa, hakuna chakula na wale waliolima maeneo mengine wakapata wanazuiwa wasiuze kwa ajili ya kuogopa kwamba chakula ni kichache wakati tuna bonde zuri la Rufiji lina maji, lina kila kitu. Hawa watu waliendeleze hili bonde lakini badala yake ukienda pale sasa hivi hukuti miwa, hukuti Mpunga, huoni mahindi, utaona ng'ombe wengi wamezagaa kwenye lile bonde ndiyo kitu pekee ambacho nafikiri unaweza kukiona. Kwa hiyo hili naunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hapa kuna marekebisho ya Sheria ya Petrol na Madini. Najuliza na wakati mwingine napata shida labda inawezekana haya yanaletwa leo kutokana na hizi shughuli zilizofanyika mwezi mmoja, miezi mwili, mambo ya makinikia, mambo haya ya hizi Tume za Mheshimiwa Spika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana leo akatokea mtu akaja akatuambia makapi ya mpunga ni dawa tutakuja kutungia Sheria hapa *as if*kwamba hatu-*predict* au hatuwezi ku-*focus* mbele, tunakwenda kwa matukio, Mheshimiwa Rais akitoa *order* ya namna hii inaletwa sheria kuja kubadilishwa, Mheshimiwa Rais akitoa *order* nyingine italetwa sheria tena kuja kubadilishwa. Kwa hiyo tunakwenda kulingana na namna ambavyo matukio yanavyotuoongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu mzuri wa Taifa ambalo tunataka kuendelea ni utaratibu wa ku-*focus* mbele, tutunge sheria ambazo zita-*survive* miaka 20, miaka 50 au miaka 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Deodorus Kamala na Mheshimiwa Omari Mgumba ajiandae

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Naomba nijielekeze kwenye kuchangia kuhusu *DAWASA* na *RUBADA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipoanzisha *DAWASA* ilianzisha kama mkakati wa kuhakikisha kwamba ile sheria ya zamani ya *NUWA* inaboreshwa na ikaanzishwa *DAWASA-Dar es Salaam* na katika miji mingine zikaanzishwa Mamlaka za Maji Mijini. Mamlaka za Maji Mijini kwa kweli nazipongeza zinafanya kazi nzuri sana, na hata *DAWASA* yenyewe nawapongeza. Isipokuwa miaka michache baada ya kuanzishwa *DAWASA* lilikuja wazo kwamba ni vizuri kukawa na *DAWASA* halafu kukawa na watu watoa huduma

nyingine ambao watapangishwa miundombinu, kwa hiyo likaja wazo la kwamba tuwe na Kampuni binafsi ambayo itakuwa inatoa huduma za maji katika Jiji la Dar es salaam, na hapo ndiyo tuliingia mkataba na *Dar es Salaam City Water Services*

Mheshimiwa Naibu Spika, badaa ya *City Water Services* kukiuka mkataba ilibidi Serikali itangaze *order* ya kuanzisha *DAWASCO* ili kazi ambazo zilikuwa zinafanywa na *City Water Services* zifanywe na *DAWASCO*. Kwa hiyo *DAWASCO* ilianzishwa *by order* na kwa sheria hii marekebisho yaliyoko hapa yaliyowasilishwa leo maana yake ni kwamba *DAWASCO* inakufa na shughuli zake zote zinahamia *DAWASA* kama idara. Kwa hiyo, hilo kwa kweli napongeza sana Serikali kwa uamuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu umechelewa kwa sababu kuwa na taasisi hizi mbili tumeingia gharama kubwa sana. Unajua pale *DAWASA* kwa kiasi kikubwa walikuwa wanafanya kazi kubwa ya kutafuta fedha tu kwa ajili ya miundombinu mikubwa, kwa hiyo kwa muda mwingi walikuwa wako ofisini pale kwenye viti vya kunesa nesa zaidi wakati kazi hasa ya kutoa huduma ilikuwa inafanywa na *DAWASCO*; kwa hiyo kwa sasa hivi watafanya kazi zote; kutafuta fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Maji kutoa huduma. Kwa uamuzi huu nawapongeza na itakuwa ni *efficiency* kubwa tunayoitegemea kutokana na maamuzi haya. Naipongeza sana Serikali kwa maamuzi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati tulitembelea Durban kuangalia namna wanavyofanya kazi na tutakuta Durban pale ile *Umgeni Water Resources* inatoa maji kama *bulk* kwa Mamlaka tatu ambazo zinatoa huduma za maji pale Durban.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza, katika mpango huu ambao tunauanzisha leo tukipitisha hapa; kwamba Kanda za *DAWASA* zilizopo sasa hivi ambazo zilikuwa ni Kanda za *DAWASCO* ziimarishwe kama ambavyo *TANESCO* wameimarisha kanda zao ili kusudi maamuzi mengi

na usimamizi mwingi ufanyike kule kwenye Kanda badala ya kufanyika Makao Makuu; hiyo itaboresha mawasiliano kati ya wateja na *DAWASA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia waanzishe vitengo vya dharura, kwa sababu wao ni kama vile hawana. Ningependa wajifunze zaidi *TANESCO*. *TANESCO* wana utaratibu mzuri sana wa kushughulikia mambo ya dharura, wana namba maalum wa kushughulikia wakati wa dharura sasa kuna wakati mabomba yanapasuka, kuna wakati wateja wazuri tu wanakosa maji kwa sababu bomba limepasuka. Naomba sana waimarisha kitengo cha dharura ili kuboresha *response* mara inapojitokeza dharura

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichangia kuhusu *RUBADA*. *RUBADA* ilianzishwa kama taasisi baada ya uamuzi wa kutekeleza au uamuzi wa kujenga mradi wa *Stiegler's Gorge*. Ule mradi wa *Stiegler's Gorge*, kama *project*, ulipokubaliwa na Serikali miongoni mwa masharti yake ilikuwa ni kuanzisha *RUBADA* ili kusudi iwe Taasisi ya kusimamia utekelezaji wa ule mradi. Sasa bahati mbaya sana *RUBADA* ilipoanzishwa ikawekwa chini ya Wizara ya Kilimo na mradi wenyewe kitaalam ulitakiwa uwe chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri hiyo ni kengele ya kwanza. Kwa mujibu wa utaalum ulivyo ule mradi wa *Stiegler's Gorge* ilitakiwa hata *RUBADA* ilivyoanzishwa iwe chini ya Wizara ya Nishati na Madini; tusingepata malalamiko na manung'uniko na kutokuelewana sana kwenye utekelezaji wa ule mradi. Hata hivyo, kwa kuwa sasa Serikali imeamua kuhamishia ule mradi wa *Stiegler's Gorge* kwenye Wizara ya Nishati na Madini maana yake ni kwamba ile *RUBADA* inakuwa imekosa ile *root of origin*, kwa hiyo inakufa kifo cha kawaida

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu ya uamuzi huu naiomba Serikali ifikirie sana namna bora ya kuimarisha *RUBABO*; kwa sababu kualikuwa na *RUBADA* na *RUBABO*; *RUBABO* ni *Rufiji Basin Water Board*, ndiyo nimeilita mimi

*RUBABO.* Sasa hii Rufiji *Water Basin Board* na *RUBADA* zilikuwa zinafanya kazi kwenye bonde lile lile na wakati mwingine walikuwa wanatekeleza majukumu yanayofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa sababu *Rufiji Basin Water Board* bado ipo, napendekeza Serikali ifikirie sana namna bora ya kuimarisha *Rufiji Basin Water Board* kwa sababu tayari *Rufiji Basin Water Board* wanao mkakati wa muda mrefu wa namna bora ya kusimamia matumizi ya maji katika bonde la Rufiji kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza sana, wakati watakapokuwa wanafanya mgawanyo wa mali na madeni ya *RUBADA* wazingatie sana namna ya kuimarisha *Rufiji Basin Water Board* au Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Rufiji ili kusudi bodi hii ya bonde la maji la Mto Rufiji iweze kufanya kazi yake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Mgumba, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja muhimu iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na naunga mkono mapendekezo ya Serikali ya kufuta *RUBADA*, kwa sababu kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 13 ni kwamba uendeshaji wa taasisi hiyo na uwepo wa taasisi hiyo unaongeza gharama zisizokuwa za lazima za uendeshaji wa Serikali kama ilivyoelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kama mnavyofahamu tulipopitisha bajeti hapa tulipitisha pamoja na mambo mengine, trilioni 9.2 kwa ajili ya mishahara peke yake. Sasa kama tunatumia trilioni 9.2 kwa ajili ya mishahara



peke yake, maana yake sehemu kubwa ya bajeti inaelekezwa huko, maana yake sasa ukubwa wa Serikali umepanuka mno, ndiyo maana jitihada nyingi ambazo zimefanyika za kuondoa wafanyakazi hewa na mambo mengine, lakini bado tu tunajikuta tunahitaji trilioni 7.2 huenda ikaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo uamuzi huu wa Serikali wa kuondoa *RUBADA* kwa sababu taasisi nyingine zilizopo za Kiserikali zinaweza kufanya kazi hii iliyokuwa ikifanywa na *RUBADA* ni vizuri tukamulika na maeneo mengine. Kwa leo sitapenda kuyagusia hayo kwa sababu sote tunayafahamu. Kuna suala la utitiri wa taasisi zinazofanya mambo yanayofanana, kuna changamoto za masuala ya Wakala, yote haya yaangaliwe kwa upana wake ili tuone zile taasisi ambazo zipo lakini hazina tija basi tuziondoe na shughuli hizo ziweze kuendelea kufanywa na Serikali, tupunguze matumizi yasiyokuwa ya lazima. Kwa hiyo, naunga mkono uamuzi wa kuondoa *RUBADA* sina shaka shughuli hizo zitaweza kufanywa na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo tu ni kwamba, tunapoondoa *RUBADA* zile mali zilizokuwa chini ya *RUBADA* lazima tuwe makini ili isije ikawa *RUBADA* imeondoka na mali zikaondoka, kwa sababu kwenye *transition* ya kipi kilikuwa chini ya *RUBADA* sasa kitaenda wapi, tusipoangalia basi mambo mengi yanaweza yakaendelea hapo katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu kumpa uwezo Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu masuala ya kutoa misamaha hasa kwa miradi ambayo tunapata fedha ya wahisani na makubaliano kati ya Serikali yetu na wahisani mbalimbali. Ni jambo muhimu kwa sababu, unaposema mradi fulani ulipe kodi lakini fedha hizo ni za mradi ama tumepata sehemu ya fedha hizo kutoka kwa wahisani maana yake unawatoza walipa kodi wa ile nchi ambayo umepata fedha hizo kwa ajili ya miradi yako ya maendeleo, si jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo uamuzi wa Serikali wa kuliona hilo ni jambo jema, tumerudi kwenye mstari. Kwa hiyo naunga mkono hoja hiyo kwa sababu itasaidia kuongeza moyo wa wahisani kutusaidia, lakini pia itapunguza gharama za miradi, pia itaharakisha utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo na tutaweza kuelekea kwenye Tanzania ya viwanda kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kama ilivyowasilishwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ajiandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana nami kupata nafasi kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nijielekeze kwenye *RUBADA*. Nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni ili ufanyiwe maboresho ili lengo hata madhumuni ya kuanzisha ile *RUBADA* yaweze kutimia. Niseme tu kwamba nakubaliana na Wabunge wengine, kazi ya Wabunge ni kutunga sheria lakini hizi sheria tunatunga binadamu, binadamu hamna aliyekamilika. Ndiyo maana tunatunga, tukiona kuna upungufu ni halali Serikali ilete hapa tufanye marekebicho ili iwe na tija ile tuliyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali msife moyo. Mkiona kuna makosa yoyote, kutunga hii sio kwamba ni Biblia au Msahafu kwamba haubadiliki. Wakati wowote kwenye hitaji hilo iletwe, hii ndiyo kazi yetu tumeiomba miaka mitano. Hakuna kazi nyingine, ni hii ya kutunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naunga Serikali mkono sana kwa ajili ya kubadilisha hii Sheria ya *RUBADA*. Kwa kweli kama walivyosema wenzangu *RUBADA* waliacha jukumu lao la msingi kwa ajili ya kuendeleza Bonde la Mto Rufiji wakawa madalali kwa ajili ya kukamata wawekezaji na kuwatafutia ardhi kwa njia ambazo siyo halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano halisi kabisa, kuna kampuni ya uwekezaji wa kiwanda cha sukari inaitwa Morogoro *Sugar*, imekuja kuomba ardhi kupitia *RUBADA* ndani ya Bonde hilo la Rufiji ambalo Bonde la Mto Rufiji maana linakuja mpaka kule Morogoro Vijijini hususan Kisaki, Mkulazi na sehemu nyingine. Wawekezaji hao wana zaidi ya mwaka wa pili hawajapata ardhi kwa sababu walienda *RUBADA* wakalipa hela zaidi ya dola 40,000, *RUBADA* wakaweka mfukoni, halafu *RUBADA* kwa hila wakaja kijijini kwetu kule wanahamasisha wananchi na Serikali za Vijiji itenge ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji tukatenga hiyo ardhi kwa ajili ya uwekezaji tunajua tutapata mwekezaji badala yake *RUBADA* wakija wanatumia nguvu kubwa kulazimisha kuwaambia hii ardhi wanawapa bure bila makubaliano yoyote na kijiji wakati wao wameshavuta. Matokeo yake mpaka leo ile kampuni haijapata hiyo ardhi mpaka pale walipojitambua kuanza kurudi, kufuata taratibu na sheria na kukutana na vijiji husika kwa ajili ya kupata ridhaa ya kupata ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hili wazo la Serikali kuifuta kabisa hii *RUBADA* ambayo sasa ije mamlaka nyingine tunayoweza kuendeleza Bonde letu la Mto Rufiji kwa faida ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri pia Serikali katika hili, kuna wengi ambao walinufaika kupata ardhi kupitia *RUBADA*. Hata hao wawekezaji walionufaika kupata ardhi kupitia *RUBADA* hawajaziendeleza ardhi hizo, badala yake walitumia ardhi hiyo kwenda kukopea kwenye mabenki

mbalimbali na kufanyia biashara nyingine tofauti na lengo halisi walilokubaliana na *RUBADA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali katika hili, pamoja na kuvunja na kuhamisha majukumu haya ya *RUBADA* kwenye Taasisi/Wizara nyingine kupitia mikataba hii, kwa wale wawekezaji wachache ambao walipata ardhi kupitia *RUBADA*, tuone kama walitimiza yale masharti na makubaliano walivyokubaliana kwa ajili ya kuendeleza ile ardhi. Kwa sababu tuna ardhi kubwa imeachwa kuanzia Morogoro Vijijini mpaka Kilombero huko, haijaendelezwa kwa kisingizio kwamba hii ardhi inamilikiwa na mwekezaji ambaye amepata *RUBADA* ana hati kila kitu wakati wakulima na wananchi wengi hawana ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali ikapitia mikataba hiyo tuone ardhi hizo ambazo hazijaendelezwa, taratibu za kisheria zifuatwe kama wamekiuka ni kuitwaa ardhi hiyo irudi Serikalini ikapewa mamlaka hiyo mpya kwa ajili ya kuendeleza ardhi hii kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania badala ya wenzetu hawa wametumia kwenda kukopa na kuendeleza biashara zao ambazo hazina malengo na tija kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili nijielekeze kwenye suala la *transit goods* kuhusu masuala ya *VAT*, ambapo nakubaliana na maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria. Ni vizuri kwamba tukaongeza muda, muda huu wa siku 30 ni mchache sana, hauendani na muda wa wapinzani wetu kama kule Afrika Kusini wana siku 180, Mozambique wana siku 90. Sasa hii inawezekana sasa hivi tuko kwenye ulimwengu wa kibiashara ikawakimbiza watumiaji na wadau wengi wa Bandari yetu ya Dar es Salaam kukimbilia hizi bandari zingine kwenda kutumia kwa sababu ya muda mchache huu ambao tumeuweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali waangalie hili kama kuna uwezekano tuongeze muda kwa ajili ya mizigo inayoenda nchi zingine ili iwe kivutio kwa watu wengi kuitumia bandari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilikuwa na hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupewa nafasi hii, nimeambiwa dakika tatu lakini nilikuwa nina mengi, dakika tatu zinatoshia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani kwa kwa Kamati ya Sheria Ndogo, kwa bahati nzuri nimeshiriki. Pamekuwa na michango mizuri sana kuhusu uboreshaji wa hizi sheria ndogo za *DAWASA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe shukurani kwa Kambi ya Upinzani, kuanzia *page* ya tano mpaka *page* sita safari hii wameandika vizuri sana. Utakuta hata lugha ya vijembe iliyotumika inakubalika. Nimesoma hapa, kufanya usafi kila Jumamosi ni siasa nyepesi lakini pia kufunga biashara kila Jumamosi kwa ajili ya usafi wanasema ni siasa nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linafanyika kwa sababu bahati nzuri mimi nimehudumia sana Jiji la Dar es Salaam. Kuna mifereji ya maji ya mvua mikubwa sana iko kule chini lakini Dar es Salaam *population* imeongezeka, wakati huo kilikuwa Kijiji, ikaja ikawa Mji, ikawa Jiji. Tusipozuia manailoni, karatasi na takataka zile ngumu zitakwenda kujaa kwenye mifereji ya chini ya ardhi kule, ndiyo maana sasa hivi tumeanzisha utaratibu kwamba tukusanye zile takataka ili zibebwe, zikatupwe, zichomwe mahali maalum, zisiendelee tena kuzuia mifereji iliyo huku chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Wabunge wamechangia suala la *DAWASA* na *DAWASCO*, kubwa ni kwamba Mheshimiwa Mbunge Waitara amesema kwamba wakati tunafanya mabadiliko ya Sheria Ndogo *DAWASCO* kuna miradi mingi ambayo wameianzisha,

hawajaikamilisha. Hatuvunji *DAWASCO*, *DAWASCO*, ipo na *DAWASA* ipo. Kwa hiyo, ule utekelezaji wa miradi iliyokuwa imeanzishwa utaendelea mpaka ikamilike na tunaendelea kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hili suala la maji ya mvua, kwamba mvua ikinyesha barabara zinajaa maji, maeneo ya wananchi yanajaa maji. Ni kweli kabisa kwamba miundombinu ya maji ya mvua ni michache kwa sababu Jiji la Dar es Salaam, *population* imeongezeka, majengo yameongezeka. Kwa sasa hivi tumeanza kupata fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji taka na tayari Waziri wa Fedha amesaini mkataba, tumepata zaidi ya dola milioni 100 kutoka Korea na utekelezaji utaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka amezungumzia kwamba tatizo la maji taka si tatizo la *DAWASCO* wala la *DAWASA*, nakubaliana na yeye. Wakati ule Miji yetu ilikuwa kama Vijiji, hakukuwa na haja hiyo, ikaja ikawa Miji, haja haikuwa kubwa, ilipofikia kuwa miji ndiyo tukawa na mashirika ya majitaka, sasa hivi limekuwa Jiji. Kwa sasa ndiyo maana tumeanza, tunabadilisha sheria na kuweka hili jukumu liwe na ufanisi zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kengele ya pili imegonga.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii.

Kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Marekebisho ya Sheria ambayo imewasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitumie fursa hii moja kwa moja kutoa ufafanuzi katika baadhi ya mambo ambayo yamesemwa kuhusu sekta ya elimu na suala ambalo limezungumziwa hapa ni kuhusiana na usajili wa shule binafsi na kwamba wamiliki wa shule wamekuwa na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba Serikali ina utaratibu wa kupokea malalamiko na tumekuwa tunayafanyia kazi kadri ambavyo yanajitokeza. Kwa hiyo, kupitia fursa hii niwaambie wamiliki wa shule za binafsi kama kuna malalamiko yoyote wayawasilishe na nawahakikishia kwamba tutachukua hatua stahiki, kwa sababu moja ya jambo ambalo limesemwa kwamba kuna urasimu na kuna dalili za rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote na wananchi wa Tanzania wote ni mashahidi jinsi Serikali ya Awamu ya Tano inavyopambana na rushwa. Kama kuna rushwa katika sekta ya elimu basi wahusika hawatasalimika. Tunachohitaji ni kupata taarifa ili tuweze kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imesemwa kwamba Serikali iache kuangalia shule binafsi jikite katika kushughulikia Serikali yake. Niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali haiwezi kuacha kuangalia zile shule binafsi kwa sababu zinapaswa kufanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na ni jukumu la Wizara yangu ni kuhakikisha kwamba wamiliki wote wa shule wanazingatia sheria, taratibu na kanuni ambazo tunajiwekea. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuzisimamia na kwa wale ambao wanakiuka taratibu hatua dhidi yao zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii.  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wametenga muda wao na kuchangia. Kwa ujumla Wabunge waliochangia ni Wabunge Nane na Waheshimiwa Mawaziri wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara Mbunge wa Ukonga; Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale; Mheshimiwa Hamidu Bobali; Mbunge wa Mchinga; Mheshimiwa Joseph G. Kakunda, Mbunge wa Sikonge; Mheshimiwa Dkt. Diodorus B. Kamala, Mbunge wa Nkenge; Mheshimiwa Omary T. Mgumba, Mbunge wa Morogoro Vijijini; Mheshimiwa Mary D. Muro, Viti Maalum; na Mheshimiwa Lucia Mlowe Mbunge wa Viti Maalum. Pamoja na Waheshimiwa Injini Kamwelwe, Naibu Waziri wa Maji na Profesa Ndalichako Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, michango yao ni mizuri na sisi tunaizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake bila kumsahau Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa hotuba zao nzuri. Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naomba tu kutoa ufafanuzi wa mambo machache ambayo yamejitokeza wakati wa michango hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja la kwanza na ambalo linajirudia ni hili suala la Hati ya Dharura. Naomba kushauri Waheshimiwa kwamba suala hili la Miswada ya Sheria kuletwa hapa kwa Hati ya Dharura ni suala la Kikatiba. Ibara ya 89 ya Katiba ndiyo inatambua kutungwa kwa Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zitasimamia uendeshaji wa



shughuli za Bunge. Kwa hiyo hili ni suala la Kikatiba, ni halali Kikatiba na limewekwa kwenye Kanuni zetu za Kudumu kwenye Kanuni ya 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusichanganye hati ya dharura kwa maana ya *emergency sijui certificate of emergency*, hii siyo *cerficiface of emergency, it's a certificate of urgency* na Bunge kama alivyosema Mheshimiwa Mgumba, Bunge kazi yake kubwa ni kutunga Sheria. Kwa hiyo sharti hili liliwekwa kwa makusudi kwamba kama kuna mambo ya msingi, ya muhimu yanayogusa jamii ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lisisubiri. Hivi kuna dharura hapo mtasubiri mpaka Muswada uende sijui mpaka miaka mingapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii ipo kwa faida ya wananchi. Hivi kwa mfano; mimi nimesikiliza hapa Wabunge wamepongeza kwa mfano juu ya kufutwa kwa *RUBADA*, imekuwa ni kero. Wabunge wamepongeza hapa juu ya *VAT*, Wabunge wamepongeza hapa karibu kila kitu. Kwa hiyo, haya nayo yangesubiri sijui lini, hamuoni kwamba ni mambo ya maana sana? Kwa hiyo, naomba kushauri kwamba hii Miswada kuletwa hapa kwa hati ya dharura ni halali Kikatiba, ni halali kwa mujibu wa Kanuni zetu lakini pia ni kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo naomba kuitolea ufafanuzi ni suala hili la mikataba tunayoingia kama Taifa na Mataifa mengine. Naomba kushauri kwamba Taifa nalo lina *legal personality* katika Jumuiya ya Kimataifa, lina haki, lina wajibu, linapohusiana na Mataifa mengine. Mataifa hayo nayo ni *sovereign*, yana mamlaka huru, mfano mkiwa na mgogoro na Malawi kwenye matumizi ya Mto Songwe, utamleta Mahakama ya hapa Kinondoni? *It's not possible*, lazima muende kwa mtu mwingine na ndiyo maana hii mikataba ambayo moja tumeiridhia jana hii ya bomba la mafuta na hii ya matumizi ya Mto Songwe inaenda kwenye usuluhisi kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwambia Uganda

kwamba aje hapa kwenye Mahakama ya kwetu hatakubali. Ndiyo hivyo tu. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge mkizisoma zile Sheria tuliacha kwa makusudi kutumia maneno *convention, protocols, statutes* ambazo ndizo sheria na mikataba zinazo-govern mahusiano ya Mataifa na Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni halali hiyo mikataba pamoja na kuwepo kwa sheria hizi ambazo tumezitaja hapa na tulizozipitisha hizi, hiyo mikataba inayohusu uhusiano wa Taifa hili na Taifa lingine iwe kwenye *Regional* yaani Kikanda, iwe *Continental*, halafu iwe *International* iende kwenye hayo Mabaraza mengine ya Usuluhishi na vyombo vingine. Hilo niliomba nilitoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, na zaidi ya hapo, hii mikataba yenyewe mnayozungumza ya mto Songwe na hii ya bomba la mafuta imeingiwa mwezi wa Mei mwaka huu, sheria hizi zimepitishwa mwezi wa saba. Kwa hiyo hata katika hali ya kawaida bado huwezi kulaumu kwamba hivi ilikuwaje? Kwa hiyo, ni halali hizo sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba kulitolea...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu naomba usubiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) nakusudia kuongeza nusu saa. Sasa kanuni inataka niwahoji Waheshimiwa Wabunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda kwa hivyo tutaendelea ili tumalize kazi iliyo mbele yetu. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba kulitolea ufafanuzi hapa ni suala la sheria kutungwa Mkutano uliopita halafu inakuja kurekebishwa hapa Mkutano unaofuata. Ni kama tulivyoshauri hapa, hayo mambo ya msingi yale kama kuna kasoro haziwezi kusubiri mpaka muda fulani upite, lakini ukweli ni kwamba tunayo sheria inayotuongoza kwenye tafsiri ya sheria. Kwa hiyo, tunayo Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambayo ndio sheria ya kwanza kabisa katika sheria inayoitwa *The Interpretation of Laws Act* (Sheria ya Tafsiri ya Sheria).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii Kifungu cha 24 kimesema sheria inaweza ikatungwa katika Mkutano mmoja wa Bunge ikarekebishwa na kufutwa katika Mkutano huo huo wa Bunge, hicho ni Kifungu cha 24 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Kwa hiyo, hii ya kuja baada ya Mkutano mwingine unaofuatia *it is not even a matter of contention*. Naomba kushauri kwamba Waheshimiwa Wabunge walielewe hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwenye zile Sheria ya *Natural Wealth and Resources, (Permanent Sovereignty) Act, of 2017 and Natural Wealth and Resources Contract (Review and Renegotiation) of Unconscionable Terms Act*. Tulizungumza pale kwamba Bunge haliwezi likawa na mamlaka ya kuwa tena sasa linakuja kuidhinisha mikataba humu, ikatu-skip kwenye hii Sheria ya *Petrol* tulipokuwa tunarekebisha ile Sheria ya Petroli *it was just an oversight*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Bunge jukumu lake sasa katika mgawanyo wa madaraka katika Mihimili mitatu ya dola kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ni kuisimamia na kuishauri Serikali inapotekeleza majukumu yake. Majukumu ya kuingia mikataba na mataifa na taasisi nyingine yale yako kwa Serikali kama Mhimili (*Executive*). Bunge likianza na lenyewe kuidhinisha mikataba tutajifunga, sasa nani atamkosoa mwingine? Hiyo kasoro tumeiona, tukasema tuoanishe hii Sheria ya Petroli na sheria hizi nyingine ambazo zinazosimamia rasilimali hizi za nchi. Halafu mnasema ni shida, shida gani jamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wakati fulani ni kutokuelewa. Kwa hiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali yuko hapa Bungeni kwa ajili ya kuwasaidia watu kwenye masuala haya ya sheria, naamini wataendelea kuelewa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala limezungumzwa juu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika maelezo yale nimeeleza kwa nini. Kwa mujibu wa Ibara ya 59(4) Mwanasheria Mkuu wa Serikali amepewa mamlaka, ana haki za kuingia katika Mahakama zote hapa nchini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa turekebishe basi Katiba kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo tunazo sheria kwa mfano Sheria ya *the Office of Attorney General Discharge of Dispute Act*, ya mwaka 2005, kwenye Kifungu cha 17 imetaja Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kwenye shauri lolote linalohusu Bunge, linalohusu Mahakama, linalohusu mali na taasisi au maslahi yoyote ya umma. Kwa mfano, mashirika ya umma yale yanamilikiwa na Serikali asilimia 100, Serikali haiwezi kufanya biashara inasema wewe utakuwepo hapa *TANESCO* kwa mfano, utafanya hiyo biashara. Sasa *TANESCO* ni mtoto wa Serikali akishtakiwa uache kwenda kumsaidia mtoto wako? *That is simple logic. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hii Tume ya Madini inayozungumzwa kwenye Kifungu cha 21 cha Sheria ya Madini, unaona ina mamlaka makubwa sana na inahodhi maliasili na rasilimali za nchi hii. Usipowalinda itakuwa shida sana, ndiyo tukasema basi kama ni lazima inapolazimika *Attorney General* aende kuwatetea, hakuna ubaya. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba mlilikubali hili nalo ni jema tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo yamezungumzwa hapa na hili la, Mheshimiwa Spika alikuwa amelizungumzia hapa lakini inajitokeza. Naomba kushauri hii habari ya migogoro kwenye Vyama vya Siasa, tuna Mhimili wa tatu wa dola ambao ni Mahakama. Hata katika uchaguzi watu wanapofanya Uchaguzi Mkuu kwenye

Majimbo yule anayeshindwa, ambaye haridhiki anaenda Mahakamani, si ndivyo tunavyofanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kazi kubwa ni kuwatetea Wabunge wote wanaoshinda, haijalishi kwamba anatoka kambi ipi, ndivyo hali halisi ilivyo. Sasa kwenye hili kama kuna mgogoro, kuna Wabunge wa Chama cha Wananchi waende Mahakamani, Bunge hili haliwezi kuamua nani awe Mbunge, nani asiwe Mbunge. Nafahamu hivi ninavyozungumza kuna kesi Mahakamani, kwa hiyo hili ni kuleta tu purukushani isiyokuwa na sababu za msingi kwenye chombo hiki, tukitumie chombo hiki kutekeleza majukumu yake ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuhitimisha na nawashukuru tena kwa mara nyingine Wabunge wote mliopata fursa ya kuchangia kwenye hoja hizi, Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge nitawahoji baadaye baada ya kumaliza utaratibu. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria  
Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2017, [The Written Laws  
Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2017]**

Ibara ya 2

Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

Ibara ya 8

Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11

Ibara ya 12

Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18  
Ibara ya 19  
Ibara ya 20  
Ibara ya 21  
Ibara ya 22  
Ibara ya 23  
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA-KATIBU MEZANI:** Ibara ya 25 na Ibara ya 26 zimefutwa na Serikali, Ibara iliyokuwa ya 27 sasa ni Ibara ya 25.

Ibara Mpya ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 26  
Ibara Mpya ya 27  
Ibara Mpya ya 28  
Ibara Mpya ya 29  
Ibara Mpya ya 30  
Ibara Mpya ya 31  
Ibara Mpya ya 32  
Ibara Mpya ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa.

## **T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imepitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2017, *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Act, 2017)*, Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2017, *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.3) Bill, 2017)*, kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge. Wanaokubaliana na hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2017, *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2017)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**



Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zipatazo 12 kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo, (*A Bill for an Act to amend certain Written Laws*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2017, (The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2017 Ulipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu kama Bunge kwenye Muswada huu tumekamilisha. Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuwapongeza Kamati kwa niaba ya Bunge pia Wabunge waliopata fursa ya kupitia Muswada huu na kutoa maoni yao wakati wa mjadala.

Pia niwapongeze upande wa Serikali kwa yale mliyoyaona na kuyaleta ili Bunge liweze kuyafanyia kazi na sasa tuwatakie kazi njema katika utekelezaji baada ya Mheshimiwa Rais kuwa ameridhia sheria hii kwa mujibu wa Ibara ya 97 ya Katiba yetu. Kwa hiyo, tuwatakie kila la kheri katika utekelezaji itakapokuwa imemaliza mlolongo wa kusainiwa na Rais.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwaombe sana, nafahamu Waheshimiwa Wabunge huwa wana majukumu mengi ndiyo maana huwa hawakai humu ndani wote, lakini wale ambao hawana majukumu mengine ni vizuri wakiwepo Bungeni, kwa sababu mambo yanayotokea wakati mwingine yanajirudiarudia kwa sababu hatufuatilii ni mambo gani yanakuwa yalizungumzwa na wenzetu na yakatolewa miongozo na viongozi wetu.

Kwa hivyo, tunakuwa tunarudia jambo hilo kila wakati hata hoja zilizokwishajibiwa tunaendelea nazo, zinakuwa zinarudiarudia na zinataka majibu

yanayorudiarudia. Kwa hiyo tunakuwa sisi wenyewe tunajipotezea ule muda wetu adhimu wa kufanya shughuli nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho, saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.19 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 13 Septemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*